# Nipashe

Jumatatu Julai 22, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579976

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US







## Wanaharakati wakubaliana na Jaji Mkuu, watoa angalizo

UKURASA 2



# JPM hajagusa mawaziri sita

• **Ni** tangu aunde serikali, mmoja amrejesha, Makamba afunguka kutumbuliwa... *Endelea ukurasa 2*



WILLIAM LUKUVI



PROF. JOYCE NDALICHAKO



DK. HUSSEIN MWINYI



JENISTA MHAGAMA



DK. PHILIP MPANGO



UMMY MWALIMU

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**ARDHI KUCHUNGUZWA KWA UFISADI WA KODI**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, ameagiza kupelekwa timu maalum...

UKURASA WA 4

**DAKTARI BINGWA ATANGAZA NEEMA KWA WENYE VITAMBI**

PUNGUA kidogo, punguza kula, utapa-suka! Ni baadhi ya kauli ambazo zimekuwa zikitolewa dhidi ya watu wanaonekana...

## Saa 96 za Majaliwa zilivyoacha machungu


UKURASA 3

## Kasoro uboreshaji wa daftari la wapigakura

UKURASA 2


TAIFA STARS vs KENYA

JULAI 28, 2019 • UWANJA WA TAIFA




HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18, TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

# Wanaharakati wakubaliana na Jaji Mkuu, watoa angalizo

**Na Salome Kitomari**

WANAHARAKATI nchini wameipongeza Mahakama kwa kusikia kilio cha muda mrefu cha kutaka dhamana kwa makosa yote, huku wakitoa angalizo kuhusu utekelezaji wake kuepuka mvurugano kwenye jamii.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wanaharakati hao wamesema lipo tatizo la msingi la mrundikano wa watu wanaosubiri upelelezi wa kesi zao kiasi cha kukaa zaidi ya miaka 10 gerezani na baadaye kukutwa hawana hatia na kuachiwa.

Rais wa Chama cha Wanasheria Tanzania (TLS), Dk. Rugemeleza Nshala, alisema dhamana ni haki ya mtu na chombo chenye mamlaka ya kuitoa ni Mahakama, hivyo ni vyema ikaachwa huru na iangalie vitu vya kuzingatia katika utekelezaji wake.

"Kama kosa ni baya na Mahakama inaona mtu anaweza kukimbia au kuhatarisha usalama, basi Mahakama iamue kwa kuongozwa na busara zake," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Nshala, makosa yote yawe na dhamana, lakini kwa makosa ya mauaji na uhaini yaangaliwe kwa umakini mkubwa, itasaidia kupunguza mrundikano wa mahabusu kwenye magereza mbalimbali nchini.

"Tunaunga mkono kauli hii, tunachosisitiza ni watu wasiwekwe mahabusu kwa muda mrefu upelelezi ufanywe kwa haraka. Watu wengi wanateseka gerezani kwa kuwa wanasubiri upelelezi na kesi zao hazina dhamana wakati ingewezekana kabisa kuwapa dhamana," anasema na kuongeza:

"Kwa mujibu wa haki za binadamu mwenye haki ya kumkamata mwingine na kumuweka ndani na inatumiwa na upande wa mashtaka kwamba upelelezi unaendelea ni kosa sana kwa haki za binadamu, demokrasia, Jamhuri na utu kwa kuwa hakuma mwenye haki ya kunyang'anya uhuru wa mwingine."

Dk. Nshala alisema watu wote hawana hatia mbele ya Mahakama hadi pale watakapotiwa hatiani kwa Mahakama kujiridhisha.

"Hii inachochea majadiliano katika haki ya kesi za jinai, watu wanaamka na kupendekeza adhabu kali, je, wameweka misingi au kinga gani kwa kuzui watu wasibambikiwe kesi? Je, kama wamekamatwa kisiasa au kwa namna yoyote ile ya uonevu?" Alihoji.

Alisema aliyeua na kukutwa na hatia anafungwa kama atakuwa na hatia, lakini kama unatuhumiwa ni ngumu kujua aliyebabikizwa kesi.

Alisema utaratibu huo utasaidia upelelezi ufanyike kwa haraka kwa

INAENDELEA UK. 8

# 6 hawajaguswa tangu wateuliwe na JPM

**Na Salome Kitomari**

IDADI ya mawaziri walioteuliwa na Rais John Magufuli tangu aingie madarakani mwaka 2015 na kudumu kwenye wizara zao imeendelea kupungua toka 19 hadi sita.

Kupungua kwa idadi hiyo kunatokana na uamuzi wake alioufanya juzi wa kumwondoka kwenye Baraza la Mawaziri, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, January Makamba.

Kabla ya kuondolewa kwa Makamba, mawaziri walioanza kazi na Rais Magufuli na kubaki kwenye wizara zao bila kuhamishwa au kutumbuliwa walikuwa saba na waliobaki kwenye nafasi za uwaziri hadi sasa ni 12.

Katika mabadiliko ya juzi, Rais Magufuli alimteua George Simbachawene, kushika nafasi ya Makamba.

Simbachawene, aliteuliwa na Rais Magufuli mwaka 2015 kwa nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Alijiuzulu nafasi hiyo Septemba 7, mwaka 2017, baada ya kutajwa kwenye ripoti ya Kamati ya Bunge kuchunguza biashara ya madini ya tanzanite na almasi.

Kadhalika, Naibu Waziri wake, Edwin Ngonyani, alijiuzulu wadhifa huo kutokana na ripoti hiyo kuonyesha waliingia mikataba iliyoisababishia hasara serikali.

Simbachawene anakuwa waziri wa kwanza aliyejiuzulu wadhifa wake na kurejeshwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa nafasi ya uwaziri, katika kipindi cha serikali ya awamu ya tano.

Katika mabadiliko hayo aliyoyafanya juzi, pia Rais Magufuli amemteua Mbunge wa Nzega Mjini, Hussein Bashe, kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, akichukua nafasi ya Innocent Bashungwa, aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

Bashungwa aliteuliwa Novemba mwaka jana kuwa Naibu Waziri wa Kilimo akichukua nafasi ya Dk. Mary Mwanjelwa, aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri, Wizara ya Menejimenti ya Utumishi.

Kufuatia mabadiliko hayo, Makamba aliandika ujumbe mfupi kwenye ukurasa wake wa Tweeter, huku akiambatanisha na picha aliyopiga na Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi, wakiwa wanacheka.

"Jamani nimeyapokea mabadiliko yaliyofanywa kwa moyo mweupe kabisa kabisa...nitasema zaidi siku zijazo," alisema Makamba katika ukurasa huo.

Naye, Kiongozi wa ACT- Wazalendo na Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kambwe, aliandika kwenye

INAENDELEA UK. 26



Baadhi ya wananchi katika Jimbo la Arumeru Mashariki mkoani Arusha, wakijiandikisha juzi katika daftari la kudumu la wapigakura linaloendelea kufanyiwa maboresho na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) mkoani humo. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Uboreshaji daftari changamoto kibao

**Na Waandishi Wetu**

UZINDUZI wa daftari hilo ulifanyika Alhamisi na utafanyika katika mikoa hiyo miwili kwa siku saba.

**KILIMANJARO**

Wananchi kadhaa mkoani Kilimanjaro bado hawana uelewa wa kutosha juu ya kupaswa kufika katika maboresho hayo.

Erinesti Mallya mkazi wa Kibosho, alisema mbali na kuzinduliwa kwa maboresho ya daftari hilo na kutolewa siku saba kukamilisha zoezi hilo, bado baadhi ya wananchi hawajui ni kina nani wanapaswa kwenda kujiandikisha.

"Wapo baadhi ya wananchi hasa waishio maeneo ya vijijini hawajapata elimu ya kutosha kuwa ni kina nani hasa wanapaswa kujiandikisha kwani mimi nimekuja mpaka hapa kituo cha Majengo Manispaa ya Moshi bila kufahamu kuwa siruhusiwi kujiandikisha tena," alisema Mzee Hamis Ali (62), na kuendelea:

"Hatufahamu lengo la serikali kutufanyia hivi kwani hakuna elimu yoyote iliyotolewa kuanzia ngazi ya kitongoji, sasa tunapata mkanganyiko mkubwa wa kwenda kujisajili hadi leo zimebaki siku nne wala hazitoshi kwenda kwenye vituo."

Mwanamkasi Jumanne, alisema mbali na watu kutokuwa na elimu ya kutosha, bado kuna changamoto ya watoto waliohitimu kidato cha sita na kwenda Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa mujibu wa sheria ambao hawana vitambulisho, hivyo hatima yao haijulikani maana baadhi yao walikuwa shule za bweni.

"Mpaka sasa hatujui hatima ya watoto wetu waliohitimu kidato cha sita 2019 ambao waliojinga na JKT na watakaporejea watakuta zoezi hilo limefungwa, hivyo hawatapata haki ya kikatiba ya kumchagua kiongozi wampendaye," alisema.

Aliiomba serikali kuangalia uwezekano ili watoto hao waweze kujiandikisha hasa wale ambao ndio wamefikia umri wa kupiga kura au ambao walipoteza vitambulisho vyao.

Mwanaisha Juma, mkazi wa Pasua Manispaa ya Moshi, anasema mbali na waliofikisha umri wa kupiga kura kuwa wengi, wanafunzi waliopo shule za bweni hawana vitambulisho vya mpigakura, hivyo ipo haja kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuangalia uwezekano wa watoto hao kupata vitambulisho vya kupiga kura.

Mmoja wa waandikishaji kutoka Masama Kati Wilaya Hai, ambaye hakutaka jina lake lichapishwe, alikiri kukabiliwa na changamoto za baadhi ya wananchi kufika katika kituo hicho pamoja na kadi zao za kupigia kura wakitaka kuandikishwa tena.

"Wapo baadhi ambao wanakuja na kudai kuwa walijiandikisha, lakini tukiwaangalia majina hayapo," alisema na kuongeza:

"Pia katika maeneo ya vijijini baadhi ya wananchi wanashindwa kujisajili kwenye mashine kutokana na mikono yao kuharibika kwa kazi za mashambani."

**MKOANI ARUSHA**

Wakazi wa mkoani Arusha wamejitokeza katika zoezi hilo, huku likikabiliwa na changamoto ndogo ndogo ikiwamo ya vituo vingi vya uandikishaji vijijini kutokuwa na umeme.

Akizungumza jana kwa njia ya simu, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA



Kaimu Mkurugenzi kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Lazaro Msasalaga, akimtunuku leseni za kutumia alama ya ubora na vyeti vya ubora Meneja Masoko kutoka Lake Lubes, Anil Gaur, katika halfa ya ugawaji wa leseni za biashara jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA:GETRUDE MPEZYA**

# Waziri ahimiza uchunguzi ufisadi ardhi

**Na Mwandishi Maalum**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, ameagiza kupelekwa timu maalum kuchunguza Idara ya Ardhi katika Manispaa ya Shinyanga kutokana na idara hiyo kubainika kupunguza kiasi cha fedha kwa baadhi ya wadaiwa wa kodi ya pango la ardhi katika madeni wanayodaiwa.

Mabula alitoa maagizo hayo wakati akifunga mkutano wa siku tatu wa wataalamu wa sekta ya ardhi jijini Dodoma.

Alisema sekta ya ardhi katika Manispaa ya Shinyanga imekuwa na mchezo mchafu wa kuwapunguzia wadaiwa sugu kodi ya pango la ardhi kwa kucheza na mfumo, hivyo kuikosesha serikali mapato kupitia sekta hiyo.

"Manispaa ya Shinyanga kuna madudu ya mchezo wa kupunguza madeni, mtu anadaiwa Sh. milioni 20 halafu anapunguziwa deni lake, hili haliwezi kuvumulika," alisema Mabula.

Mbali na mchezo, Naibu Waziri alisema Manispaa hiyo imekuwa pia ikiandaa hati nyingi kwa udanganyifu na kusisitiza kuwa timu maalum ya uchunguzi lazima ipelekwe ili kubaini udanganyifu huo kwa kuwa manispaa hiyo imetia aibu na kuondoa uaminifu kwa serikali. Kadhalika, Mabula alishangazwa na idara ya ardhi katika manispaa hiyo kushindwa kufuatilia hati za madai ilizowapelekea wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi na kusubiri Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Wilaya kuwakumbusha, jambo alilolieleza kuwa ni kinyume cha taratibu za utendaji kazi.

Kuhusu makusanyo ya kodi ya pango la ardhi tangu kuanza kwa operesheni maalum ya kufuatilia

INAENDELEA UK. 8

# Saa 96 za Majaliwa zilivyoacha machungu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SAA 96 za Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa mkoani Kilimanjaro, zimeacha machungu baada ya kuwasimamisha kazi watendaji wa miradi mbalimbali kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao.

Katika ziara yake ya siku nne ya kutembelea, kukagua, kuzungumza na watendaji, wananchi na kuzindua reli ya mizigo ya kaskazini (Tanga, Kilimanjaro na Arusha) pamoja na daftari la kudumu la wapiga kura, Majaliwa alitangaza 'maumivu' kwa wahandisi 68 wa miradi ya maji nchini ambao serikali imewasimamisha kazi.

Pia, Majaliwa alitangaza kusimamishwa kuendelea na kazi ya ujenzi wa miundombinu ya maji, kampuni 30 pamoja na kuzivunja bodi tatu za watumia maji vijijini zilizopo katika Wilaya ya Same, kutokana na utendaji usioridhisha.

Akiwa Wilaya ya Same, Waziri Mkuu, alimsimamisha kazi kwa muda usiojulikana Mhandisi wa Maji wa Wilaya hiyo, Mussa Msangi, baada ya kumdanganya akafungue mradi wa Maji Hedaru, wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.7 ilhali hautoi maji.

Mradi huo uliojengwa kwa fedha za serikali ulikuwa na uwezo wa kuhudumia zaidi ya wananchi 20,000. Baada ya kumsimamisha kazi, Waziri Mkuu alimkabidhi Mhandisi huyo kwa Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso na kumtaka asiondoke katika mji mdogo wa Hedaru hadi hapo maji yatakapopatikana na uchunguzi dhidi yake uanze mara moja.

Akiwa katika mji wa Hedaru, Waziri Mkuu pia alivunja bodi tatu za watumia maji katika Wilaya ya Same, kutokana na kushindwa kuwajibika na miradi hiyo kugubikwa na hujuma mbalimbali ikiwamo matumizi ya fedha za umma.

"Kamanda wa Polisi mkoa wa Kilimanjaro, (RPC-Hamisi Issah) upo hapa, nitafutie viongozi hao wa bodi za maji na walete kwangu, waniambie kwanini wananidanganya, utaondoka nao hawa," aliagiza Waziri Mkuu akionekana kuchukizwa na kitendo hicho.

Alipomuuliza Mhandisi wa Maji (Msangi) kwanini amemdanganya, alijitetea akisema: "Mheshimiwa, maji yapo, lakini tatizo mradi huu unatumia Solar (umeme wa jua) na kunapokuwa na mawingu, maji yanasumbua."

**WIZI TANI TANO ZA NONDO**


Akiwa katika ziara yake Manispaa ya Moshi ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo cha kimataifa cha mabasi cha Ngangamfumuni, Waziri Mkuu alikutana na hujuma za kuikwamisha serikali kutekeleza moja ya miradi yake ya kimkakati, baada ya watu wasiojulikana kuiba nondo tani tano ndani ya eneo la mradi huo, ambalo tayari mkandarasi ameanza kazi.

Stendi hiyo ya kimataifa ya Ngangamfumuni ambayo tayari serikali imetoa kiasi cha Sh. bilioni tisa kwa ajili ya kuanza ujenzi wake, inajengwa na kampuni ya ujenzi ya kimataifa ya CRJE (East Africa) Ltd., kwa mkataba wa miezi 24.

Hujuma hizo zilimchefua Waziri Mkuu na kuagiza walinzi na mmiliki wa kampuni ya ulinzi iliyopewa zabuni ya kulinda eneo la mradi kukamatwa ndani ya muda usiozidi siku nne kabla hajaondoka mkoani Kilimanjaro.

"Ni aibu serikali kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo halafu wanajitokeza wachache na kuihujumu. Kama walinzi hao hawatapatikana, viongozi wa

INAENDELEA UK. 8

MAHOJIANO MAALUM

# Daktari bingwa atangaza neema kwa wenye vitambi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

PUNGUA kidogo, punguza kula, utapasuka! Ni baadhi ya kauli ambazo zimekuwa zikitolewa dhidi ya watu wanaonekana kunenepa na kuwa na vitambi.

Kauli hizo zimekuwa zikiwasukuma wanaopatwa na changamoto hiyo kusaka mbinu za kupunguza unene, lakini baadhi huchukulia kuwa na kitambi ni fahari na hata ishara ya utajiri.

Wapo wanaoamua kupunguza unene na vitambi kwa kujinyima kula na kuingia katika utaratibu maalum wa kufanya mazoezi ya mwili. Wengine huamua kutumia dawa za kupunguza unene na hata kwenda ughaibuni kufanyiwa upasuaji.

Kwa kuiona changamoto hiyo, Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma imeanza rasmi kutoa huduma ya upasuaji wa kuondoa uzito tumboni.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dodoma juzi, Dk. Martin Sindani (pichani), bingwa wa upasuaji wa hospitali hiyo, alisema huduma ya upasuaji wa kupunguza uzito ambao kitaalamu unaitwa 'Bariatric Surgery', imeanza kutolewa kwenye hospitali hiyo Aprili mwaka huu.

Alibainisha kuwa aina mbili za upasuaji huo ambazo ni upasuaji wa kufungua tumbo na wa matundu kwa kutumia darubini.

"Kwa upasuaji wa kufungua tumbo hadi sasa tumewafanyia wagonjwa watatu na upasuaji wa njia ya matundu kwa kutumia darubini (Laparoscopic Surgery), tulianza mwezi wa Juni na tumefanikiwa kumfanyia mgonjwa mmoja," alisema.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na mtaalamu huyo wa upasuaji:-

**SWALI:** Ni kigezo gani kinazingatiwa kujua kwamba mteja amezidi uzito na anatakiwa kufanyiwa upasuaji huo?

**DK. SINDANI:** Kikubwa hapa ni uwiano wa uzito na urefu. Tunapopunguza uzito, uwiano wa urefu na uzito hutakiwa kutozidi 35.

Kama ni zaidi ya 35, kuna hatua mbalimbali zinafanyika kupunguza, kuna vitengo kadhaa vinahusika ambapo kuna mtaalamu wa lishe na mazoezi tiba.

Kwa hiyo, mtu 'anakuwa-trained' (anafundishwa) kwenye mazoezi na chakula angalau kwa mwaka mmoja, ikishindikana ndio tunamfanyia upasuaji.

**SWALI:** Tatizo la vitambi ni kubwa kiasi gani?

**DK. SINDANI:** Utafiti uliofanywa mwaka 2017 na wataalamu wa Marekani na India unaonyesha wanawake ndiyo wenye uzito uliozidi kuliko wanaume na kwa watu wenye umri kuanzia miaka 40 na kuendelea, wana hatari ya uzito uliozidi.

Kitakwimu duniani inaonyesha kwamba zaidi ya watu bilioni moja wanakabiliwa na tatizo la uzito uliozidi na pia inakadiriwa asilimia 25 ya watu kuanzia miaka 20 na kuendelea, wana uzito uliozidi na kwa kiwango kikubwa ni wanawake. (Dunia mwaka huu inakadiriwa kuwa na watu bilioni 7.714)

Kwa Tanzania, ripoti iliyotolewa mwaka 2016, inaonesha tatizo hilo kwa wanaume ni asilimia 13 huku wanawake ikiwa ni asilimia 36.



Na inaonyesha watu wa mijini ndiyo wanakabiliwa na uzito uliozidi wakati watu wanaoishi vijijini inaonyesha asilimia 10 kwa wanaume na asilimia 26 kwa wanawake.

Kuna vitu vinachangia hasa kwa wanawake zikiwamo homoni. Kiasilia, homoni za wanawake zinaonekana kuchangia sana katika mfumo wa umeng'enyaji wa chakula cha wanga na mafuta.

Lakini pia anapokuwa mjamzito, zile homoni zinachangia uwapo wa mafuta mengi kutokana na mtiririko wa kumeng'enya vyakula. Na (wanawake) ni watu ambao hawafanyi kazi zinazochangia kuunguza mafuta kama wanaume.

Akishajifungua wanasema kwamba lazima ale zaidi ili mtoto apate maziwa ya kutosha. Kuna makabila wanakuweka ndani miezi sita, wanakulisha tu.

Ukija kwenye masuala ya lishe, unabaini sasa huyu mtu ana uzito uliozidi japo wengine wakinyonyesha wanabaki na mwili wa kawaida. Kwa hiyo, ni muhimu kula vyakula ambavyo havitengenezi mafuta mengi mwilini.

Asilimia 70 ya watu wenye uzito uliozidi, wako hatarini kupata magonjwa ya moyo na kisukari. Wanawake wenye hali hiyo wako hatarini kukosa uwezo wa kubeba mimba.

**SWALI:** Gharama za upasuaji huu zikoje daktari?

**DK. SINDANI:** Gharama zinatofautiana kwa sababu tuna aina mbili za upasuaji. Upasuaji wa kufungua tumbo ni Sh. 350,000 na ule wa njia ya matundu ni Sh. 450,000, lakini malipo hayo ni nje ya gharama za vifaa.

Kwa upasuaji huo wa matundu akinunua vifaa moja kwa moja, gharama yake inakwenda hadi Sh. milioni nne.

**SWALI:** Nifanye nini kuepuka kitambi?

**DK. SINDANI:** Unatakiwa kuzingatia mazoezi endelevu na chakula. Lazima ule vyakula ambavyo una uhakika unakitumia mwilini, usile ambacho kitabaki mwilini na matokeo yake kinabadilika na kupelekwa stoo.

Kwa mtu aliyefanyiwa upasuaji, anapaswa kuzingatia ulaji wake kwa kuwa akila zaidi kuna uwezekano wa tumbo kutanuka na kupokea chakula kwa wingi.

**SWALI:** Changamoto zipi ambazo zimekuwa zikiwakumba katika utoaji wa huduma hii?

**DK. SINDANI:** Changamoto kubwa ni gharama za vifaa na upatikanaji wake kwa ujumla. Hata hivyo, mwitikio bado ni mdogo kwa kuwa watu bado hawajajua kwamba huduma hii sasa inapatikana nchini.

Wananchi wafike hapa hospitalini ili si tu kwamba wapate matibabu, bali pia ushauri wa kukabiliana na tatizo hili.

**ALIYEPASULIWA ALONGA**

Mkazi wa Rukwa, Stella Makyao (37), ni miongoni mwa waliofanyiwa upasuaji huo katika hospitali hiyo. Aliiambia Nipashe kuwa Juni 11, mwaka huu, alifanyiwa upasuaji wa kupunguza uzito akiwa na uzito wa Kg 120.

"Upasuaji uliofanyika ni wa njia ya matundu, nilikuwa na kilo 120 lakini sasa nina kilo 89. Huu upasuaji ni mzuri kwa sababu unapona kwa haraka majeraha ya nje, ya ndani ndiyo yanachukua muda," alisema.

"Changamoto ninayoipata kwa sasa ni maumivu ya tumbo hasa nikinywa maji au kula chakula, na uwezo wangu wa kula umepungua, nakula robo ya chakula nilichokuwa nakula awali."

Alisema amefurahi kupunguza uzito kwa kuwa hilo ni tatizo alilokuwa akipambana nalo kwa muda mrefu bila mafanikio.

"Hili tumbo ni kama limesetiwa, ukisema uongeze tu, tumbo lenyewe halikubali, unywaji wa maji na ulaji kwa kweli kwa sasa ni mdogo," alisema.

"Masharti niliyopewa ni kupunguza au kuacha vyakula vya sukari, wanga ambavyo vinafanya mtu anaongezeka uzito kwa haraka sana."

Makyao aliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama za matibabu hayo ili wananchi wengi wamudu gharama zake.

Alisema kuwa licha ya gharama nyingine kulipwa kupitia bima ya afya (NHIF), yeye mwenyewe alilipa Sh. 500,000 ili kutibiwa.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kwa takriban watu bilioni 1.3 duniani wana uzito mkubwa. Kati yao, milioni 600 wana vitambi.

# Wataalamu: Stigler's Gorge itachochea ukuaji uchumi

**Na Mashaka Mgeta**

TATHMINI ya wataalamu wa utafiti kwenye uwekezaji katika mradi wa kuzalisha umeme wa Stiegler's Gorge wamebaini kutokuwapo madhara ya kimazingira yanayopaswa kukwamisha utekelezaji wake.

Ripoti hiyo imetolewa ikiwa imebaki takribani wiki moja kabla ya kuzinduliwa rasmi kwa mradi huo unaotekelezwa katika eneo la Mto Rufiji.

Serikali ya awamu ya tano, imeufanya mradi huo kuwa miongoni mwa vipaumbele vitakavyochochea azma ya kuifanya Tanzania kuwa taifa lenye uchumi wa kati unaochangiwa zaidi na sekta ya viwanda.

Ripoti ya wataalamu hao iliyowasilishwa na wanataaluma watano, Saleh Pamba, Dk. Abubakar Rajab, Abdulkarim Shah, Dk. Magnus Ngoile na Dk. Thomas Kashilila, ikitokana na matokeo ya awali yaliyofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco) na World Wide Fund (WWF) yalionesha madhara yanayoweza kusababishwa na mradi huo.

Akizungumza kwa timu iliyofanya tathmini hiyo, Pamba alisema ilifanyika baada ya kuchapishwa taarifa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kimataifa, zikionyesha kuwapo madhara ya kimazingira kwa mradi huo.

"Hivyo tukaona ni vema tukiwa na wanataaluma wa ndani tufanye tathmini yetu kupitia maeneo yaliyoainishwa kwenye taarifa hizo ili tukibaini usahihi wake, tujue namna bora ya kuishauri serikali yetu," alisema Pamba.

Alisema mradi huo umebainika kuwa utawezesha upatikanaji wa uhakika wa nishati yenye gharama nafuu kwa uzalishaji utakaofanywa na wawekezaji nchini.

Mradi wa Stiegler's Gorge unaotarajiwa kuzalisha umeme wa megawati 2115, umetengewa eneo la takribani asilimia mbili ya kilomita 50,000 za mraba za pori la akiba la Selou.

Pamba alisema ishara za kuonyesha kwamba mradi huo hauna faida kwa nchi hazikuonekana, badala yake mradi huo umebainika kuwa wenye manufaa kadri ya agenda ya kuifanya nchi kuwa ya viwanda ifikapo mwaka 2025.

Pia, alisema matokeo ya tathmini yao yamedhihirisha kuwa mradi huo utafanikisha uzalishaji wa umeme wenye gharama ya Sh. 36 kwa 'uniti' iliyo ndogo zaidi ikilinganishwa na tozo kutoka vyanzo vingine.

Pamba alisema licha ya kuuzwa kwa bei nafuu, nishati hiyo itachochea ufanisi katika sekta za viwanda, madini, umeme vijijini, kilimo biashara na uendeshaji wa reli ya kisasa maarufu kama SGR. Pia mradi huo unatarajiwa kutengeneza ajira rasmi na zisizokuwa rasmi zinazofikia 12,000, kuchochea utalii wa michezo ya majini, upigaji picha na uwekezaji mpya katika nyanja za malazi kama makambi, hoteli na kuwa sehemu ya kuongeza kipato kwa jamii zinazoishi kandoni mwa eneo hilo.

Alisema, uzalishaji wa megawati 2115 za umeme huo utakaoingizwa kwenye gridi ya Taifa, utaongeza idadi ya wanufaika kutoka asilimia 67.5 ya sasa kufikia asilimia 100 kwa mwaka 2025. "Hatua hiyo itawezesha kukabiliana na uharibifu wa misitu kwenye eneo kubwa la nchi," alisema.

Kwa mujibu wa Pamba, imebainika kuwa jitihada za kubuni na kuanzisha mradi wa kuzalisha umeme huo zilianza mwaka 1980 ikiwa ni miaka miwili kabla ya Selou kutangazwa kuwa urithi wa dunia mwaka 1982.

"Kwa hiyo uamuzi uliofikiwa sasa sio mpya, na kwa maana hiyo mashirika ya kimataifa yalitambua nia ya kutumia eneo dogo la pori la Selou kwa ajili ya shughuli nyingine za kiuchumi," alisema Pamba.



Ofisa Mifugo wa Kata ya Bulige, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, Devid Chiloleth, jana akimpulizia dawa ng'ombe wa mmoja wa wafugaji wa kijiji na kata ya Kashishi walipotembelewa na Shirika lisilo la Kiserikali ya Haki na Ustawi wa Wanyama Tanzania (TAPO). **PICHA NA SHABAN NJIA**

# Narco kuongeza ng'ombe kwa asilimia 100

**Na Enock Charles**

WIZARA ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi imesema ina mkakati wa kuongeza idadi ya ng'ombe katika Ranchi za Taifa (Narco) kufikia 30,000 kutoka ng'ombe 15,000 waliopo sasa ili kuongeza uzalishaji wa nyama nchini.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa Wizara ya hiyo, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema kampuni hiyo ina malengo ya kushikilia soko la uzalishaji nyama nchini kwa siku zijazo.

"Lengo letu hapo baadaye Narco ishikilie soko la uzalishaji wa nyama na hata maziwa kwa sababu Narco ina eneo kubwa na ina rasilimali kubwa za kujiendesha yenyewe," Prof. Gabriel alisema.

Katika mkakati huo uliopewa jina Making Narco Great Again, Prof. Gabriel aliwataka wananchi kuona umuhimu wa ranchi hizo na kuonya wanaozivamia na kuchungia mifugo yao bila kufuata utaratibu.

Akizungumzia kuhusu wawekezaji wanaodaiwa na Narco, alisema wizara hiyo inawadai wawekezaji wa ndani zikiwamo kampuni tano zilizokopeshwa mashamba na Narco zaidi ya Sh. bilioni 7.56.

Katika hatua nyingine, Prof. Gabriel alisema wizara hiyo ina mkakati wa kujenga kiwanda cha nyama Ruvu mkoani Pwani kwa kushirikiana na Serikali ya Misri ili kuboresha uzalishaji wa nyama na bidhaa zitokanazo na ng'ombe.

"Tuna mpango ambao tunaendelea kuujadili na Serikali ya Misri ili kiwekwe kiwanda kikubwa pale Ruvu ambapo ng'ombe anaingia asubuhi mchana unapata nyama, unapata pochi, unapata mikanda, unapata viatu siku hiyo hiyo sio kesho yake," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Narco, Paul Kimiti, alisema ranchi hiyo ni mfano kwa wafugaji wa ng'ombe nchini ili waweze kujua ufugaji bora.

"Mashamba haya ya ranchi za taifa ni ya Watanzania na kwa ambao hamjui yalianza na Mwalimu Nyerere mwaka 1974, ni ya kufugia ng'ombe wa mfano ili wengine wapate kujua namna ya ufugaji bora na zilikuwa na ng'ombe 80,000," Kimiti alisema.

# Kijaji ahimiza kuchangamkia huduma bima

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, amewataka Watanzania kuchukulia bima kama hitaji muhimu na kujifunza aina mbalimbali za bidhaa za bima zilizopo sokoni ili wazitumie kujikinga.

Dk. Kijaji ambaye pia ni Mbunge wa Kondoa, alisema hayo akiwa ziarani wilayani Kondoa, mkoani Dodoma.

Alikuwa katika uzinduzi na makabidhiano ya madarasa mawili, ofisi ya walimu na madawati 40 vyenye thamani ya jumla ya Sh. milioni 49 kwa Shule ya Msingi Lusangi iliyopo wilayani Kondoa, vilivyojengwa kwa msaada wa kampuni ya bima ya Sanlum, ambayo ndiyo mtoaji mkubwa wa bima barani Afrika.

"Huduma ya bima inahitajika sana ili kuwawezesha watu kujikinga na majanga yasiyotabirika ya siku za usoni," alisema Dk. Kijaji, na kuongeza kuwa ishara iliyoonyeshwa na kampuni ya Sanlam ya kurudisha sehemu ya faida yake kusaidia miradi ya jamii ichukuliwe kama ishara ya namna gani bima ni muhimu kwa uhakika wa maisha.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kanda ya Afrika Mashariki wa Sanlam Pan-Afrika, Julius Magabe, alisema kampuni hiyo itaendelea kusaidia miradi ya jamii mbalimbali Tanzania.

"Naomba nichukue fursa hii kuwahakikishia kuwa Sanlam tutaendelea kushirikiana na serikali ya Tanzania katika kutoa fedha kwa miradi mbalimbali ya jamii," alisema Magabe, na kuongeza kuwa kampuni hiyo ambayo imesherehekea mwaka 2018 miaka 100 tangu kuanzishwa kwake, iko thabiti katika kurejesha sehemu ya faida yake kusaidia jamii.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Lusangi, Josephine Paul, alisema shule hiyo ilikuwa inakabiliwa na upungufu mkubwa wa madarasa, kwa kuwa madarasa matano yaliyokuwapo kabla ya kutosheleza idadi ya wanafunzi ambayo ni 348.

"Kutokana na mradi huu kukamilika, utakuwa umepunguza changamoto ya upungufu wa madarasa na ofisi ya walimu uliokuwapo," alisema mkuu huyo wa shule.

Nidhamu ya matumizi ya fedha za wafadhili ilimvutia Dk. Kijaji na ujumbe wa Sanlam, kutokana na ujenzi huo siyo tu ulikamilika ndani ya muda uliopangwa, bali zaidi ya Sh. milioni 2.7 zimeokolewa kutokana na kupunguza gharama, fedha ambazo zimewekezwa katika ujenzi wa vyoo wa wanafunzi wa kike na wa kiume. "Sisi Sanlam hatujawahi kushuhudia mradi tunaoufadhili ukisimamiwa kwa umakini wa hali ya juu kiasi hiki," alisema Magabe, ambaye kampuni anayotumikia ina matawi ndani ya nchi 38 barani Afrika, huku huduma zake zikiwa zimesambaa mabara ya Amerika, Asia na Australia.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uongozi Simba chukueni ushauri wa Rage

**KLABU** ya Simba imeripotiwa kwamba inapanga kumpeleka mwanachama wa timu hiyo, Hamis Kilomoni kwenye Kamati ya Nidhamu ya Shirikisho la Soka Tanzania, TFF, ili achukuliwe hatua kwa kosa la kutumia kivuli cha udhamini kudhoofisha timu hiyo.

Wakati Simba wakijipanga hivyo, mwenyekiti wa zamani wa klabu hiyo, Aden Rage ameibuka na kunukuliwa na vyombo vya habari akitoa ushauri wake kwamba, pande zote mbili kukutana na kumaliza tofauti zao.

Rage amesema haoni kama ni afya kwa klabu hiyo kuendelea kubishana kwenye vyombo vya habari, jambo ambalo si mwarobaini wa kumaliza sintofahamu hiyo inayoendelea.

Ni muda mrefu sasa Simba imekuwa ikitunishiana misuli na Kilomoni jambo liloulazimu uongozi wa wekundu hao wa Msimbazi kutoka hadharani na barua kutoka serikalini iliyoweka bayana kwamba Kilomoni sio mdhamini.

Lakini sisi Nipashe tunawakumbusha viongozi wa Simba kwamba, wanapaswa kufahamu Kilomoni ameitumikia timu hiyo toka inaitwa Sunderland si mtu mdogo na badala yake wanatakiwa kukaa na kuzungumza naye.

Hatudhani kwamba kama kuendelea kubishana kila siku kwenye vyombo vya habari kunaweza kuleta suluhisho, kwani ni vyema uongozi wa Simba ukubali kukutana kulimaliza jambo hili kwa busara.


Kwani viongozi wa Simba kuendelea kujibu kila jambo kwenye vyombo vya habari, kulinalifanya kuendelea kukua na hapo baadaye likaleta mpasuko mkubwa.

Klabu ya Simba hivi sasa ipo kwenye wakati mzuri ikipitia kwenye mabadiliko ya uwezekezaji, hivyo huu ni muda muhimu zaidi kwa wadau wote wa klabu hiyo kukaa pamoja na kumaliza tofauti zao.

Simba haipaswi kuendelea kulumbana na mtu mmoja ambaye wana uwezo wa kukaa naye chini ya kuyamaliza, kwani kwa sasa wanapaswa kujiimarisha zaidi katika harakati za kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu na michuano ya kimataita.

Nipashe tunashauri kwamba, uongozi wa Simba ukutane na Kilomoni na kuyamaliza mambo yao kiurafiki, kwani wote wanajenga kibanda kimoja kwanini wagombee fito.

Ifikie wakati sasa, mambo ya ndani ya klabu yamalizwe humo humo, badala ya kutoka nje na kuwanufaisha wengine, hivyo tunashauri uongozi wa Simba kuangalia namna ya kulimaliza tatizo hilo.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kengele ya hatari kwa wachezaji wa Kibongo



Na Adam Fungamwango

**ILIKUWA** inakwenda taratibu, lakini sasa ni dhahiri kuwa klabu nyingi zimeanza kupenda kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi.

Zamani ilionekana kwa Simba, Yanga na Azam tu, lakini taratibu kwa sasa imeanza kuvuka mipaka, klabu hata Biashara ya Mara, Kagera Sugar, Stand United, Mwadui FC, Alliance FC zimeanza kuvutika na wachezaji wa kigeni.

Hata Namungo FC, ambayo imepanda daraja msimu huu imeonekana kufukuzia pia wachezaji wa kigeni. Kwa mara ya kwanza kabisa msimu huu, sijaona zile pilikapilika za Simba, Yanga na Azam kugombea wachezaji wa Kibongo waliowika kama ilivyokuwa huko nyuma.

Nina uhakika kabisa kama ingekuwa miaka ya nyuma, Simba na Yanga zilipokuwa zikipigana vikumbo kugombea wachezaji waliovama vema, basi wachezaji kama Salum Aiyee aliyekuwa Mwadui FC na kuwa wa pili kwenye nafasi ya ufungaji bora nyuma ya Meddie Kagere wa Simba, angezua zogo kubwa la kugombewa na klabu hizi kubwa.

Kulikuwa na wachezaji waliotia fora kama Ramadhani Kapera na Kassim Khamisi wa Kagera Sugar, Raidhin Khafidh wa Coastal Union na wengine wengi, ingekuwa ile enzi ya zamani ingekuwa balaa.

Na hii ilikuwa inasababisha wachezaji hao kujiwekea gharama kubwa usajili kutokana na kuhitajika kwa udi na uvumba na klabu hizo.

Msimu huu haiko hivyo. Pamoja na kupata mafanikio makubwa, lakini Simba, Yanga na wala Azam haikuwa na mpango kabisa na wachezaji hao.

Badala yake zimesajili wachezaji wachache tu wa ndani, na wengi wa nje ya nchi.

Pamoja kwamba kumekuwa kama kuna mpango hivi wa kutaka kuwafanyia wepesi kwa kuwapunguza wageni wawekewe idadi ndogo tu ya kucheza uwanjani, lakini hii haiwezi kuwasaidia bali kuwapoteza zaidi.

Tatizo kubwa la wachezaji wa Kitanzania kwanza kabisa gharama zao wa usajili ni kubwa kuliko uhalisia wa uwezo wao wa kawaida.

Pili ni kwamba wachezaji wengi wa Kibongo hawana mwendelezo wa uwezo wao. Leo anaweza kucheza vizuri, kesho akawa vingine kabisa isivyotarajiwa.

Lakini pia mara nyingi ni wachezaji wa msimu. Yaani msimu huu anaweza kufunga magoli 19, lakini msimu ujao akashindwa kufikisha japo magoli 10 tu, akafunga manne au matano.

Wengi wao wanabweteka mapema na sifa za mashabiki mitaani na kushindwa kujituma na kufanya mazoezi kwa bidii baada ya hapo.

Kingine ni kwamba wachezaji wa Kitanzania wanakosa nguvu, stamina na pumzi, na hii inatokana na kutopenda mazoezi magumu, badala yake huetegemea zaidi vipaji vyao tu.

Kwa sasa soka duniani limebadilika sana, nguvu hutumika zaidi na mifumo kuliko vipaji binafsi, hivyo klabu kubwa kama za Simba, Yanga na Azam zinapenda kusajili wachezaji wa nje ya nchi kwa ajili ya kufanya vema kwenye mechi za kimataifa.

Klabu hizo tayari zimeshagundua kuwa ili ziweze kufanya vema kwenye michuano hiyo ni lazima ziwe zaidi na wachezaji wa nje na wachache tu wa ndani.

Hii ndiyo imesababisha msimu huu wa usajili usiwe mzuri sana kwa wachezaji wa Kitanzania.

Kilichobaki sasa kwa wachezaji hao inafaa kukaa na kujitafakari na kuangalia udhaifu wao ambao nimejaribu kuuelezea.

Kingine ni kuondoka nchini kwa kwenda kucheza soka nje ya nchi kwenye klabu mbalimbali na kukutana na changamoto ili kujijengea uwezo wa kupambana.

Na hata wale ambao watakaobaki, wajaribu kubadilika, kwani ukiona hata Biashara ya Mara na Namungo FC wanatafuta wachezaji wa kigeni, hii si dalili nzuri kwa mustakabali wao wa baadaye na nchi nzima.

Ikumbukwe kuwa klabu hazilazimishwi kusajili wachezaji wa nje, bali wanafanya hivyo kutokana na mahitaji na kama siku wakijirekebisha, tutaanza kuona klabu hizo hizo zikipunguza kusajili wachezaji kutoka nje.

**MJADALA**

# Kundi la Stars AFCON si gumu, wala jepesi




**Na Adam Fungamwango**

**KUELEKEA** kwenye fainali za Mataifa ya Afrika 2021, timu ya Soka la Tanzania Taifa Stars imewekwa kwenye Kundi J, ikiwa na timu za Tunisia, Libya na Equatorial Guinea.

Baada ya Shirikisho la Soka Afrika kupanga makundi hayo, Watanzania wengi wamegawanyika sehemu mbili.

Kundi la kwanza linaona kuwa ni kundi gumu, hasa ikizingatiwa kuna timu kigogo kama Tunisia ambayo mara nyingi huwa kufuzu kwenye fainali kwake ni kama ada.

Watanzania wa kundi hili wanaona kuwa hata Libya ni moja kati ya timu ngumu kwa sasa na inakuja juu kisoka, huku Equatorial Guinea ikionekana kama si nchi mchekea sana na inaweza ikafanya maajabu, hasa ikizitiwa kuwa ni moja kati ya nchi za Afrika Magharibi ambazo zina wachezaji wengi wanaocheza nje ya nchi, japo kwenye madaraja ya kati.

Wasiwasi wa wabongo hao pia unatokana na kufuzu kwa Stars kwenye michuano iliyomalizia kuwa kulikuwa kwa tabu mno, licha ya kundi la kufuzu kuwa mchekea likiwa na timu za Uganda, Lesotho na Cape Verde.

Wanatanabaisha kuwa kundi hili ni gumu zaidi kuliko lile lililopita na kama ilisubiri hadi mechi ya mwisho kufuzu, basi wana wasiwasi na kundi hili kama Tanzania inaweza kushika nafasi mbili za juu.

Kundi la pili ni lile ambalo linaona kuwa hili ni kundi rahisi mno na halitoipa shinda Stars kufuzu.

Na wanaona Tanzania inaweza tena kucheza fainali za AFCON mwaka 2021.

Sababu wao wanaitazama Tunisia tu kuwa ndiyo timu tishio na zilizobaki, Libya na Equatorial Guinea zote hizo zipo kwenye levo za Stars.

Ukizisikiliza na kuchambua mantiki za mashabiki wa pande zote mbili utaona kuwa wote wako sahihi. Kundi J ambalo Stars imetupwa binafsi naliona si gumu na wala si jepesi.

Na sababu ni hizi ambazo naziainisha. Ukiangalia kwenye fainali za AFCON kwa sasa imedhihirika kuwa soka la Afrika kwa sasa linashabihiana. Si kama zamani tena. Hakuna timu kubwa wala ndogo.

Timu vigogo vilivyokuwa vikiogopwa huko nyuma kama Cameroon, Nigeria, Ghana, Misri, na zingine zimeonekana kuteseka na kuchezeshwa 'kindumbwendubwe' na timu za mataifa ambayo zamani yalionekana si lolote si chochote kwenye soka.

Kwenye mechi ambazo mashabiki walitarajia timu fulani ifungwe magoli mengi, ikawa kinyume chake.

Kwa kile kilichoonekana ni kwamba Timu ya Taifa ya Tanzania inatakiwa iwe na maandalizi kabambe, pamoja na wachezaji wenye uwezo mkubwa wa kupambana, wenye vipaji na wala si tena kucheza kwa kuangalia historia.

Kama maandalizi ya kiufundi na kisayansi yatafanyika, kuteua wachezaji ambao wako kwenye viwango vizuri kwa wakati huo, hakuna kitakachoshindikana hata kama Tanzania ingewekwa kundi moja na Senegal, Algeria na Nigeria.

Hii ina maana ugumu wa kundi utatokana na wabongo wenyewe watakavyojipanga kuanzia serikali, Shirikisho la Soka nchini (TFF), benchi la ufundi na hata wachezaji wenyewe. Kama haya yote hayatafanyika, basi itakuwa ni kazi bure tu.

Kwa sasa soka la Afrika ni kujiandaa kisawa sawa tu, hakuna kundi gumu wala jepesi kwa sababu hata Madagascar kwa sasa si timu mchekea tena.

Haitakiwi kudharau timu wala kundi kwani Madagascar imewafunza wengi, hivyo hata timu kama Equatorial Guinea si ya kuiendea kichwa kichwa tukidhania kuwa itakuwa ni mechi nyepesi.

Kwa maana hiyo haitakiwi Stars iende kucheza michuano hiyo ikiwa inadhani kuwa kundi hilo ni gumu kwa sababu inaweza kuingia uwanjani wachezaji wakiwa na woga.

Na wala haitakiwi kwenda ikidharau kuwa ni jepesi kwa sababu wachezaji wataingia na dharau na kukutana na kitu tofauti uwanjani kama vile timu zilipokuwa zikikutana na Madagascar AFCON.

Na kwa bahati nzuri mechi zitakuwa ni nyumbani na ugenini, basi itumie zaidi uwanja wa nyumbani kuhakikisha kuwa inapata ushindi kwenye mechi zote tatu bila kujali inacheza na nani.

Kikubwa ni kujipanga kisawawasa kiufundi zaidi na kuweka siasa pembeni.

**BUGANDO MEDICAL CENTRE**

Consultant and Teaching Hospital

## ADVERTISEMENT FOR

## Invitation for Pre-qualification

**Date: 22nd July, 2019**

1. The Bugando Medical Centre has set aside funds towards the cost of the Supply of different goods and it intends to apply part of the proceeds of this funds towards the payments under the contract for:
   i. Supply of Consumable medical supplies & Equipment Tender no. BMC/HQ/G/2019-2020/02
   ii. Supply of Dressing, Bedding, Uniform and Line material Tender no. BMC/HQ/G/2019-2020/03
   iii. Supply of Medicines(drugs) Tender no. BMC/HQ/G/2019-2020/06
   iv. Supply of Laboratory reagents ,chemical,& equipment Tender no. BMC/HQ/G/2019-2020/09
   v. Supply of Orthopedic material Tender no. BMC/HQ/G/2018-2019/12
   vi. Supply of Dental consumables Tender no. BMC/HQ/G/2019-2020/14
   vii. Supply of Radiology material Tender no. BMC/HQ/G/2019-2020/15
   viii. Supply of Ophthalmology material Tender no. BMC/HQ/G/2019-2020/17

   The Bugando Medical Centre intends to pre-qualify Applicants for listed tenders above to be used for the FY 2019/2020.

2. Pre-qualification will be conducted through the procedures specified in Regulation 119 of the Public Procurement (Regulations– Government Notice 446 of 2013, and is open to all Applicants as defined in the Regulations.

3. Interested applicants may obtain further information from and inspect the pre-qualification documents at the ***Secretary of BMC tender board H4 Block P.O BOX 1370 Mwanza from 7:30 am to 15:30 pm local time*** on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.

4. A complete set of pre-qualification documents in English may be purchased by interested Applicants on the submission of a written application to the address given under paragraph 4 above and upon payment of a non-refundable fee of **[Fifty thousand only, TSH 100,000/=].** Payment should be by Cash deposit into ***BMC Health Service Fund account no. 01J1051393600 CRDB*** bank and bring original pay slip

5. All applications one original plus **One copy,** properly filled in, and enclosed in plain envelopes properly written the name of the tender, address, time and the word **"DO NOT OPEN BEFORE"** mentioned time of the deadline and must be delivered to the address ***Secretary of BMC tender board H4 Block P.O BOX 1370 Mwanza at or before 10:00 am local time on 5th August, 2019.*** Applications will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Applicants' representatives who choose to attend in the opening at the **Administration Block H4 Conference Hall.**

6. Late applications, portion of applications, electronic applications, applications not received, applications not opened and not read out in public at the tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**Prof. Dr. Abel N. Makubi**
**Director General**
**P.O Box 1370,**
**Mwanza, Tanzania**
**Telephone 2540610/5 or 2500513**
**Fax: 255-028-2500799**
**Email: info@bugandomedicalcentre.go.tz/ hospbugando@gmail.com**

XXXXXXXX

# Uboreshaji daftari changamoto kibao

INATOKA UK. 2

Ngorongoro, Raphael Siumbu, alisema wananchi ambao kadi zao za kupigia kura zilikuwa zimepotea na kuwa na kasoro pamoja na waliokuwa hawajafikia umri na kuhama makazi, wamejitokeza kujiandikisha katika vituo mbalimbali.

Alisema licha ya wengi kujitokeza, lakini wengi wao ni wafugaji na hawajui kusoma na kuandika, hali iliyosababisha maofisa uandikishaji kutumia muda mwingi ili kupata taarifa zao sahihi.

"Licha ya wananchi kujitokeza kwa wingi, tumekabiliwa na changamoto ndogo ndogo ikiwamo karatasi za kujiandikisha kuisha kwa baadhi ya vituo, japo tumewasiliana na tume na tumetatua changamoto hii," alisema.

Pia alisema maeneo ya wafugaji mengi hayana umeme, hali inayowaladhimu kupeleka jenereta ili huduma iendelee hadi usiku.

Alifafanua kwamba wanalazimika kupeleka jenereta kutokana na hali ya hewa, ambayo jua haliwaki la kutosha na kusababisha taa za sola walizopewa na NEC kuzimika muda mfupi.

Ofisa Mwandikishaji Jimbo la Arumeru Mashariki, Emmanuel Mkongo, alisema mwitikio ni mkubwa kwani katika kata alizotembelea za Akheri, Kwarisambu, na Poli wananchi wamejitokeza kwa wingi hasa vijana wa miaka 18 ambao wanajiandikisha kwa mara ya kwanza.

Pia katika kata hizo mwitikio mkubwa zaidi katika maeneo yenye mkusanyiko wa watu unaotokana na shughuli za kibiashara wanazofanya tofauti na maeneo ya pembezoni ambako mwitikio ni mdogo.

Mkongo alisema hakuna changamoto zaidi ya moja ya mashine za BVR zilizokuwa na hitilafu na kushindwa kuchapa vitambulisho ilitatuliwa na wataalamu wa Tehama.

"Kama nilipopita kituo cha Chuo cha Mifugo Tengeru Lita nilikuta BVR KIT haifanyi kazi na kwa sasa wataalamu wetu wa Tehama wameshatatua na wananchi wanaendelea kupata huduma," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Arusha DC wilayani Arumeru, Dk. Wilson Mahera, alisema zoezi linaendelea vizuri japo kuna changam to ya uelewa mdogo wa wananchi, lakini wanaendelea kufanya matangazo na kutoa elimu.

"Lakini kuna sehemu kulijitokeza wananchi wengi na kukawa na uhaba wa vifaa, hivyo tuliwasiliana na tume na wakatuletea vifaa na sasa tunaendelea na zoezi vizuri bila shida yoyote," alisema.

Mratibu wa Uchaguzi Mkoa wa Arusha, Elgin Nnkya, alisema zoezi hilo kwa ujumla kwa mkoa huo linaendelea vizuri na changamoto zinazojitokeza wanajitahidi kuzitatua kwa wakati.

**Imeandikwa na Mary Mosha, Moshi na Cynthia Mwilolezi, Arusha**

# Saa 96 za Majaliwa zilivyoacha machungu

INATOKA UK. 3

kampuni husika wakamatwe ili kutoa ushirikiano wa sehemu walipo wafanyakazi wao. Wananchi wa Moshi mmetukatisha tamaa, naagiza wasakwe popote walipo," aliagiza.

**AKATAA KAMPUNI ZA UWAKALA**

Pia, Waziri Mkuu amepingana na uamuzi wa Kampuni ya Mohamed Enterprises (MOETL) inayosimamia Kiwanda cha Hassan Sisal Estates kilichopo Wilaya ya Same, kuendelea kuzitumia kampuni mbili za uwakala ya Unique na Upami, kwa kuwa zinalalamikiwa na wafanyakazi kupunja jasho lao.

Kutokana na malalamiko ya wananchi aliyokutana nayo kwenye mabango katika kiwanda hicho, Majaliwa alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu, Jenista Mhagama kwenda kushughulikia haraka malalamiko ya wafanyakazi 500 wa kiwanda hicho.

**MADC MSIOMBE PESA**

Vile vile, ameonya asijitokeze mkuu yeyote wa wilaya kuomba fedha kwa wakuu wa idara, wakurugenzi, taasisi au kitengo chochote kwa maslahi yake binafsi, lakini anaruhusiwa kuagiza kupatiwa taarifa kwa muda anaoutaka yeye. "Ma-DC wangu msiombe pesa ila mnaruhusiwa kisheria na kwa mamlaka mliyoongezewa kikatiba ya kuwa mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama, aagiza taarifa kwa muda unaotaka wewe upatiwe, lakini usiombe tu pesa," alionya.

`Chuma ulete'

Moja ya mambo yaliyomshtua ni kuelezwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, kwamba imani za kishirikina katika wilaya hiyo zinazohusiana na madai ya kuchukua fedha za watu wengine kwa kwa kutumia nguvu za giza maarufu kama 'chuma ulete' zinaathiri utendaji wa serikali.

Dk. Mghwira alimweleza Waziri Mkuu kwamba wilaya hiyo inatishiwa na imani za kishirikina kiasi cha kuathiri shughuli za maendeleo.

Baada ya kuelezwa hayo, Majaliwa alisema serikali haiamini uchawi, lakini kama hali ikiendelea hivyo inaweza ikasababisha wafanyakazi 888 ambao wanahitajika kuajiriwa katika Wilaya ya Same ili kukabiliana na upungufu uliopo, kukataa kwenda kufanya kazi huko.

"Hiyo chuma ulete sio jambo jema kabisa na hali ikiendelea hivi ni balaa. Ni vizuri mkashirikiana na wazee, mkakaa nao na mkazungumza nao wasaidie kutatua jambo hili ili athari zilizotokea zisijitokeze tena, alishauri Waziri Mkuu.

# Waziri ahimiza uchunguzi ufisadi ardhi

INATOKA UK. 3

wadaiwa sugu wa kodi hiyo, Mabula alisema zoezi hilo limekuwa na mafanikio makubwa kwa kuwa wizara imefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 20 ndani ya mwezi mmoja, jambo ambalo halijawahi kutokea.

Kwa mujibu wa Mabula, wizara inaanza utendaji wa kimatokeo badala ya kusubiri hadi mwisho wa mwaka ndiyo ianze ufuatiliaji wa wadaiwa kodi ya pango la ardhi na kubainisha kuwa lengo katika mwaka wa fedha 2019/2020 ni kukusanya Sh. bilioni 180.

Katika hatua nyingine, Mabula ameziagiza halmashauri za wilaya nchini kuainisha maeneo yote ya wazi kwa lengo la kubaini maeneo yaliyovamia na kutuma taarifa ya matokeo ya zoezi hilo wizarani ifikapo Oktoba 1, 2019.

Mabula alisema maeneo mengi ya wazi yamevamiwa kwa kuwa baadhi ya watendaji wa sekta ya ardhi wasio waaminifu wameuza ama kutoa vibali vya ujenzi katika maeneo hayo bila kufuata taratibu, hivyo kusababisha kukosekana maeneo ya wazi.

"Tuwe na tabia ya kutunza maeneo ya wazi... baadhi ya watendaji wameuza maeneo, hivyo maeneo yote yapitiwe upya na yale yaliyovamiwa kwa kiasi kidogo taratibu za kuwaondoa zifanyike na Oktoba 1, 2019 taarifa kuhusiana na zoezi hilo ziwe zimefika wizarani," alisema.

Pia alipiga marufuku ofisi za ardhi katika halmashauri kukodisha vifaa vya upimaji pale ambapo kuna vifaa vya wizara na kusisitiza kuwa halmashauri hizo zinaweza kuazima vifaa pale tu ambapo kuna idadi kubwa ya wananchi wanaotaka kupimiwa kama vifaa vilivyopo havitoshi.

Vile vile, alizitaka halmashauri wakati wa kuchukua kampuni kwa ajili ya kupima maeneo kama urasimishaji kuzingatia kampuni zenye uwezo na kasi ya kufanya kazi hiyo badala ya kuchukua ambazo utendaji unategemea fedha kutoka kwa wapimiwa, na kuzionya halmashauri ambazo hazijaomba kupima maeneo.

Kwa upande wake Waziri wa Wizara hiyo, William Lukuvi, aliwataka washiriki wa mkutano huo kuhakikisha wanabadilika kwa kutatua kero za wananchi na kusisitiza kuwa migogoro ya ardhi katika maeneo yao lazima yamalizwe haraka badala ya kusubiri viongozi wa kitaifa waende kuitatua.

Katibu Mkuu wa Wizara, Drothy Mwanyika, aliwaambia washiriki kuwa ana imani baada ya mkutano kutakuwa na mabadiliko katika sekta hiyo na wizara kwa ajili ya kuleta mabadiliko na kitaundwa kikosi kazi cha kufuatilia.

# Wanaharakati wakubaliana

INATOKA UK. 2

maslahi ya nchi, upelelezi wa kesi za jinai ufanyike mapema watu washtakiwe na kukutwa na hatia, watu wako ndani miaka minne hadi 10 upelelezi unaendelea jambo ambalo siyo sawa.

"Watu serikali haiwaumi kabisa, kuna mambo machafu sana kwa kuwa kuna watu wanashikiliwa kwa uonevu kwa muda mrefu na hawajasaidiwa, siku hizi imekuwa kawaida watu kunyimwa dhamana kwa makosa yenye dhamana," alibainisha.

**THRDC**

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alipongeza kauli hiyo na kutaka utekelezaji ufanyike kwa haraka kwa kuwa ndiyo matakwa ya haki za binadamu.

"Tunampongeza sana kwa kuwa ni vitu tumevipigia kelele kwa muda mrefu, mtuhumiwa ana haki za msingi mtu ni mtuhumiwa kabla Mahakama haijamkuta na hatia, lakini kwa mazingira ya sasa wanatuhumiwa kabla ya Mahakama kujiridhisha na matokeo yake wanasota gerezani kwa muda mrefu," alisema.

Alisema kinachotakiwa aliyoyasema yasiishie hewani bali kuwe na utekelezaji ikiwamo mabadiliko ya sheria pamoja na kuheshimu sheria husika.

Kwa mujibu wa Olengurumwa, sheria ya kumshikia mtu kwenye kituo cha polisi kwa saa 24 ipo, lakini watu wanashikiliwa ndani ya vituo vya polisi kwa zaidi ya muda huo hata siku saba kuendelea bila kufikishwa mahakamani na hapewi dhamana. Alisema makosa makubwa duniani ni uhaini na mauaji ambayo mtu hapewi dhamana iwapo itathibitika ameyatenda na sasa kesi yake inasikilizwa, lakini kwa Tanzania hata makosa ya kawaida mtu ananyimwa dhamana.

"Makosa yasiyo na dhamana ni mawili, lakini upelelezi wake unachukua miaka mingi sana na tuna mifano ya watu wako gerezani miaka 10 kesi zao hazijasikilizwa sababu upelelezi unaendelea. Kwa kauli hii sasa upelelezi uharakishwe ili haki ipatikane," alisema.

**LHRC**

Naye Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema wanaunga mkono kauli hiyo na kwamba imekuwa kilio cha muda mrefu kwa kuwa ndiyo matakwa ya haki za binadamu.

"Kwanini mtu ananyimwa dhamana ambayo ni haki, unapomnyima maana yake umemhukumu, nia ya dhamana ni kwamba mtu hana kosa hadi Mahakama iseme," alibainisha na kuongeza:

"Tumepigania sana kwanini kuna makosa yana dhamana na mengine hayana, maana huwezi kujua kama mtu ameua hadi mahakama itamke, kwanini mwingine unampa dhamana na umemnyima? Tumefurahishwa na kauli hii sasa iende kwenye utekelezaji."

Henga alisema dhamana inatolewa kwa ajili ya kumlinda mtu ni vyema jaji au hakimu aangalie, mfano mtuhumiwa wa kubaka na kulawiti ni kosa kubwa ukimweka ndani inapoza machungu ya waliotendewa, hivyo ni vyema ikaangalia aina ya kesi, lakini kwa usalama wa mtuhumiwa ananyimwa dhamana. Vile vile, alisema wametembelea magereza mara kadhaa na kukuta watu waliokaa muda mrefu wakisubiri upelelezi wa kesi zao ukamilike na wengine wamekaa miaka mitatu hadi 10 ndiyo kesi inasikilizwa na kuhukumiwa.

"Mtu amekaa miaka minne kwa kosa lisilo na dhamana baadaye anaachiwa, mwingine anakaa miaka minne anahukumiwa mwaka mmoja na kufanya jumla ya miaka mitano kwa kosa ambalo adhabu yake ni mwaka mmoja, hii sio sawa kabisa," alisema.

Naye aliyekuwa Rais wa TLS, Fatuma Karume, katika ukurasa wake wa Tweet aliandika kuhusu kauli hiyo huku akiweka video ya Jaji Mkuu.

"Jua kwamba sheria mbovu zinabatilishwa na Mahakama! Ndio maana mfumo wetu ni Serikali, Bunge na Mahakama. Kuisikia Mahakama inaomba kuwaachiwa huru itoe haki ni maajabu. Maana Katiba imeipa Mahakama uhuru huo."

Mmoja wa watu waliochangia kwenye ukurasa huo alisema: "Mahakama pamoja na majaji wamebanwa na sheria mbovu. Ni wajibu wa Bunge kurekebisha sheria, pamoja na mtuhumiwa kupewa dhamana. Ndicho alichokimaanisha Jaji Mkuu."

Pia, Karume aliandika: "Eti Mahakama inaiomba Serikali na Bunge iwaachie haki ya kusimamia dhamana! Kama Mahakama inaomba haki sisi wananchi tuende wapi kudai haki? Maskini hata hawaelewi kwamba wao ndio watoaji wa haki! Wao wanaiomba kutoka kwa Bunge na Serikali!"

HABARI KITAIFA

# Waziri: Marufuku maofisa madini kufunga viwanda uchenjuaji madini

Na Shaban Njia, KAHAMA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amewataka maofisa madini wilayani Kahama mkoani Shinyanga kuacha mara moja tabia ya kuvifunga viwanda vya uchenjuaji wa madini vitakavyobainika kuwa dosari, badala yake watoe maelekezo yatakayowezesha kiwanda kuendelea na uzalishaji.

Biteko alitangaza marufuku hiyo wakati akizungumza na maofisa madini pamoja na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya mjini Kahama, na kusema serikali haitaki kuona viwanda vinasimama kwa kuwa na dosari ambazo zinaweza kurekebika.

Alisema tutakuwa watu wa ajabu kuhubiri sera ya viwanda huku viwanda vikiendelea kufungwa kwa dosari ndogo ndogo na kuongeza kama mmiliki wa kiwanda atakuwa na makosa ya jinai anatakiwa kufikishwa mahakamani na sio kufunga kiwanda.

"Ndugu zangu, tutakuwa viongozi wa ajabu sana kuendelea kuhubiri sera ya serikali ya viwanda, huku bado tunaendelea kuvifungia viwanda ambavyo makosa yake yanaweza kurekebika. Sitaki kuona biashara za uchenjuaji wa madini zinasimama huku serikali ikiendelea kukosa mapato," alisema Biteko. Katika hatua nyingine, Biteko alisema atawachukulia hatua za kisheria wanunuzi ambao wamekuwa wakinunua madini kutoka kwa wachimbaji wadogo kinyume cha sheria kwa kuwa wamekuwa wakichangia utoroshwaji wa madini na kwenda kuuzwa Kenya.

Alisema mpaka sasa kuna zaidi ya wanunuaji 12 ambao wameshafahamika wananunua madini kutoka kwa wachimbaji wadogo, kisha kuyasafirisha hadi Kenya, kitendo ambacho kinaikosesha serikali mapato.

Pia Biteko alisema kwa muda wa wiki moja mnunuzi mmoja alinunua dhahabu zaidi ya kilo tatu yenye dhamani ya shilingi milioni 300, lakini mpaka sasa hajalipa mrabaha wa serikali na hii ni kutokana na kununua kinyemela kutoka kwa wachimbaji wadogo.

Aliongeza kuwa mnunuzi wa pili alinunua dhahabu kwa muda wa wiki mbili na alipata kilo 2.64 na kuuza kwa shilingi milioni 241, pia naye hakulipa mrabaha wa serikali.

Mwenyekiti wa viwanda vya uchenjuaji wa madini mkoani Shinyanga, Nicodemas Majabe, alisema wachimbaji wadogo wamekuwa wakishawishiwa na wanunuzi na kuuza madini kinyemela kwa kuwa kwa wakati huo wanakuwa hawana fedha za matumizi wawapo mgodini.

Naye Kamisheni wa Tume ya Madini, Prof. Abdulkari Mruma, alisema kila mchimbaji mdogo anatakiwa kuhakikisha anauza dhahabu yake kwenye masoko, hivyo kumwezesha kuuza dhahabu yake kwa bei ambayo itakuwa sokoni wakati huo.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Rukia Muwango (mwenye ushungi), akipokea msaada wa vyakula na mafuta kutoka kwa Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Runali, Hassan Mpako, kwa ajili ya kambi za taaluma za wanafunzi wa darasa la saba juzi. Chama hicho kilitoà kilo 1,360 za mchele, kilo 340 za maharage na lita 170 za mafuta ya kula. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Miaka mitatu jela kumwibia majeruhi wa ajali mil. 12/-

Na Ahmed Makongo, BUNDA

CHARLES Mwita (32), mkazi wa Nyasura mjini Bunda mkoani Mara, amehukumiwa na Mahakama ya Wilaya hiyo kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela baada ya kupatikana na kosa la wizi wa kuaminiwa wa Sh. milioni 12, mali ya Edward Njumbi, mkazi wa Kunanga Guta wilayani hapa.

Mwendesha Mashtaka Inspekta Jonas Kaijage, alidai kuwa mshtakiwa huyo alikabidhiwa kiasi hicho cha fedha zilizokuwa ndani ya begi, baada ya mlalamikaji katika kesi hiyo, (Njumbi) kupata ajali ya pikipiki kwenye barabara kuu ya Bunda-Ukerewe, eneo la Virian mjini Bunda.

Alidai kuwa baada ya Njumbi kupata ajali katika eneo hilo, mshtakiwa huyo ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kufika katika eneo la tukio na kumwokoa mlalamikaji huyo kisha kukabidhiwa begi lilokuwa na fedha hizo.

Aidha, Kaijage alidai kuwa Njumbi alimwamini mshtakiwa huyo kwa vile wakati mwingine humtumia kama dereva wake katika shughuli zake.

Kufuatia ushahidi uliotolewa na mashahidi watatu katika shauri hilo, Hakimu Majinge alisema kuwa ameridhika pasipo kuacha shaka yoyote, na ndipo akamhukumu adhabu ya kifungo cha miaka mitatu jela, kisha amrudishie fedha zake zote shilingi milioni 12.

Kabla ya hukumu kutolewa, Inspekta Kaijage aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa, kwa maelezo kuwa kitendo alichofanya siyo cha kiungwa hasa ukizingatia kwamba mlalamikaji huyo alikuwa ni majeruhi na alimpatia fedha hizo kwa kuamini kuwa ni dereva wake.

Kwa mujibu wa Kaijage, vitendo kama hivyo vya kutaka utajiri wa haraka haraka vinarudisha nyuma juhudi za watu wengine wanaojishugulisha na kazi halali katika kujiletea maendeleo, na kwamba pia adhabu hiyo itakuwa fundisho kwake na kwa watu wengine wenye nia au tabia kama hiyo.

Kabla ya hukumu kutolewa Hakimu Majinge alimpa nafasi mshtakiwa huyo kujitetea, ambapo aliiomba mahakama hiyo kumpunguzia adhabu, lakini ombi hilo lilitupiliwa mbali na mahakama hiyo na kusema kuwa anayo haki ya kukata rufani katika mahakama nyingine ya juu.

## Mikakati ya Takukuru kukabiliana na rushwa

Na Neema Sawaka, KAHAMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, imewekeza nguvu kwenye utoaji elimu kwa umma ili jamii ielewe madhara na matatizo ya kutoa na kupokea rushwa.

Aidha, lengo ni kuhakikisha vitendo hivyo vinapungua kwa kiwango kikubwa kama si kumalizika kabisa.

Akizunguma na vyombo vya habari mjini Kahama, Mkuu wa Takukuru Wilaya ya Kahama; Richard Kiula, alisema wamewekeza nguvu kubwa ya elimu kwa umma ili jamii iweze kuelewa tatizo la rushwa na madhara yake na nini wafanye wanapokumbana na changamoto hiyo.

Kiula alisema njia zinazotumika kutoa elimu hiyo ni pamoja na mikutano ya hadhara, semina kwa taasisi za serikali, umma na vyama vya siasa pamoja na kufungua klabu za wapinga rushwa shuleni. Alisema hatua hiyo imesaidia kuleta matokeo chanya kutokana na jamii kuhamasika kutoa taarifa ambazo zimesaidia kudhibiti mianya ya rushwa.

"Kupitia elimu hiyo, tumekuwa tukipokea malalamiko ambayo mengine tumeyatolea ushauri na mengine kutokana na uzito wake, tumeyafanyia uchunguzi kisha kuifikisha mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria," alisema Kiula. Pia, alisema baadhi ya malalamiko wanayofikishwa na wananchi ma hubaini kutohusika nayo, kuyapeleka katika sehemu husika, huku wakifuatilia kwa karibu kwa kuomba wapatiwe taarifa juu ya kinachoendelea.

Kwa mujibu wa Kiula, mbalimbali na shughuli hizo pia wamekuwa wakijihusisha na kufanya utafiti mbalimbali katika idara kadhaa za serikali na sekta za umma ili kukabiliana na mianya ya rushwa, hatua iliyotoa mchango mkubwa katika udhibiti wa upotevu wa mapato ya serikali.

Katika utoaji huo wa elimu kwa umma, kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Juni 30, 2019 wamefanya mikutano ya hadhara 27, semina 17 na kutoa elimu kwa klabu za wapinga rushwa 41, huku akieleza kuwa kwa mwaka huu wa fedha wamejipanga zaidi katika utoaji wa elimu hiyo kwa umma.

## KESI YA MAUAJI DAR:

# Shahidi adai alivyomwona mama ubatizo akimpiga mpwa

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDi (Jina linahifadhiwa), amedai mahakamani katika kesi ya mauaji ya Naomi John (7) kwamba alimwona mama yake wa ubatizo, Ester Lyimo, akimpiga mpwa wake mpaka akafariki dunia.

Andrew ambaye alikuwa akiishi nyumbani kwa mshtakiwa, kwa sasa anaishi Moshi mkoani Kilimanjaro, mbali na kumwita mama wa ubatizo ni mama yake mdogo.

Ushahidi huo ulisikilizwa Ijumaa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji iliyoketi chini ya Naibu Msajili, Pamela Mazengo.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Cecilia Mkolongo, shahidi huyo wa kwanza katika kesi hiyo, alidai kuwa anamfahamu mshtakiwa alikuwa anaishi naye hapa Dar es Salaam kama mama yake wa ubatizo.

Alidai kuwa nyumbani kwa mshtakiwa aliishi pia na dada Sia, Basila, Junior na Naomi.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano kati ya Wakili wa Jamhuri na shahidi:

**Wakili wa Jamhuri:** Naomi kwa sasa yupo wapi?

**Shahidi:** Amezikwa.

**Wakili wa Jamhuri:** Kwanini amezikwa?

**Shahidi:** Alipigwa na mama wa ubatizo mpaka akafariki.

**Wakili wa Jamhuri:** Alipigwa kwa sababu gani?

**Shahidi:** Naomi alimwaga maji ndani yakasambaa akaambiwe apige deki nyumba nzima na mimi nikaambiwa nimsadie, lakini alifika mahali alishindwa kuendelea akaanza kupigwa na fimbo za mpera mpaka zikaisha, mama mdogo (mama wa ubatizo) akamng'ata na meno mgongoni.

"Alimwingiza kwenye maji yaliyokuwa katika pipa akamtoa akamweka barazani akammwagia chai ya moto, nilimwona Naomi amechoka akampeleka bafuni akamtoa akamlaza kitandani akamwashia feni."

**Wakili wa Jamhuri:** Nini kiliendelea baada ya hapo?

**Shahidi:** Mama mdogo alinituma dukani nikanunue unga ili ampikie uji, nilikwenda niliporudi nilimwona Naomi anatoa povu mdomoni na puani.

**Wakili wa Jamhuri:** Nini kiliendelea?

**Shahidi:** Mama mdogo alitoka alikwenda kununua dawa aliporudi

INAENDELEA UK. 24



Mafundi wakijenga mtaro wa maji ya mvua kwenye barabara mpya ya kiwango cha lami, inayounganisha eneo la Tandale na Mwananyamala, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Barabara hiyo imerahisishia wananchi wa Tandale kuwahi kwenye shughuli zao na hata kwenda kupata huduma za afya katika Hospitali ya Mwananyamala. **PICHA: SABATO KASIKA**

# AICC kufanyia ukarabati mkubwa nyumba zake

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KITUO cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), kimejizatiti kufanya ukarabati mkubwa wa nyumba zake za makazi zilizoko katika eneo la Kijenge na Kaloleni jijini hapa, ili kuhakikisha zinakidhi hali ya sasa ya ushindani wa soko.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa AICC, Elishilia Kaaya, alisema kituo chake kimedhamiria kuzifanyia ukarabati nyumba zake ili ziendani na ushindani wa soko.

"Tumepanga kufanya ukarabati mkubwa ili kuendana na ushindani wa soka na kukidhi haja ya sasa hasa kutokana na kuongezeka kwa uhitaji wa nyumba za kisasa kutokana na kukua kwa sekta ya utalii," alisema.

Alisema kituo kimeshafanya ukarabati wa wa nyumba 16 ikiwamo kuweka bati za kisasa zaidi na nyumba zingine 32 zipo kwenye mpango wa kufanyiwa ukarabati mkubwa ukiacha ukarabati wa dharura unaofanyika mara kwa mara.

Aidha, alisema kituo kimekamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa kufanya marekebisho ya mitaro iliyopelekea baadhi ya nyumba za AICC zilizoko Kaloleni kukumbwa na mafuriko baada ya ujenzi wa Barabara ya Moshi-Namanga kuelekeza mitaro ya maji kwenye eneo la Kaloleni badala ya to Naura kama ilivyokuwa awali.

Alisema mkandarasi anaweza kuanza ujenzi wa mitaro hiyo ikiwamo kupanua mitaro husika na kujenga eneo la kupita maji juu ya barabara ili kuziokoa nyumba za Kaloleni kukumbwa na mafuriko tena wakati wa mvua.

Kaaya pia alisema ili kuondoa msongamano katika hospitali yake iliyopo kwenye eneo la Corridor, kituo kimepanga kujenga jengo moja la idara ya wagongwa wa nje. Ujenzi huo unatarajiwa kuanza muda wowote kuanzia mwezi ujao.

"Tumepanga pia kuzifanyia ukarabati barabara kwenye eneo la makazi ya nyumba zetu kwa kutumia 'pavement blocks' kutokana na barabara hizo hasa zilizopo Kijenge zilijengwa muda mrefu, hivyo kuwa na mashimo mengi," alisema.

AICC ni kituo kinachomilikiwa na serikali chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na kinamiliki nyumba mbalimbali za makazi, hospitali na kumbi za mikutano katika vituo vyake viwili vya JNICC Dar es Salaam na AICC mkoani Arusha.

# Viongozi ushirika wafungwa miezi sita kisa wizi wa mil. 10/-

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Mwanzo Mtama Wilaya na Mkoa wa Lindi, imewahukumu viongozi wawili wa kikundi cha Muungano kikoba cha Nyengedi kifungo cha miezi sita kila mmoja, baada ya kupatikana na kosa la kula njama na kuiba Sh. 9,999,000.

Viongozi hao ni Bakari Chande Beno na Sharifa Saidi, ambao ndio waliopewa dhamana na wanachama kutunza fedha zao.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Mtama, Teddy Mvula, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa walalamikaji wa kikundi hicho.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, washtakiwa waliulizwa kama wanazo sababu za msingi za kuiambia mahakama isiwape adhabu kali, ambapo kila mmoja kwa nafasi yake aliomba waonewe huruma kwa madai ni wakosaji wa mara ya kwanza na wanazo familia wakiwamo watoto na wazee wanaowategemea.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Mvula alisema amesikia vilio vyao, hivyo akawahukumu kila mmoja kifungo cha nje cha miezi sita, huku akiwapa muda wa mwezi mmoja kuanzi Ijumaa kurejesha kwa wanachama wenzao fedha hizo.

Awali ilielezwa mahakamani hapo kuwa Mei 22, mwaka huu, usiku wakiwa ni viongozi walioaminiwa na wenzao kutunza fedha za michango yao, walikula njama na kuiba shilingi 9,999,000 kwa kuiba kisanduku cha kutunzia fedha kikundi cha Muungano Kikoba.

Pia, ilielezwa kuwa baada ya kutekeleza njama hizo, walitoa taarifa kwamba watu wasiojulikana walivamia nyumbani kwao na kuiba kisanduku hicho na kutokomea kusikojulikana, kisha kuiba fedha zilizokuwamo ndani, huku kisanduku kikitelekezwa pembezoni mwa njia.

# Muro atoa siku 30 ujenzi wa sekondari ukamilike

**Na Novatus Makunga,** ARUMERU

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, ameagiza awamu ya kwanza ya ujenzi wa mradi zaidi ya Sh. bilioni 2.5 wa Shule ya Sekondari ya Elimu Maalumu Patandi, uwe umekamilika ndani ya mwezi mmoja.

Muro alitoa agizo hilo baada ya kukagua ujenzi unaoendelea wa shule hiyo iliyopo maeneo ya Tengeru, wilayani humo mkoani Arusha.

Alisema ujenzi huo ulitakiwa uwe umekamilika Aprili 7, mwaka huu na kuitaka Halmashauri ya Wilaya ya Meru, pamoja na kamati ya ujenzi kuhakikisha unakamilika ndani ya mwezi mmoja.

"Pamoja na kwamba ujenzi unaendelea, lakini kasi yake ni ya kusuasua, hivyo mnapaswa kuongeza kasi, ili ndani ya mwezi mmoja tuwe tumekamilisha na kuikabidhi hii shule kwa mamlaka husika," alisema.

Muro alisema kuwa ifikapo mwishoni mwa mwezi Agosti mwaka huu, wanatarajia kuikabidhi shule hiyo, kwa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Alisema serikali itaendelea kuelekeza nguvu katika shule hiyo maalumu na ya mfano, ili kufanikisha mkakati wa kutoa elimu kwa watu wenye uhitaji maalumu nchini.

"Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya elimu hasa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ili iendelee kuwa mfano katika sekta ya elimu," alisema.

Awali Mkuu wa Chuo cha Ualimu Patandi, Luciano Segela, alisema ujenzi huo, umekamilika kwa asilimia 97 unahusisha majengo matano ya awali.

Aliyataja majengo hayo kuwa ni pamoja na mawaili ya upande wa utawala, madarasa, bwalo na bweni.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Meru, Emmanuel Mkongo, alimwakilishia mkuu huyo wa wilaya, kwamba awamu hiyo ya kwanza ya mradi huo itakamilika ndani ya mwezi mmoja.

Mkongo alisema mpaka sasa kamati ya ujenzi wa mradi wa shule hiyo imepokea kiasi cha Sh. bilioni 2.3.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Zephania Chaula, akikagua wakazi wa eneo la Orkesumet wanavyopata maji kwa shida wakati huu wa ukame juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wananchi wamwomba Rais utatuzi mgogoro wa ardhi

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WANANCHI wa Kijiji cha Vilima Vitatu kilichopo katika Kata ya Ngaiti, wilayani Babati Vijijini, wamemwomba Rais John Magufuli, kutembelea kijiji hicho ili kuwasaidia kutatua mgogoro wa ardhi uliopo kijijini hapo.

Baadhi ya wananchi hao wakizungumza jana na waandishi wa habari kwenye semina ya siku mbili iliyoandaliwa na Shirika la Mtandao wa Wafugaji na Wawindaji wa Asili (Pingo's Forum), walilalamika kuchomewa maboma yao kwa madai ya kuvamia njia za mapito ya wanyama (ushoroba) kuelekea Ziwa Manyara.

Mmoja wa wananchi walioathirika katika uchomaji wa maboma hayo, mwanaharakati Dorcas Elesh, alisema katika uchomaji huo uliofanywa Julai 7, 8 na 9, mwaka huu, umewasababishia kukosa makazi ya kuishi.

"Sasa sisi wananchi wa nyumba 34 tuliochomewa tumekosa nyumba na tunaishi chini ya miti, huku usalama wa maisha yetu ukiwa hatarini kwa kuwa wanyama na baridi kali vyote wanakabiliana navyo," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo, hawana mtetezi wanamwomba Rais John Magufuli, ambaye ni mtetezi wa kweli wa wanyonge atembelee eneo lao ili aweze kubaini ukweli wa tukio hilo.

Said Ghamunga, Mkazi wa Kijiji cha Minjingu, alisema nyumba walizochomewa zipo sawa na viota vya ndege, hivyo wanasikitika kuona wenye nyumba za kifahari wanawaonea kuwachomea viota vyao na kusababisha kukosa pa kulala na watoto.

"Tunaomba tusikilizwe na tutendewe haki, hasa Rais Magufuli aje kutusikiliza ili afahamu ukweli wa eneo hili na sisi tuondokane na kunyanyasika," alisema.

Mwenyekiti wa wafugaji Wilaya ya Babati, Lomnyaki Ngoiseye, aliomba serikali kuwasaidia kubaini waliohusika kuchoma maboma yao na kukosa mahali pa kulala.

Naye Mwanasheria wa kampuni ya mawakili ya Matelu, Belinda Alphayo, aliwaomba wananchi hao kwenda katika vyombo vya haki, kama mahakamani kupigania haki yao endapo wanaona wameonewa.

"Nasema hivi sababu wananchi wa eneo la Malamboi wanaoishi hifadhi ya Burunge miaka ya 2012, walishaondolewa maeneo yao ya makazi kwa madai kuna ugonjwa wa kimeta, huku mwekezaji mmoja akiachwa kuendelea kuishi katika eneo hilo walienda mahakama ya rufani mwaka 2013 na walishinda kesi yao namba 70/2012 na kuamriwa kubaki katika eneo hilo," alisema.

Alisema njia za kupigania haki zipo nyingi endapo wananchi wanaona wanadhulumiwa haki zao za msingi wasikae kimya au kulalamika wakati kuna vyombo vya sheria.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Monduli, Julius Kalanga, alisema ingekuwa busara kusubiri uamuzi wa tume iliyoundwa na Rais Januari 15, mwaka huu na kujumuisha wizara saba ili kuzungukia maeneo ya wafugaji kuangalia changamoto zinazowakabili na kutatua.

"Ingekuwa busara kusubiri uamuzi wa tume hiyo kama wangepita na kuamuru wananchi waondoke hapo sawa sasa hawajapita baadhi ya watu wanaamua kuwaondoa hiyo inakuwa sio busara, naamini Rais na viongozi mbalimbali wameona watashughulikia," alisema.

# NIC yatoa msaada mabati 300 sekta ya elimu

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

SHIRIKA la Bima la Taifa (NIC) limekabidhi mabati 300 yenye thamani ya Sh. milioni 8.1, kwa Wilaya ya Arusha ili kusaidia sekta ya elimu mkoani humo.

Akiongea mwishoni mwa wiki na waandishi wa habari, jijini hapa, Mkurugenzi wa shirika hilo, Sam Kamanga, alisema, masaada huo ni moja kati ya misingi ya utawala bora ambayo serikali inahimiza.

Kamanga alisema ni mara ya kwanza kutoa msaada kwa Mkoa wa Arusha, lakini wameshatoa msaada kama huo kwa mikoa mbalimbali ikiwamo Morogoro na Mwanza.

Alisema licha ya kutoa msaada huo pia wanatarajia kuja na bima ya kilimo, watakayoizindua katika maonyesho ya Nanenane mwaka huu, mkoani Simiyu, ambayo ina lengo la kumkomboa mkulima.

"Tumeamua kuileta bima ya kilimo kwa sababu wakulima wengi wamekuwa wanaingia katika kilimo na wakilima na kupata hasara, wengine wanakata tamaa wengine wanakufa, kwa sababu ya BP ya kupata hasara, hivyo ndio maana tumeleta bima hii sasa," alisema Kamanga.

Alisema wanatarajia baada ya kuanza kwa bima hiyo, kuona mafanikio makubwa kwa wakulima na kufanikisha katika uchumi wa kati na suala la uanzishwaji wa viwanda.

"Tunaamini mkulima akifanikiwa atazalisha mazao mengi yenye tija na watu watapata fursa ya kuanzisha viwanda vya kusaga unga na kuuza, hivyo watachangia sana katika kufikia azma ya serikali ya kufikisha nchi katika uchumi wa viwanda.

Kwa upande wa Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Fabian Daqarro, alilishukuru shirika hilo kwa msaada, kwa kuwa utasaidia katika maandalizi ya uhitaji wa sekta ya elimu na kuziomba wizara nyingine kuitikia maombi waliyoomba.

Alisema tangu serikali ya awamu hii itangaze elimu bure, kumekuwapo na mwamko wa wanafunzi na wazazi kupeleka watoto shule, hivyo itawasaidia katika kuwekeza madarasa, vyoo na nyumba za walimu.

# Malalamiko ya wafanyakazi 500 kupatiwa ufumbuzi

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WAZIRI wa Nchi anayeshughulikia Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu, Jenista Mhagama, ameagizwa kwenda kushughulikia malalamiko ya wafanyakazi 500 wa Kiwanda cha Hassani Sisal Estates kilichoko Wilaya ya Same ambao wanadai kunyonywa mishahara yao na kampuni mbili za uwakala.

Pia ameagizwa kupitia upya mikataba ya ajira ya wafanyakazi hao na kujiridhisha kama inalingana na kazi wanayoifanya na ikiwezekana asimamie ifumuliwe na kuandikwa upya. Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliagiza hayo juzi, wakati alipokwenda kutembelea kiwanda cha kusindika mkonge cha Hassani Sisal Estates kilichopo Kata ya Makanya, Wilaya ya Same, ambacho kinadaiwa kumilikiwa na Kampuni ya Mohamed Enterprises (MOELT).

"Wafanyakazi hawa wanalalamika mikataba ni mibovu, wanalalamika kwamba kuna kampuni mbili za Unique na Upami ambazo zinawanyonya na hasa kupunjwa mishahara yao. Nitaleta majembe yangu mawili hapa baada ya ziara yangu kumalizika, nitamleta waziri wangu anayeshughulikia kazi na ajira (Jenista) au Naibu wake Athony Mavunde, waje hapa washughulike na malalamiko haya.

"Moja ya malalamiko niliyosoma hapa kwenye mabango ambayo wananchi wamekuja nayo ni lile la kuzikataa kampuni za uwakala za Upami na Unique zisiendelee kuwa hapa, haiwezekani wafanyakazi walalamike kupunjwa mishahara yao na kukosa huduma ya gari la wagonjwa kwa ajili ya rufani. Narudia tena, suala la matibabu ni lazima lionekane kwenye mikataba ya ajira."

Akiwa katika mashamba ya mkonge, Majaliwa alisema tatizo lililopo katika kiwanda hicho ni menejimenti kuamua kujiondoa katika jukumu lake muhimu la kulipa mishahara na kuajiri na kusukuma mzigo huo kwa kutoa zabuni kwa kampuni hizo za uwakala ya Upami na Unique.

Akijitetea kuhusu malalamiko hayo, Mshauri na Meneja wa Kiwanda cha Hassani Sisal Estates, Ndekirwa Nyari, alimweleza Waziri Mkuu kwamba kampuni ya uwakala ya Unique, imepewa kazi ya kutafuta wafanyakazi na kampuni ya Upami, imepewa kazi ya kuhudumia mashamba kama kuotesha mkonge na kusimamia uvunaji.

"Nakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimepokea maelekezo yako na naomba nikuahidi hapa kwamba hata kabla ya waziri wako utakayemtuma hajafika hapa, tutakuwa tumeshughulikia hizi kero. Lakini hili la gari la wagonjwa naomba nilipeleke kwenye menejimenti ya kampuni na nina hakika watalishughulikia," alieleza Nyari.

Vile vile, Waziri Mkuu ametoa maelekezo kwa Kampuni ya Mohamed Enterprises kuhakikisha inapeleka gari la wagonjwa katika mashamba yake yaliyopo Makanya kwa ajili ya kuhudumia wafanyakazi hao wanapougua na kupewa rufani kwenda Hospitali ya Wilaya ya Same, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi) na Hospitali ya Rufani ya KCMC.



Diwani wa Kata ya Bomambuzi katika Manispaa ya Moshi, Juma Raibu, akiteta jambo na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Simon Sirro, wakati wa uzinduzi wa zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kitaifa uliofanywa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, mjini Moshi. **PICHA: JAMES LANKA**

# PM atoa amri kuhamishwa walimu saa 24

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa amri ya kuhamishwa walimu sita ndani ya saa 24 waliopo katika shule za mjini za Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro na kuwapeleka kwenye Shule za Msingi Kiti cha Mungu na Emangulai zilizoko katika Kata ya Kirya, kukabiliana na upungufu wa walimu.

Majaliwa alifikia uamuzi huo jana, baada ya kukuta Shule ya Msingi Kiti cha Mungu yenye madarasa manane na wanafunzi zaidi ya 400 ina walimu wawili pekee ambao wanafundisha masomo tisa kila darasa, kuanzia la kwanza hadi la saba.

Kutokana na changamoto hiyo, Waziri Mkuu amemwagiza Ofisa Elimu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Paulina Nkwama, kumsukuma Ofisa Elimu wa Wilaya ya Mwanga kuwahamishia walimu hao katika shule hizo.

"Inasikitisha kusikia kuwa shule yenye madarasa manane, wanafunzi zaidi ya 400 ina walimu wawili tu au watatu wanaotakiwa kufundisha masomo tisa kila darasa kuanzia darasa la kwanza hadi la saba," alisema.

Alitoa agizo hilo jana, wakati akizungumza na wananchi wa kata hiyo baada ya kukagua ujenzi wa mradi mkubwa wa maji unaotarajiwa kuzinufaisha Wilaya za Mwanga, Same na Korogwe.

Alitoa maagizo hayo, baada ya baadhi ya wananchi kumpa malalamiko yao kupitia mabango waliyokuwa wameyaandika.

"Nakuagiza Ofisa Elimu kesho (Jumapili) tafuta walimu pale mjini, waandikie barua ya uhamisho kuja Kirya, Jumatatu wawe wameshafika hapa na nataka taarifa ukimaliza hayo," alisema pia alimwagiza Ofisa Elimu wa Mkoa wa Kilimanjaro kufuatilia suala hilo.

Alisema pamoja na juhudi zinazofanywa na serikali kuondoa tabia ya walimu kupenda shule zilizoko maeneo ya mijini, inasikitisha kuona bado wengi wanapenda kung'ang'ania kufundisha shule zilizoko maeneo ya mijini huku shule za vijijini zikabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu.

Awali kupitia mabango yao, wananchi hao walilalamikia changamoto hiyo ya kusema katika Shule ya Msingi Kiti cha Mungu yenye madarasa manane na wanafunzi zaidi ya 400, ina walimu wawili pekee, nyingine ya msingi ya Emangulai yenye idadi kama hiyo ya madarasa na wanafunzi ilikuwa na walimu watatu.

# Wanaodaiwa kutafuna fedha za maafa kusakwa

**Na Godfrey Mushi,**

MWANGA

SERIKALI imeagiza vyombo vya usalama kufanyika uchunguzi wa kina wa madai ya kutafunwa fedha za maafa zilizochangwa na wananchi pamoja na wadau mbalimbali, baada ya Soko la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mwanga kuteketea kwa moto.

Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa, alitoa agizo hilo kufuatia malalamiko ya wananchi na kutaka vyombo vya usalama kuanza kazi hiyo wiki hii ya kuchunguza madai hayo yaliyotolewa na wananchi ili kujiridhisha kama tuhuma hizo zina ukweli na kufahamu matumizi sahihi ya fedha hizo na ikithibitika, waliofanya hivyo wakamatwe mara moja na kufunguliwa mashtaka.

Majaliwa aliagiza kufanyika kwa uchunguzi huo, wakati akizungumza na wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.

Kwa mujibu wa taarifa alizozitoa Waziri Mkuu, fedha hizo zilichangwa na wadau wa maendeleo ikiwamo Benki ya NMB, wafanyabiashara wakubwa na wananchi kwa ajili ya kuwapiga jeki, wajasiriamali waliopatwa na maafa hayo.

Kabla ya uamuzi huo, wananchi hao walimwambia Majaliwa kwamba eneo la choo cha soko hilo, limeuzwa na mtu amejenga kibanda, lakini pia soko hilo halina choo kwa sasa.

Waziri Mkuu amemtaka Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mwanga (TEO), aliyefahamika kwa jina moja la Lubumba, kuandaa taarifa ya jumla ya namna fedha hizo zilivyotumika na mahali zilipo kwa sasa.

"Lubumba wewe simamia hili tunataka taarifa ya fedha zilizochangwa, tuipate na pili, fedha ziko wapi na hawa waliozitafuna wako wapi na kama wamekula zote au zingine wamefanyia kazi tuambie," aliagiza Majaliwa.

Alitaka hatua kali zichukuliwe dhidi ya waliohusika, huku pia akimtaka ofisa huyo kuripoti kwa Mkuu wa Wilaya hiyo ili aweze kutatua jambo hilo.

Vile vile, alisema ni lazima soko hilo lipate usimamizi wa karibu ili wananchi wakae wapate huduma zao.

Alihoji bila choo wananchi watajisaidia wapi na kwamba sokoni ni muhimu kuwe na huduma zote muhimu na lazima fedha hizo zirudishwe.

Awali, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mwanga, alisema yeye ni mgeni katika nafasi hiyo ana mwezi tu hivyo hana taarifa za kutosha kuhusu soko hilo.

# Nipashe Spotika




KLABU INAYOMFAA DANI ALVES EPL UK.18

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Gareth Bale, sasa amekaribia kuondoka klabuni hapo kwa mujibu wa kocha Zinedine Zidane.
Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 aliachwa kwenye mchezo wa Real Madrid wa maandalizi ya msimu mpya ambao walichapwa mabao 3-1 na Bayern Munich mjini Houston nchini Marekani juzi.






Beki wa timu ya Fiorentina, Federico Ceccherini (kushoto), akiburuzika kumkaba Eddie Nketiah wa Arsenal wakati wa mchezo wao baina ya timu hizo kwenye maandalizi ya msimu mpya. **PICHA: MTANDAO**

SOKA




# SABABU 5 ZA YANGA KUTWAA UBINGWA MSIMU 2019/20

Na Adam Fungamwango

KIKOSI cha Yanga kiko mkoani Morogoro kuweka kambi kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2019/20.

**Yanga, kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu imebadilisha sehemu kubwa ya kikosi chake na imefanya usajili kuendana na matakwa na hadhi ya klabu kubwa kama hiyo.**

Msimu uliopita wakati kikosi hicho hakikuwashtua sana wanachama na mashabiki wa klabu hiyo, kilimaliza nafasi ya pili, nafasi ambayo hata hivyo wachambuzi wa masuala ya soka wanasema kuwa hakikupaswa kuwa kutokana na wachezaji dhaifu iliyokuwa nao.

Ilitegemewa labda ingeweza kuwa kwenye nafasi ya nne au tano.

Hata hivyo, msimu huu baada ya kufanya Uchaguzi Mkuu uliowaweka madarakani viongozi wapya chini ya Mwenyekiti Dk. Mshindo Msolla na Makamu wake Fredrick Mwakalebela, Yanga ni kama imefufuka upya.

Kwa ushawishi waliokuwa nao walitumia nguvu za wanachama wao, baadhi wakiwa ni wabunge, viongozi wa serikalini, viongozi wastaafu kufanya harambee iliyosababisha kupatikana pesa ambazo zilitumika kufanya usajili 'wa kufa mtu'.

Yanga iko katika harakati ya kutaka kutwaa ubingwa ambao imeupoteza misimu miwili mfululizo, ukitwaliwa na mahasimu wao wa jadi Simba.

Mara ya mwisho kikosi cha Yanga kutwaa ubingwa ilikuwa ni msimu wa 2016/17. Mwandishi wa makala haya anakuletea sababu tano ambazo zinaweza kuifanya timu hiyo kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara kwa msimu wa 2019/20...

### 1. USAJILI WA HADHI YAKE

Kuelekea msimu ujao Yanga imejitahidi sana kusajili wachezaji ambao wanaendana na hadhi ya klabu hiyo.

Imesajili wachezaji wa ndani na nje ya nchi ambao sasa unaweza kusema kuwa wana uwezo wa kuichezea klabu kubwa kama hiyo.

Ni tofauti na msimu uliopita ilipokuwa na wachezaji wachache tu ambao kweli unaweza kusema wana hadhi ya kuichezea Yanga.

Wachezaji kama Ibrahim Ajibu, Gadiel Michael, Heritier Makambo, Papy Tshishimbi na Godfrey Paul ndiyo haswa unaweza kusema walikuwa na hadhi ya kuichezea klabu hiyo kutokana na uwezo wao waliokuwa wakionyesha uwanjani.

Kwa sasa Ajibu, Gadiel na Makambo hawapo kwenye kikosi hicho, lakini usajili uliofanywa unatia matumaini kuwa kama wachezaji wao wakiwa fiti, basi hakuna kitakachoshindikana.

Baadhi ya wachezaji hao ni Farouk Shikalo, Patrick Sibomana, Sadney Ukhrob, Lamine Moro, Juma Balinya hawa ni kutoka nje ya nchi.

Wengine ambao ni Watanzania ni Abdulaziz Makame, Ally Ally, Ally Mtoni Sonso na wengine ambao wamerudisha matumaini kwa wanachama na mashabiki wa Yanga.

### 2. STAILI YA UFUNDISHAJI WA ZAHERA

Sifa kubwa kwa Yanga kuweza kumaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu msimu uliopita inapelekwa zaidi kwa Kocha Mkuu Mwinyi Zahera kutokana na uwezo wake mkubwa unaoonekana kwenye kufundisha na kusoma mchezo.

Wengi wanasema kama si Zahera, basi Yanga isingeweza kumaliza kwenye nafasi hiyo kutokana na kuwa na kikosi dhaifu, lakini uwezo wa kocha huyo kwenye maeneo mbalimbali kama vile kufundisha, kuusoma mchezo wakati ukiendelea, kubadilisha mbinu kutokana na mchezo husika, kufanya mabadiliko kwa wakati, lakini pia kusimamia nidhamu, huku akiwa hasiti kumkemea mchezaji yoyote anayekwenda kinyume chake, kumesababisha Yanga imalize ikiwa ya pili.

Kama ikiwa hivyo kwa kikosi cha msimu uliopita, hali itakuwa vipi kwa kikosi kama cha msimu ujao ambacho kimekamilika kila idara, hivyo akiongeza na mbinu zake kama za msimu uliopita, sina shaka wanachama na mashabiki wa Yanga msimu ujao unaweza kuwa kicheko kwao.

### 3. WACHEZAJI KUCHEZA KWA KUJITOLEA

Hii ni sifa ya Yanga miaka nenda rudi. Klabu hiyo imejaliwa na utamaduni wa kuwa na wachezaji wenye kupambana hata wakiwa kwenye hali ngumu. Iwe migogoro ya viongozi au matatizo ya kifedha. Wachezaji wa Yanga huweka yote pembeni na wanafanya kazi moja tu ya kuipambania jezi ya timu yao na mara nyingi hufanikiwa kwa hilo.

Cha ajabu ni kwamba mchezaji yeyote yule, atoke popote pale ndani au nje ya nchi, akiingia kwenye klabu hiyo naye anageuka na kuwa kama wenzake, yaani ni kama wanaambukizwa tabia hiyo ya upambanaji bila kujali hali ilivyo.

Yanga ilikuwa na matatizo ya kifedha kwa muda mrefu msimu uliopita, lakini hii haikuwafanya wachezaji wasite kupambana na hatimaye wakamaliza wakiwa kwenye nafasi ya pili.

Tatizo lilioonekana ni kwamba pamoja na upambanaji wao, lakini uwezo mdogo wa wachezaji ndiyo ulikuwa umefikia pale.

Inawezekana kabisa kama wangekuwa wachezaji wenye viwango vya hali ya juu kama waliosajiliwa sasa na wanajitolea, hali ingekuwa tofauti. Kwa maana hiyo usajili uliofanyika msimu huu na wachezaji wakicheza kwa 'jihad' kama kawaida yao, basi msimu unaweza kuwa mzuri kwa Yanga.

### 4. MASHABIKI NA WANACHAMA KUJITOLEA

Kwa sasa klabu ya Yanga ni kama inaendeshwa tu na kichango ya wanachama na mashabiki wao.

Kumekuwa na harambee mbalimbali za kuichangia klabu hiyo kwa ajili ya kujiendesha na mambo mengine.

Hiyo inawafanya kuwa karibu na klabu yao na kufuatilia chochote kile ambacho kinafanyika na hii inaleta ufanisi wa hali ya juu kwa viongozi na wachezaji kufanya kila njia ili kuwafurahisha mashabiki wao, waendelee kutoa michango. Kuwafurahisha wanachama na mashabiki ni kupata ushindi tu uwanjani.

Kinyume cha hayo kitawafanya kukata tamaa na kupunguza michango, hivyo juhudi za viongozi na wachezaji kutaka kuwapa furaha mashabiki, ndiyo itasababisha timu hiyo kuwa karibu zaidi na ubingwa.

### 5. AMANI NA UTULIVU KLABUNI

Klabu ya Yanga inaonekana kuwa kwa sasa imetulia. Moja ya matatizo yanayofanya klabu za Simba na Yanga kukosa ubingwa ni kuwa na migogoro. Na mara nyingi migogoro ya klabu hizi huwa haiwi kote kwa wakati mmoja. Simba kukitulia Yanga kunakuwa na matatizo na Yanga kukiwa safi, Simba kinawaka. Hii husababisha kurahisisha upande mmoja kuwa bingwa.

Amani na utulivu kwa sasa umetamalaki kwenye klabu hiyo, hata yule mwanachama wao maarufu mzee Ibrahim Akilimali ambaye mara kwa mara amekuwa na tabia ya kuibuka na kuleta mtafaruku yuko kimya. Utulivu huu pamoja na mengine yaliyoainisha yanaweza kusababisha Yanga kutwaa ubingwa msimu wa 2019/20 kama ikijipanga vema.

JE, WAJUA?



GOLIKIPA wa Algeria, Rais M'bolhi amemaliza mashindano ya mataifa ya Afrika, Afcon 2019, akiwa na rekodi bora zaidi, kwani ameruhusu mabao mawili tu kutikiswa kwenye nyavu zake hadi kunyanyua kombe hilo.

# MTIBWA ILIVYOBOMOLEWA TENA KWENYE USAJILI



Kikosi cha Mtibwa kikiwa na baadhi ya wachezaji walioihama klabu hiyo msimu huu ambao ni Benedict Tinoko (wa tatu waliosimama toka kushoto), Hassan Isihaka (wa nne waliosimama kutoka kushoto) na Ally Shomari (wa kwanza kulia aliyepiga goti).

**Na Adam Fungamwango**

MTIBWA Sugar ndiyo klabu inayoonekana kuwa na mkosi hasa inapomalizika Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Ndiyo klabu inayoondokewa na wachezaji wake wengi kwenda kujiunga na klabu nyingine mbalimbali.**

Msimu huu pia tayari wachezaji wa klabu hiyo wameshaanza kupukutika kwenye klabu mbalimbali kutafuta malisho mengine.

Pamoja na kuwa na mkosi huo, imekuwa na bahati ya kupata wachezaji wengine mbadala na wanakuwa na viwango kama vile vile vya wale wa mwanzo, au wakati mwingine kuzidi.

Msimu unapomalizika kazi inakuwa ni ile ile tena. Klabu zinanyemelea kwa mara nyingine tena zinachukua na wao wanaendelea na kazi ya kutafuta vibaji vingine.

Ila kuna wakati wachezaji hao hao wanapokosa kufanya vizuri huko wanakokwenda hurejea tena kwenye klabu hiyo na kupokelewa kwa mikono miwili na viwango vinarejea upya.

Baadhi ya wachezaji wa Mtibwa ambao wameshawahi kuondoka kwenye klabu hiyo na kurejea ni Issa Rashid 'Baba Ubaya' ambaye alimtimkia Simba, Mussa Hassan 'Mgosi' aliondoka na kurejea mara mbili akielekea Simba, lakini pia Henry Joseph na kapteni Shaaban Nditi, wote kwa nyakati tofauti wameshawahi kuondoka hapo na kwenda Simba, baadaye wakarejea tena, akiwamo pia Ally Shomari.

Mastraika Hussein Javu na Said Bahanuzi nao wameshawahi kuondoka kwenye mashamba ya miwa na kwenda kwenye klabu ya Yanga, yalipowashinda walirejea tena Mtibwa Sugar.

Hata hivyo kwa sasa Javu yupo Alliance, huku Bahanuzi taarifa zikisema kuwa huenda akatua Biashara ya Mara. Wapo pia baadhi ya wachezaji ambao waliondoka na mpaka sasa hawapo kwenye klabu hiyo, badala yake wanapambana kwenye maisha ya soka.

Hao ni Mohamed Ibrahim, ambaye alikwenda Simba na sasa taarifa rasmi ya klabu hiyo inasema kuwa itampeleka Namungo kwa mkopo, Salim Mbonde ambaye tangu ajiunge na Wekundu wa Msimbazi amekuwa kwenye chumba cha daktari tu muda wote na sasa taarifa inasema kuwa ameambiwa atafute klabu nyingine isiyokuwa na presha, kwani hawezi tena mikikimikiki na ushindani wa namba hapo.

Wengine ni Shiza Kichuya ambaye alikwenda Simba ambayo imemuuza nchini Misri anakocheza soka la kulipwa, Mzamiru Yassin ambaye ameweza kupambania namba yake Msimbazi mpaka sasa, Said Mohamed 'Nduda', Andrew Vicent 'Dante' aliyejiunga na Yanga na wengine wengi.

Maana yake klabu hii imekuwa kama kitalu. Msimu huu pia imeshaanza kuondokewa na baadhi ya wachezaji na huenda kabla dirisha la usajili kufungwa Julai 31 wanaweza kuongezeka.

Wafuatao ni baadhi ya wachezaji ambao tayari wameshaachana na Mtibwa Sugar waliokuwa wakichezea msimu uliopita na kujiunga na klabu nyingine kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu.

**1. BENEDICT TINOKO**

Ndiye aliyekuwa golikipa tegemeo kwa Mtibwa Sugar misimu miwili iliyopita. Kwa msimu ujao hawatokuwa naye, kwani tayari ameshatia saini kwenye klabu ya Kagera Sugar.

Tinoko ameshambulishwa na Kagera Sugar kama mchezaji rasmi wa klabu hiyo, huku Mtibwa Sugar ilikubali yaishe kwa kumtakia kila la kheri kwenye maisha yake mapya.

Jina lake lilianza kuvuma alipokuwa na timu hiyo hiyo ya Kagera Sugar, kabla ya kutimkia Yanga mwaka 2015.

Hata hivyo maisha ya soka kwenye klabu hiyo kubwa hayakuwa mazuri na kutimkia Mtibwa Sugar.

Akiwa huko alionyesha kiwango cha hali ya juu, hadi timu yake ya zamani ilipoamua kumrudisha tena nyumbani.

**2. KELVIN SABATO**

Ameondoka kwenye klabu ya Mtibwa na kwenda kujiunga na klabu ya Daraja la Kwanza Gwambina FC.

Kelvin Sabato, mmoja wa mastraika hatari nchini, hakuwa na msimu mzuri, lakini ukiacha msimu uliomalizika, msimu mwingine uliopita alikuwa moto wa kuotea mbali, akiibeba Mtibwa kwenye mechi mbalimbali na kuiwezesha hata kupata tiketi ya kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika msimu uliopita.

Klabu ya Mtibwa imetoa taarifa za kumtakia mafanikio mema straika wao huyo. Kabla ya kujiunga na Mtibwa, Sabato alizichezea pia klabu za Ndanda, Mwadui, Stand United na Majimaji.

**3. ALLY SHOMARI**

Beki huyu na kulia, lakini pia mwenye uwezo wa kucheza kama winga wa kulia, ameondoka kwenye klabu ya Mtibwa na kutimkia Kagera Sugar.

Kwenye mtandao wao rasmi wa klabu umesema kuwa unashukuru kwa yote aliyoyafanya na kumtakia safari njema na kazi njema kwenye klabu yake mpya.

Alirejea misimu miwili iliyopita akitokea Simba ambayo nayo ilimsajili kutoka klabu hiyo hiyo ya Mtibwa Sugar.

Ni mmoja wa wachezaji waliochukuliwa ili kutengeneza ukuta wa Kagera Sugar ambayo msimu uliopita ilipotea chupuchupu kushuka daraja, kama si mechi ya 'play off' dhidi ya Pamba, iliyomsaidia kurejea Ligi Kuu.

**4. RODGERS GABRIEL**

Huyu pia ni beki wa kulia wa Mtibwa Sugar kwa miaka mingi. Naye ameamua kuipa kisogo klabu hiyo na kutimkia pia Mwadui FC.

Alikuwa akishirikiana na Shomari, hivyo unaona Mtibwa ina kazi ya kutafuta mabeki wa kulia wawili ili kuziba nafasi ya hawa waliowapoteza.

Mwadui FC ambayo nayo imeponea chupuchupu kushuka daraja nayo ikiokolewa kwenye mechi ya 'play off' dhidi ya Geita FC, imeonekana kufanya usajili wa nguvu ili yasije kujirudia tena msimu ujao wa Ligi Kuu.

**5. HASSAN ISIHAKA**

Kagera Sugar inaonekena kuongoza vita ya kumbomoa 'ndugu yake' Mtibwa Sugar, kwani kwa mara nyingine tena imemsajili Hassan Isihaka kutoka Mtibwa Sugar.

Ikumbukwe Isihaka ni zao la kikosi cha pili cha Simba na ameshawahi kuwa nahodha wa klabu hiyo ya Msimbazi. Ni mmoja kati ya wachezaji waliopandishwa na kuichezea kwa muda mfupi, kabla ya kutimka kwenye klabu hiyo na kwenda kutafuta malisho sehemu nyingine.

Huyu ni beki wa kati na Kagera imeonekana kwenye usajili imeonekana kuangalia zaidi eneo la ulinzi. Mtibwa imempa baraka zote, lakini taarifa zinasema kuwa klabu hiyo inasajili wachezaji wachache, lakini itapandisha wachezaji wengi vijana waliotwaa ubingwa chini ya miaka 20 hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

NDANI YA 18



## Jezi mpya ya City yachefua mashabiki

KLABU ya Manchester City imesema kwamba, jezi yake mpya imeonekana kuwatatiza na kuwavutia baadhi ya mashabiki na kuibua mjadala mkubwa katika mitandao ya kijamii.

Jezi hizo mpya zenye rangi mchanganyiko ya njano na chungwa, imeonakana kama imemwagiwa kimiminika kichafu.

Extra Time



# BAHATI ILIWABEBA ALGERIA IKAWAPOTEZA SENEGAL

**CAIRO, Misri**

ALGERIA ilitwaa taji lake la pili la michuano ya mataifa ya Afrika, Afcon, kwenye fainali iliyopigwa Ijumaa usiku kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Senegal kwenye uwanja wa Cairo.

**Iliwachukua Algeria dakika moja tu kupata bao hilo baada ya shuti la Baghdad Bounedjah kumbabatiza Salif Sane na kujaa wavuni.**

Timu zote mbili zilitengeneza faulo nyingi zisizo na umuhimu katika kipindi cha kwanza, huko zote zikishindwa kutengeneza nafasi nzuri za kufunga mabao katika mchezo wote huo.

Senegal walianza kipindi cha pili kwa kuonekana wenye bahati baada ya kuzawadiwa penalti, lakini teknolojia ya maamuzi ya usaidizi kwa njia ya video, VAR, iliikataa penalti hiyo.

Wote M'Baye Niang na Youssouf Sabaly walipata nafasi nzuri ya kufunga, lakini hadi mwisho wa mchezo, Senegal walishindwa kabisa kupata bao au kutengeneza nafasi nzuri ya kufunga, na mwisho wa siku Algeria wakajibebea taji hilo.

**SENEGAL**

Baada ya kipigo hiki kikosi cha Senegal kitazidi kuwa kwenye wakati mgumu na pengine kusambaratika, kwani kizazi hiki kilikuwa kinapewa nafasi kubwa ya kulitwaa taji hilo kwa mara ya kwanza katika historia yao.

Walishindwa kutengeneza nafasi za maana, huku Algeria wakionekana wakiivunja kiurahisi safu ya ushambuliaji ya Senegal. Kulikuwa na faulo nyingi, lakini Simba hao wa milima ya Teranga walishindwa kabisa kufurukuta.

Kuruhusu bao kwa staili ile ilikuwa ni bahati mbaya kwao, na kukosa penalti katika kipindi cha pili kwa maamuzi ya VAR kitawaumiza zaidi, na ilikuwa wazi kwamba ule haukuwa usiku wa bahati kwa Senegal. Nafasi nyingi walizojaribu kuzitengeneza hazikuwa na madhara yoyote na matokeo yake walishindwa kabisa kupenya kwenye safu ya ulinzi ya Algeria.

Kwa Senegal, hili lilikuwa kombe ambalo walikuwa na matumaini makubwa mno ya kulibeba kwa mara ya kwanza, lakini bahati ikawakataa.

**ALAMA KWA WACHEZAJI**

Gomis (5), Gassama (5), Kouyate (6), Sane (6), Sabaly (6); Saivet (6), Ndiaye (6), Gueye (7), Sarr (5), Niang (5), Mane (6), Diatta (6), Diagne (6).

**NYOTA WAO - IDRISSA GUEYE**

Wachezaji kama Sadio Mane na Ismaila Sarr walioneka kubanwa zaidi na hawakuwa na mchango mkubwa kwa timu dhidi ya Algeria, lakini kazi kubwa ilifanywa na Idrissa Gueye ambaye alionekana kuikamata vizuri safu ya kiungo.

Mchezaji huyo waKlabu ya Everton ya England, alitumia uwezo wake binafsi kwa kujaribu kuzuia mipira eneo la kiungo na kusukumiza mashambulizi mbele pamoja na kuwatengenezea nafasi wachezaji wenzake.

Nguvu na kasi ya Gueye ilimfanya kuzunguka uwanja mzima na ndiye aliyeonkena kutibua kila mbinu za Algeria wakati wakijaribu kusukumiza mashambulizi yao mbele.

Ulikuwa usiku ambao Gueye alikuwa kwenye kiwango cha juu zaidi, lakini bahati mbaya alikuwa kwenye kikosi cha kupoteza.

**ALGERIA**

Hiki ni kipindi bora zaidi kwa Algeria, waliingia kwenye michuano hii wakiwa na molari kubwa tangu mwanzo wa mashindano, ingawa wachache walikuwa hawaipi kabisa nafasi ya kulibeba kombe hilo.

Matumaini yalianza kujengeka kwa Algeria baada ya kushuhudia Ivory Coast na Nigeria wakipoteza na ushindi wao kwenye hatua ya makundi dhidi ya Senegal ukawafanya wawe na ari zaidi. Tangu kuanza kwa michuano hiyo, Algeria walionekana kuwa ndio wenye kikosi bora zaidi na kilichokamilika, na sasa wamethibitisha ubora wao.

Kwa mara ya mwisho, Algeria ilitwaa kombe hili mwaka 1990, lakini sasa wamelitwaa kwa mara ya pili baada ya kusubiri kwa miaka 29.

**ALAMA KWA WACHEZAJI**

M'bolhi (6), Zeffabe (6), Mandi (7), Benlamri (7), Bensebaini (6), Mahrez (5), Guedioura (7), Bennacer (7), Feghouli (5); Bounedjah (6), Belaili (6), Brahimi (6).

**NYOTA WAO - AISSA MANDI**

Baada ya kupata bao la mapema, Algeria ilihitaji kuwa imara zaidi kwenye safu ya ulinzi, na shukrani hizo zinamuendea Aissa Mandi, ambaye ndiye aliyefanya kazi kubwa mno kuhaikisha Senegal hawapenyi.

Mchezaji huyo wa Klabu ya Real Betis ya Hispania, aliitawala safu ya ulinzi na alizuia kabisa mashambulizi ya Senegal.

Alikuwa ngao kubwa mno kwa Algeria, huku pia akimsaidia golikipa wake, alikuwa anahakikisha hatari yoyote inaondolewa haraka langoni mwake na kupeleka mpira mbele. Fainali hii inaweza kuishi kwa muda mrefu zaidi kwenye akili za Mandi, kwani ndiye alikuwa kama 'roho' ya Algeria.

**KINACHOFUATA**

Sasa wachezaji wote watarudi kwenye klabu zao, tayari kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu za Ulaya mwezi ujao, huku wengine wakiwa na machungu, lakini wale wa Algeria wanarudi kwenye timu zao wakiwa na kitu cha kujivunia mkononi.

## Nukuu

"Tuna wachezaji wazuri ambao wanaweza kutusaidia na kusonga mbele. Kuna wachezaji wengine ambao wanaweza kuja ili kutusaidia. Tunatafuta wachezaji wazuri sana na sasa tunazungumzia kuhusu uwezekano wa kuwasajili wachezaji maarufu na walio ghali," **amesema kocha wa Arsenal, Unai Emery wakati akizungumzia usajili wa timu hiyo kwa kipindi hiki cha majira ya joto.**




"Wafahamu, ninampenda mchezaji huyu. Nilipokuwa kocha wa Chelsea nilijaribu kumleta Chelsea. Na ninamchukulia kama mchezaji muhimu kwetu ili kuweza kupata mafanikio, lakini wakati huo huo kuna soko la uhamisho. Tutaona kitakachotokea, lakini kwa sasa Romelu Lukaku ni mchezaji wa Manchester United," **amesema kocha mpya wa Inter Milan, Antonio Conte akizungumzia nia yake ya kutaka kumsajili mchezaji huyo.**



"Hatuna tatizo kubwa kwa sasa kwani kwa asilimia kubwa tumekamilisha usajili kwa wachezaji ambao tulikuwa tunahitaji kuwapa kandarasi. Ni nafasi chache ambazo zimebaki hivyo muda si mrefu tutakamilisha kazi yetu," **amenukuliwa kocha wa Kagera Sugar, Mecky Mesime wakati akizungumzia usajili wa klabu yake.**






# KLABU HII INAMFAA ALVES EPL

**LONDON,** England

DANI Alves kwa sasa ni mchezaji huru katika kipindi hiki cha majira ya joto, baada ya kumaliza muda wake wa kuitumikia Paris Saint-Germain kule Ufaransa, na pengine kuna timu chache ambazo zinamwania beki huyo wa kimataifa wa Brazil.

**Kwa sasa Alves ndiye mchezaji pekee duniani ambaye ametwaa mataji mengi zaidi katika mchezo wa soka kuliko mwingine yeyote, kwani taji la mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, lilikuwa kombe lake la 40 tangu aanze kucheza soka.**

Katika Ligi Kuu ya England, Klabu za Manchester City, Arsenal na Tottenham Hotspur zote zimekuwa zikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili beki huyo mwenye umri wa miaka 36, lakini je, usajili wa Alves kwa timu moja kati ya hizo unaweza kuwa na manufaa yoyote kwao?

Sasa makala hii inakuchambulia kati ya City, Arsenal na Spurs ipi inayomhitaji zaidi Alves na inayomfaa kwenda.

**MANCHESTER CITY**

Kwanini wanamhitaji: Huku wakiwa tayari na beki wa kulia chaguo lao la kwanza Kyle Walker, Alves anaweza kuwa msaidizi wake. Tayari wana Danilo, lakini bado hajawa na kiwango cha kuvutia kwenye Ligi Kuu. Amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa kule Juventus, kitu ambacho kitaacha nafasi wazi kwa Alves.

Kwanini hawamhitaji: Tayari wana mabeki wawili wa kulia Walker na Danilo, na Walker tayari ameshajihakikishia nafasi kwenye kikosi cha kwanza na tayari amesaini mkataba mpya Juni mwaka huu. Ndio, wanahitaji beki mwingine msaidizi wa hawa wawili, lakini wanaweza kutafuta mwingine, kwani Alves ni wazi kwamba hatakuwa suluhisho kwao.

Njia pekee ya kumchukua Alves ni kama Danilo ataondoka, na nafasi ya yeye kutua hapo inaweza kuchangiwa kwa kiasi kikubwa na kocha, Pep Guardiola ambaye walikuwa wote kule Barcelona.

**ARSENAL**

Kwanini wanamhitaji: Kwa sasa beki wa kulia chaguo la kwanza kwa Arsenal ni Hector Bellerin, ambaye kwa sasa anajiuguza majeraha ya goti na anakaribia kurudi uwanjani.

Safu yao ya ulinzi sio imara na kwa uhakika kabisa wanamhitaji Alves ambaye licha ya kiwango chake, lakini pia ni kiongozi mzuri dimbani na kwa kuwa hakuna ada yoyote inayotakiwa kumsajili, wana nafasi kubwa ya kumchukua.

Kwanini hawamhitaji: Kwa sababu kutoa kiasiki kubwa cha fedha kwa Arsenal ni tatizo, mshahara anaoutaka Alves wa pauni 200,000 kwa wiki, unaweza kuwa kikwazo kikubwa kumsajili na hasa kwamba anakwenda kuwa msaidizi wa Bellerin.

Hata hivyo, Arsenal inamhitaji zaidi Alves kwa ajili ya kuimarisha safu yake ya ulinzi ambayo bado haijawa imara.

Pia wanamhitaji mtu kama Alves kwa sababu ya uzoefu wake pia na uwezo wake wa uongozi akiwa uwanjani.

Ingawa kikwazo kingine kwa Alves kutua Arsenal ni kwa sababu hawajafuzu kucheza Ligi ya mabingwa Ulaya.

Alves mwenyewe ameshabainisha kwamba, angependa zaidi kujiunga na timu ambayo ipo kwenye michuano ya ligi ya mabingwa Ulaya, lakini Arsenal hawapo kwenye mashindano hayo msimu huu.

**TOTTENHAM HOTSPUR**

Kwanini wanamhitaji: Spurs tayari wameshampoteza beki wao wa kulia chaguo la kwanza, Kieran Trippier ambaye ametua kule Atletico Madrid na sasa wamebakiwa na Serge Aurier na Kyle Walker-Peters. Wote hao hawana uzoefu wa kutosha, hivyo kwa namna yoyote Spurs wanamhitaji beki wa kulia mwenye uzoefu.

Kwanini hawamhitaji: Kumsajili Alves litakuwa suluhisho la muda mfupi tu, kwani umri wake unamtupa mkono tayari hivi sasa akiwa na miaka 36.

Spurs kwa sasa wanatakiwa kumtafuta beki mpya ambaye atakuwa suluhisho la kudumu klabuni hapo.

Kwa sasa wanatakiwa kuwa na beki kijana ambaye anatakiwa kupewa nafasi nyingi zaidi ya kucheza kwa ajili ya kujijenga na kujiamini na ili aweze kupata uzoefu.

Hata hivyo, nafasi yao ya kumsajili Alves ni kubwa hasa ukizingatia kwamba wapo kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na uzoefu wa Mbrazil huyo unaweza kuongeza kitu fulani kwao.

Spurs kwa sasa ni moja ya kikosi kinachocheza soka la kuvutia zaidi barani Ulaya, wanaweza kumsajili Alves kwa ajili ya kumtumia kwa muda mfupi, lakini anaweza kuwa msaada kwao pia.

**NAJUA WAJUA**



KLABU ya Yanga ya Dar es Salaam imetambulisha jezi zake za nyumbani za msimu mpya wa 2019-2020 za rangi ya njano na nyeusi za kashata pia, ambazo zinakaribia kufanana na za mwaka 1992 walizopewa nchini Misri.

SOKA

# KWA NINI KLABU ZA EPL ZIMSAJILI NABIL FEKIR



**LYON,** Ufaransa

ANA umri wa miaka 25, amefunga mabao 71 na pasi za mwisho 46.

Kwa muda mrefu amekuwa akitajwa kama mmoja wa viungo wabunifu zaidi barani Ulaya, lakini hakuna anayeonekana kumhitaji Nabil Fekir.

**Klabu za Ligi Kuu England nazo hakuna yenye mpango naye na mwaka jana alitajwa kuwa na thamani ya euro milioni 70 wakati Liverpool ilipoonyesha nia ya kweli ya kutaka kumsajili.**

Klabu za Manchester City na Arsenal pia zimetajwa kwamba zinawania saini yake, kama kweli kile tunachokisoma ni kweli.

**NINI KIMEBADILIKA?**

Kwanza, wengi wanasema kwamba, hajaweza kujithibitishia yeye mwenyewe uwezo wake wa juu zaidi, kwani kwa karibia kipindi chake chote tangu aanze kucheza soka la kulipwa barani Ulaya amekuwa akicheza kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, akiwa na klabu ya Lyon.

Wengine pia wanasema kwamba, atakuwa na wakati mgumu kulizoea soka la Uingereza, lakini pamoja na yote hayo, Fekir ameendelea kuwa chaguo la kwanza katika klabu yake ya Lyon na ndiye nahodha wake.

Makala hii inakufafanulia kwanini Fekir anaweza kuwa bora zaidi kwa klabu za ligi Kuu za England.

Msimu wa 2017/18 kwenye Ligi ya Europa, ilimshuhudia Fekir akifunga wakati Lyon ikiwafumua Everton mabao 2-1 kwenye uwanja wa Goodison Park, kabla ya mchezo wa pili kupata ushindi wa mabao 3-0 katika dimba la Groupama.

Msimu uliopita wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, ulimtambulisha Fekir kama kiungo mwenye kasi zaidi akifunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho mbili katika mechi sita za hatua ya makundi. Hiyo haitoshi?

Muhimu zaidi ni kwamba, Fekir ndiye alikuwa nguzo muhimu zaidi wakati Lyon wakiwafunga Manchester City ya Pep Guardiola mabao 2-1 katika dimba la Etihad na yeye ndiye aliyehusika na mabao yote mawili.

Ukiacha mchango wake wa mabao hayo, kiwango chake kilikuwa cha juu zaidi ukilinganisha na wachezaji wote kwenye mchezo huo.

Akicheza kama kiungo mshambuliaji, Fekir anakuwa hatari zaidi kwenye lango la timu pinzani kwa sababu uwezo wake wa kupenyeza mipira ni mzuri zaidi.

Ni mchezaji ambaye amepevuka na mwenye mbinu za ufundi wa hali ya juu ambaye anaweza kutengeneza nafasi nyingi zaidi uwanjani, akijitengenezea yeye mwenyewe pamoja na wachezaji wenzake.

Kasi yake ni kubwa mno, kwani anaweza kuzunguka na mpira kutoka kiungo wa kati na akaambaa nao hadi kwenye winga na kutengeneza pasi zenye 'macho'.

Msimu uliopita mafanikio ya Memphis Depay na Moussa Dembele yalitengeneza na uwezo wa nahodha wao Fekir kwa kuwalisha vizuri zaidi mipira.

Lakini unashangaa timu kama Arsenal inashindwa kuvunja benki na kumsajili Fekir ambaye kwa namna yoyote anaweza kuwa msaada mkubwa mno kwa kikosi hicho.

Kwa uwepo wa washambuliaji kama Alexandre Lacazette na Pierre Emerick-Aubemeyang kungewapa nafasi nzuri zaidi Arsenal kama wangemsajili Fekir kwa ajili ya kuwatengenezea nafasi.

Fekir akicheza nyuma ya washambuliaji hao kuna uwezekano mkubwa mwisho wa msimu wafungaji bora wa Ligi Kuu England wakatoka Arsenal.

Wachezaji kama Mesut Ozil na Henrikh Mkhitaryan hawana kasi ya kutosha kwenye kusukumiza mashambulizi na kutengeneza nafasi.

Lakini Fekir anaweza kucheza nafasi ya wawili hao na Arsenal ikawa na kasi zaidi kwenye kutengeneza mashambulizi na kufunga mabao.

Kama ilivyoripotiwa na gazeti la Mirror, Arsenal wamepewa nafasi ya kumsajili Mfaransa huyo kwa pauni milioni 30.

Ingawa kikosi hicho cha kocha, Unai Emery kina tatizo la fedha za usajili, lakini kamwe hawatajuta kumsajili Fekir, kwani mchango wake utakuwa mkubwa mno kwao.

Kwa upande wa Liverpool, mjadala wa usajili wa Fekir umedumu kwa zaidi ya miaka miwili sasa.

Tangu kipindi akiwa na umri wa miaka 24 katika msimu wa 2017/18, ambako alifunga mabao 23, kocha Jurgen Klopp alijaribu kutaka kumsajili kumleta pale Anfield kwa ada iliyotajwa kuwa ni pauni milioni 52.

Hata hivyo, mpango huo ulishindikana dakika za mwisho kwa sababu iliyotajwa kuwa ni matatizo ya kiafya, ambayo hajawahi kuwekwa wazi, na pengine hilo ndilo linaweza kuwa kikwazo kwa Fekir kutua kwenye Ligi Kuu ya England.

NDANI YA 18



KINDA wa Klabu ya Arsenal, Eddie Nketiah, mwenye umri wa miaka 20 alifunga mabao mawili kuwawezesha washika bunduki hao kupata ushindi dhidi ya Fiorentina kwenye mchezo wa kirafiki wa maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu za Ulaya.

Nipashe
Spotika



ALGERIA ilitwaa taji lake la pili la michuano ya mataifa ya Afrika, Afcon, kwenye fainali iliyopigwa Ijumaa usiku kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Senegal kwenye uwanja wa Cairo.

Uk. 16&17

# TIMU TANO ZITAKAZOMALIZA UTAWALA WA JUVE SERIE A




**ROME,** Italia

IMETWAA taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A maarufu kama Scudetto, mara nane mfululizo. Imemaliza Ligi kwa kuwa na zaidi ya pointi 90 kwa misimu minne mfululizo. Inaonekana haizuiliki.

Juventus imetawala soka la Italia kwa miaka ya hivi karibuni. Hata hivyo, licha ya kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa mara mbili ndani ya misimu mitatu, imeshindwa kulibeba taji hilo.

Kwa sasa imeendelea kufanya usajili wa nguvu na kuzidi kuwekeza fedha, lakini je, nani atamaliza utawala wa kibibi kizee hicho cha Turin?

Hebu tuziangalie klabu hizi tano, je, zinaweza kumaliza umwamba huo wa Juve kwenye soka la Italia kwa msimu unaoanza mwezi ujao?

**SSC NAPOLI**

Imemaliza nafasi ya pili katika misimu mitatu kati ya minne iliyopita, Napoli inaonekana ndio klabu pekee inaweza kuchukua Scudetto kutoka pale Turin.

Ingawa kikosi hicho cha kocha, Carlo Ancelotti bado hakijavunja benki kwa ajili ya kufanya usajili msimu huu, kumwongeza Konstantinos Manolas kunaweza kukanyanyua matumaini ya nafasi hiyo.

Hata hivyo, klabu hiyo inakabiliwa na wachezaji wake wengi nyota kutakiwa na timu nyingine na hilo linaweza kuwapa wakati mgumu. Wachezaji kama Lorenzo Insigne, Dries Mertens, na Kalidou Koulibaly wamekuwa wakitajwa kuwaniwa kwa udi na uvumba na klabu nyingi barani Ulaya.

**INTER MILAN**

Kabla ya Juventus, Inter Milan ndiyo ilikuwa mtawala wa soka la Italia. Jose Mourinho aliwaongoza Nerazzurri hao kutwaa mataji matano mfululizo kati ya mwaka 2006 na 2010.

Kwa mara ya mwisho walitwaa mataji matatu kwa mpigo, kombe la Coppa Italia, Serie A na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, wameshindwa kupenya kwenye tatu bora tangu msimu wa 2010/2011, lakini kwa ujio wa kocha mpya, Antonio Conte kunaweza kuifanya Inter kurudi kwenye zama zake na kulitwaa tena taji la Scudetto.

Inter pia imeanza kufanya usajili mzuri, kwani tayari wamemchukua Diego Godin ambaye anaweza kuwa msaada mkubwa kwa kikosi hicho msimu huu na pia bado wapo sokoni kusaka wachezaji wengine wakali.

**AC MILAN**

Ilimaliza nafasi ya tano na kushindwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa tofauti ya pointi moja.

Ingawa Milan imepigwa marufu kucheza michuano ya Ligi ya Europa msimu unaokuja kutokana na kuvunja sheria ya haki ya matumizi ya fedha kwenye usajili wa wachezaji, bado ina nafasi kubwa ya kutoa changamoto kubwa kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Miamba hao 'waliolala' walitumia kiasi cha pauni milioni 170 msimu wa 2018/19, lakini zimeshindwa kuwalipa, lakini usajili wa Theo Hernandez kutoka Real Madrid kipindi hiki cha majira ya joto kinaweza kuipa timu hiyo ya kocha, Marco Giampaolo nafasi nzuri ya kutoa ushindani kwenye Serie A.

**AS ROMA**

AS Roma iliisumbua Juventus iliyokuwa chini ya kocha, Massimiliano Allegri kwa kipindi chote cha msimu wa 2016/17, ikimaliza kwa tofauti ya pointi nne tu na mabingwa hao.

Hata hivyo, msimu iliopita ulikuwa mgumu kwa Giallorossi hao wakati walipomaliza nafasi ya sita kwenye msimamo. Kipindi hiki cha majira ya joto tayari Roma wamewapoteza Manolas na Luca Pellegrini waliotimkia Napoli na Juventus, hivyo wana kazi ya ziada kwa msimu huu.

Hata hivyo, uwezo wa wachezaji vijana na wenye vipaji kama Justin Kluivert, Patrik Schick, na Cengiz Under pamoja na Edin Dzeko (kama atabakia), wana nafasi ya kutoa changamoto kwenye ligi hiyo.

**ATALANTA**

Atalanta ilikuwa ni timu isiyozuilika mwaka jana, ikifunga mabao 77 yakiwa mengi zaidi kuliko timu nyingine yoyote.


Wanaweza kuwa wanaonekana sio wakongwe, lakini wana nafasi nzuri zaidi ya kutoa changamoto kwenye ligi hiyo msimu huu unaokuja.

Klabu hiyo kutoka pale Lombardy imefuzu kwa mara ya kwanza katika historia yao kucheza kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya. Ikiongozwa na viwango bora vya Duvan Zapata, Josep Ilicic na Alejandro Gomez, Atalanta pia inatoa ishara kwamba itakuwa na moto mkali msimu unaokuja.

Katika soka lolote linaweza kutokea, aina ya uchezaji wao inaweza kuleta ushindani mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya Italia hasa katika mbio za kuwania Scudetto.

**USILOLIJUA**

MCHEZAJI Antoine Griezmann alikataliwa kwenye klabu za watoto kwa kuwa na umbo dogo la mwili wake na pia ni mpenzi mkubwa wa mpira wa ligi ya kikapu ya NBA ya Marekani na mchezaji anayempenda zaidi ni Derrick Rose wa Detroit Pistons.





# Fursa zatajwa kwa wanawake wajasiriamali

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAWAKE wajasiriamali katika mkoa wa Mbeya wameshauriwa kuchangamkia fursa za kibiashara zinazojitokeza badala ya kuogopa na kujiona hawawezi kufanya mambo makubwa.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa Taasisi inayojihusisha na kuunganisha nguvu ya Wanawake na Vijana ili kuchagiza maendeleo chanya ya kiuchumi na jamii nchini (TABWA), Norine Mawala, wakati wa kikao kilichowakutanisha kinamama mbalimbali kujadili na kubadilishana uzoefu kwenye shughuli za ujasiriamali.

Norine alisema wanawake wanapaswa kujitoa kimasomaso kuchangamkia fursa mbalimbali za kiuchumi zinapopatikana ili waweze kuendesha maisha yao.

Alisema TABWA imekuwa msaada mkubwa kwa wanawake na vijana katika kuwaunganisha na fursa za kibiashara pamoja na kutoa ushauri, uundwaji wa mtandao wa wanawake na vijana wenye lengo la kukuza biashara na kuleta tija kiuchumi.

"TABWA ni taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria ya kampuni na lengo lake ni kuchochea fikra ya maendeleo kwa wanawake na vijana ili kuamsha ari chanya katika makundi hayo na kujengewa uwezo wa maarifa, mitaji na teknolojia," alisema Norine.

Alisisitiza kuwa TABWA imejipanga kuhakikisha inapanua wigo wa fursa za kuwaunganisha wanawake na vijana, na kwamba wamejipanga kufungua tawi mkoani Mbeya ili kutoa huduma zao karibu.

Mmoja wa wanufaika wa taasisi hiyo, Severine Msuya, ambaye ni mjasiriamali wa mifuko mbadala jijini Mbeya, alisema amenufaika na masuala mbalimbali yanayohusu TABWA ambapo aliweza kushiriki warsha mbalimbali na kutembelea nchi mbalimbali ikiwamo China kujifunza.

Aliwataka kinamama kuchangamkia fursa zilizopo ndani ya TABWA kwa kujiunga kuwa wanachama kwa kuwa watapata faida mbalimbali ikiwamo kufahamiana na kubadilishana uzoefu pamoja na ushauri wa kibiashara.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Marryprisca Mahundi, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila katika kikao hicho, alisema wanawake hawanabudi kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza.

Alisema katika kuunga mkono jitihada za wajasiriamali na wafanyabiashara, serikali ilitoa mwongozo wa kila halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya mikopo ambapo kinamama wananufaika na asilimia nne vijana pia asilimia nne.

Aliwataka kutumia fursa hiyo kujiunga kwenye vikundi ili waweze kufanikiwa.



Mbunge wa Jimbo la Singida Magharibi, Elibariki Kingu, akihutubia katika mkutano wa hadhara uliofanyika juzi Kijiji cha Mtavira Kata ya Makilawa wilayani Ikungi mkoani Singida. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**

# Ahadi ya JPM ulipaji fidia Kyela yatimia

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

HATIMAYE agizo la Rais John Magufuli la kutaka wananchi wa Kata ya Njisi Wilaya ya Kyela Mkoa wa Mbeya, ambao walipisha mradi wa kituo cha pamoja cha forodha kati ya Tanzania na Malawi katika mpaka wa Kasumulu kulipwa fidia zao, limetekelezwa.

Utekelezaji umeanza baada ya Wizara ya Fedha na Mipango kutoa kiasi cha Sh. bilioni tano.

Wananchi wa kata ya walipisha mradi huo tangu mwaka 2016 na kuahidiwa kulipwa fidia kwa kipindi chote hicho hadi sasa ambapo mchakato umekamilika.

Akizungumza juzi kwenye Kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi), Msanifu Majengo, Elius Mwakalinga, alieleza kuwa Rais Magufuli alitoa agizo Aprili 30, mwaka huu, katika mkutano wa hadhara kuwa hadi kufikia mapema Mei wananchi waliopisha mradi wa kituo hicho, wawe wamelipwa fidia. Alisema viongozi wa serikali wakiwamo wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano walilishughulikia suala hilo usiku na mchana na hatimaye kulikamilisha kwa kupata kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi 205.

"Tumefanya kila jitihada kuhakikisha tunatekeleza agizo la Rais la kuharakisha fidia kwa wakazi wa Kata ya Njisi waliopisha mradi wa kituo cha pamoja cha forodha, Wizara ya Ujenzi,

Uchukuzi na Mawasiliano walikabidhi fedha hizo kwa Wakala wa Barabara (Tanroads) ambao ndio wamepewa jukumu la kutoa fedha hizo," alisema Mwakalinga.

Mwakalinga aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa watathmini watakaopita kufanya tathmini ya mwisho kabla ya kutoa fedha hizo kwa lengo la kujiridhisha.

Diwani wa Kata ya Njisi, Omary Mwijuma, alieleza kufurahishwa na hatua hiyo ya serikali ya kutekeleza ahadi ya muda mrefu ya kuwalipa fidia wananchi waliopisha mradi huo. Aidha, aliwashukuru wananchi kwa kuwa wavumilivu katika kipindi chote hicho cha kusubiri fidia zao na kwamba walikuwa wanatoa ushirikiano kwa viongozi mbalimbali.

# Wajawazito watembea kilomita 28 kusaka chanjo

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAJAWAZITO wa Kijiji cha Mkandami kilichopo Kata ya Mawindi Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya, wanatembea kilomita 28 kufuata huduma ya chanjo kwenye Kituo cha Afya cha Mawindi.

Akizungumza na Nipashe baada ya kumalizika kwa kikao cha Baraza la Madiwani wa wilaya hiyo, Diwani wa Kata ya Mawindi, Yusuph Mhando, alisema wajawazito wa Kijiji cha Mkandami hulazimika kutembea umbali huo kufuata huduma ya chanjo kwenye Kituo cha Afya cha Mawindi kwa sababu zahanati yao ya kijiji haina jokofu la kutunzia dawa za chanjo.

Mhando alieleza ni mara kadhaa amekuwa akiongea na mganga mkuu wa Wilaya ya Mbarali kuhusiana na adha wanazopata na hitaji la jokofu licha ya kuwapo kwa umeme katika zahanati hiyo.

"Zahanati hii ya Mkandami ilijengwa kwa asilimia 100 na nguvu kazi za wananchi, lakini cha kusikitisha hakuna huduma za chanjo kwa wajawazito, hiyo hali inayowalazimu kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo mahali pengine," alisema Mhando.


Diwani wa Viti Maalum Wilaya ya Mbarali, Salome Stemile, alisikitishwa na hali hiyo na kueleza ni lazima chanjo kwa wajawazito zitolewe kwenye zahanati walizo karibu nazo au vituo vya afya.

Alisema chanjo hizo zina umuhimu kwa maendeleo ya mama na mtoto aliyeko tumboni kuwa zinamsaidia kujikinga na maradhi.

"Chanjo ya mjamzito ni muhimu sana kwani akikosa chanjo na magonjwa mengi yanaweza kumwelemea, tunaendelea kutoa ushauri kwamba kadri inavyowezekana haya majokofu katika maeneo ya huduma za afya, kama kuna kata ambazo zina majokofu na ziko karibu za hospitali za wilaya basi ni vyema yakapelekwa sehemu zenye uhitaji," alisema Salome.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Dk. Godfrey Mwakalila, alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo na kuwa inatokana na uhaba wa majokofu.

Alisema serikali kwa kushirikiana na mashirika kama vile mashirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na Shirika la Afya (Duniani WHO), wamekuwa wakisaidia ununuzi wa majokofu na sasa Wilaya ya Mbarali inatarajiwa kupewa majokofu 18, zahanati ya kijiji cha Mkandami itanufaika.





# Sababu kuolewa umri mdogo yatajwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SABABU inayomfanya mtoto wa kike kuolewa na umri mdogo imetajwa kuwa ni changamoto ya familia nyingi kuamini watoto wa rika hilo wana soko la kutolewa mali nyingi.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jamii wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Patrick Golwike, katika warsha ya tathmini kuhusu ndoa za utotoni iliyokuwa chini ya Shirika la Save the Children.

Golwike alisema miongoni mwa vitu vinavyosababisha watoto wa kike kuolewa katika umri mdogo ni kuwapo kwa uelewa mdogo wa kuwa watoto wa kike wana soko na hivyo hutolewa ng'ombe wengi, jambo ambalo linakatisha ndoto za vijana hao.

Alisema mabinti wamekuwa wakiolewa kwa ng'ombe kati ya 25 hadi 50 kiwango ambacho wao huamini ni kikubwa, lakini kiuhalisia malengo yake yana thamani kubwa kuliko ambacho wanakipata kwa muda huo.

Alisema pamoja na juhudi kubwa za serikali katika vita hiyo, bado kuna tatizo katika jamii ambalo linaendelea kwa kuwa wanafanya mambo hayo wakati wanatambua ni kosa kisheria na wanawanyima haki watoto wa kike.

"Hizi imani za ng'ombe wengi ndizo huchangia kuwafanya watoto wa kike waendelee kuolewa katika umri mdogo, ni kosa kisheria, lazima tuungane na mashirika kupinga vitengo hivyo ili tumpe nafasi mtoto wa kike asome shule atimize malengo yake," alisema Golwike.

Alisema baadhi ya mikoa ikiwamo ya Shinyanga, Dodoma, Mara, Rukwa, Katavi na Tabora, kuna malalamiko mengi kuhusu vitendo hivyo ambavyo vinafanyika usiku na mchana.

Alisema kuwa ndoa za utotoni zimekuwa kikwazo kwa watoto na kuwanyima haki za kupata elimu pamoja na mahitaji muhimu ya watoto.

Mratibu wa Ufuatiliaji wa Shirika la Save the Children, Kanuty Munishi, alisema mradi wa mapambano hayo ulianza tangu 2017 wakijikita zaidi katika wilaya za Kishapu na Ushetu, zote za Mkoa wa Shinyanga, lakini alikiri licha ya uelewa wa tatizo hilo, bado kunahitajika usimamizi wa kutosha.

"Watoto wengi wamekuwa na mbinu za uelewa wa kujikinga na madhara hayo kwa kuwa wanaposhauriwa kwamba wasifanye vizuri katika mitihani ya darasa la saba ili waolewe, huitikia, lakini kwa vitendo hawafanyi hivyo," alisema.

# Oktoba Mosi maeneo yote yaliyovamiwa kuchukuliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeagiza kuwa Oktoba Mosi, mwaka huu, maeneo yote yaliyovamiwa na watu bila kufuata utaratibu yachukuliwe.

Agizo hilo limetolewa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Anjelina Mabula, wakati akifungua mkutano wa wataalamu wa sekta ya ardhi uliofanyika kwa siku tatu kwa lengo la kufanya mageuzi ya utendaji ndani ya wizara hiyo.

Mabula alisema ni wakati wa kila mmoja kusimama kwa nafasi yake ili kufanya kazi bila kuogopana vinginevyo wizara hiyo itabaki kwenye lawama kutokana na utendaji unaofanywa.

Alisema katika maeneo ambayo watu wanamiliki kihalali na kulipa kodi, watendaji wanapaswa kuonyesha wanajali na kuwasaidia ili wanufaike na ardhi zao, lakini maeneo ambayo wanadhani yamechelewa kufanya maboresho waangalie namna ya kutumia busara isipokuwa wavamizi kusiwe na huruma.

Mabula alisema wizara hiyo bado ina matatizo kwa baadhi ya watumishi wake kutokuwa waaminifu na kutoa mfano kwa watumishi wa Wilaya ya Shinyanga na amemwagiza Katibu Mkuu wa wizara hiyo kufanya uchunguzi wa kina.

"Shinyanga ni mfano mbaya kwetu, nakuagiza kuanzia leo Katibu Mkuu peleka timu ya uchunguzi na ushahidi waje wachukue kwangu," alisema Mabula.

Naibu Waziri Mabula, alikuwa mgeni rasmi katika mkutano huo, na kumtaka mkurugenzi wa mfumo wa mtandao (IT), kuangalia mifumo yake kwa sababu inaweza kudukuliwa na watendaji kisha kuwapunguzia madeni wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi. Awali, Mwenyekiti wa mkutano huo, Waziri mwenye dhamana, William Lukuvi, alisema kwenye mabaraza ya ardhi kuna matatizo na tuhuma nyingi ambazo zinasababisha kutokuaminika kwa watumishi.

Lukuvi alisema katika maeneo mengi inaonyesha kuna migogoro ambayo mingi inatengenezwa na wataalamu wenyewe na kuagiza lazima lishughulikiwe ili kuwabaini wenye tabia hiyo.

Katika hatua nyingine Lukuvi alishangaa kuwa tangu ameingia katika wizara hiyo hajawahi kupewa ramani ya Tanzania yenye kuonyesha mikoa na wilaya zote kwa sasa bali ziko ramani za zamani na alipodai watumishi walimwambia hawatoi ramani mpya kwa sababu ya mgogoro wa mipaka katika ya Wilaya ya Ubungo na Kisarawe.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Doroth Mwanyika, alisema siku tatu za mkutano huo lazima zitoe matunda kwa kuwa watumishi walifundishwa usalama na utunzaji wa siri za serikali huku wakichukuliwa alama za vidole na kulishwa kiapo cha uaminifu.



Msimamizi wa miradi ya ujenzi kampuni ya Kichina ya Stecol Corporation, Xu Lei (aliyonyosha mkono), akiwaonyesha wahandisi kutoka Benki ya Dunia pamoja na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) walipokagua mradi wa ujenzi wa kituo cha malori eneo la Nala jijini Dodoma mwisho wiki, kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kupaki malori 300 kwa pamoja. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Takukuru yataka rushwa ya ngono kufichuliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru), Mkoa wa Dodoma imewataka wanawake kutoa taarifa dhidi ya vitendo vya rushwa ya ngono vinavyofanywa sehemu za kazi dhidi yao ili kuisaidia taasisi hiyo kutokomeza ukatili huo unavyofanywa kwa kificho.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu rushwa ya ngono inayoendelea katika sekta mbalimbali hapa nchini.

Kibwengo alisema tatizo hilo lipo katika sekta binafsi, taasisi za umma na majumbani, lakini taarifa haziwafikii Takukuru kutokana na walengwa kuhofia kuzitoa kwa kuogopa kujulikana. "Tunaomba wanawake muwe na ujasiri wa kutoa taarifa ya vitendo hivyo, kwa sababu hakuna sheria inayoruhusu mtu kunyanyaswa kijinsia kazini, Takukuru itakulinda," alisema Kibwengo.

Alisema kumekuwa na matukio mengi ya aina hiyo kwenye jamii, lakini taarifa ya tuhuma zilizowasilishwa ni chache kulingana na uhalisia wa jambo lenyewe ndio maana wameamua kutoa taarifa hiyo na kuitaka jamii kutoa ushirikiano ili kutokomeza unyanyasaji wa aina hiyo.

"Tumeletewa tuhuma chache kipindi hiki haziendani na hali halisi ilivyo mitaani hususani katika sehemu za kazi," alisema Kibwengo.

Alifafanua kuwa hivi sasa taasisi hiyo imeanzisha dawati maalumu la jinsia la kushughulikia vitendo vya unyanyasaji wa kingono kwa wanawake na wanaume kama wapo wanaofanyiwa vitendo hivyo.

"Naomba jamii isisite kutoa taarifa kama wanafanyiwa vitendo hivyo kwa sababu ni kinyume na sheria namba 25 ya mwaka 2007, ambayo inakataza suala la ngono kazini," alisema.

Vile vile, alisema hakuna sababu ya jamii kuogopa kutoa taarifa ya kuwa ananyanyaswa kijinsia iwe kazini au nyumbani, kinachotakiwa ni kutoa taarifa yenye ukweli na wao watachukua hatua ya kuchunguza na kubaini kama ina ukweli na baadaye watachukua hatua stahiki za kisheria.


Alisema lengo lao ni kuona rushwa inatokomezwa katika sehemu za kazi hususani kwa wanawake ambao wamekuwa wakinyanyaswa kijinsia jambo ambalo haliteti picha nzuri kwa jamii. "Hata kama kuna wanaume wananyanyasika kingono kazini kupitia mwanamke naye anapaswa kutoa taarifa kwa sababu hakuna sheria inayoruhusu mtu kunyanyaswa kijinsia akiwa kazini," alisema.

Jamii imetakiwa kutoa taarifa pale wanapoona wananyanyaswa kijinsia ili kuisaidia taasisi hiyo iweze kubaini na kukomesha watu wanaotumia madaraka vibaya kwa ajili ya kuwanyanyasa wengine.

"Wote wanaotumia nafasi zao za madaraka kuomba rushwa ya ngono ni kinyume na sharia, wakibainika nao watawajibishwa ikiwamo kupelekwa mahakamani," alisema.

Alisema watu wamekuwa wakijificha hawako huru kutoa taarifa ya vitendo hivyo hata kama kunadalili za rushwa ya ngono au wametoa rushwa ya ngono.

Akizungumzia suala la utapeli unaofanywa na baadhi ya watu wakijifanya ni maofisa Takukuru, alisema wananchi wanapaswa kuwa makini na watu wa aina hiyo kwa sababu taasisi hiyo haitoi vitisho kwa jamii bali inafanya kazi kwa ushirikiano na wananchi.





Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohammed Khamis Mussa (Baucha} (Kushoto) na Mkuu wa Huduma na Upangaji Bei wa Zantel, Aneth Muga wakionyesha bango lenye maelezo ya promosheni ya MSAKO TIME wakati wa uzinduzi uliofanyika katika viwanja vya Kisonge mjini Zanzibar, mwishoni mwa wiki. Huduma hiyo itawezesha wateja wa Zantel kutumia data kwa saa moja bure kila siku katika kipindi cha miezi mitatu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Z'bar yahitaji utalii daraja la kwanza'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema Zanzibar inahitaji utalii wa daraja la kwanza utakaokwenda sambamba na miundombinu ya viwanda katika mwelekeo wake wa kuimarisha uchumi utakaoustawisha maisha ya wananchi na kuongezeka kwa mapato ya taifa.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, iliamua kuelekeza nguvu zake katika sekta hizo, ili kuondokana na utegemezi wa zao moja la karafuu lililotegemewa kwa karne kadhaa zilizopita na liliwahi kutetereka katika soko la dunia miaka ya 90.

Balozi Iddi alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na ujumbe wa viongozi waandamizi kutoka Jimbo la Zhejing, nchini Jamhuri ya Watu wa China, ukiongozwa na Mwenyekiti wake Ge Huijun aliyefika Zanzibar.

Alisema sekta ya utalii Zanzibar, imeanza kuleta matumaini makubwa kutokana na kukua kwa uchumi na mapato ya taifa sambamba na kustawisha maisha ya wananchi kunakotokana na ongezeko la watalii wanaotembelea visiwa vya Zanzibar.

Balozi Iddi alisema ujio wa viongozi hao waandamizi wakiwamo wakurugenzi wa taasisi tofauti pamoja na kampuni za miradi ya kiuchumi ya jimbo hilo, utaongeza chachu kwa watalii wa nchi hiyo Bara la Asia kupanga ratiba zao za matembezi visiwani humo. Alisema zipo fukwe adimu hupatikana katika maeneo mengine duniani, vivutio vya utalii, rasilimali za baharini pamoja na utamaduni wa asili vinavyotoa ushawishi kwa mwekezaji yeyote kuitumia fursa hiyo ya soko la utalii katika kuwekeza miradi ya hoteli. Aliipongeza China kwa uamuzi wake wa kushirikiana na mataifa ya Bara la Afrika katika azma ya kusaidia kunyanyua hali za kiuchumi za mataifa hayo yaliyobarikiwa kuwa na rasilimali nyingi ambazo bado hazijatumika ipasavyo.

Alisema kampuni na taasisi za uwekezaji za majimbo mbalimbali nchini China zinaweza kulitumia soko la Afrika Mashariki na mataifa yaliyopo Mashariki na Kusini mwa Bara la Afrika katika kuwapatia huduma za msingi wakazi wake wanaokaridiwa kufikia 300,000,000.

Alisema soko la pamoja la Afrika Mashariki, bado halijaweza kukidhi mahitaji halisi kutokana na kukosekana kwa taalamu na mbinu kwenye masuala ya uwekezaji vitega uchumi na matokeo yake baadhi ya bidhaa hadi sasa zinatoka nje ya maeneo hayo.

Naye kiongozi wa ujumbe huo wa viongozi waandamizi kutoka Jimbo la Zhejing, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Jimbo la Ge Huijun alisema rasilimali ya asili inayopatikana visiwani Zanzibar inawahamasisha wawekezaji wa jimbo lake kutaka kuwekeza Zanzibar.

Ge Huijun alisema wawekezaji wa jimbo lake wako tayari kuwekeza miradi yao katika mfumo wa kubadilishana uzoefu katika miradi ya kiuchumi na biashara katika dhana ya kuimarisha uhusiano wa miaka mingi uliopo kati ya China na Tanzania kwa jumla.

# Sera, sheria za utamaduni kuangaliwa upya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI imesema ipo haja ya kuangaliwa upya sera, sheria na taratibu zinazosimamia utamaduni ili kudhibiti vitendo vinavyokwenda kinyume na mila na silka za Kizanzibari.

Imesema hakuna taifa ulimwenguni linaloridhia na kukaa kimya pale mihimili ya utamaduni wake inapoanza kutikiswa na kusababisha nyufa kwa kisingizio cha wakati wa sasa au maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyopo ulimwenguni.

Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, alisema hayo wakati akifungua Tamasha la 24 la Utamaduni wa Mzanzibari lililofanyika katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika kipindi hiki taifa linaendelea kukumbwa na changamoto inayotokana na baadhi ya makundi ya vijana wakiwamo pia wazee wanaothubutu kujiingiza katika matendo ya udhalilishaji ambao ni kinyume na mila, silka pamoja na utamaduni uliorithiwa na kizazi kilichopita.

Alisema kumbukumbu za kihistoria zinaonyesha utamaduni wa Zanzibar umejengeka kwa mnasaba wa upendo, ukarimu, huruma, ustaarabu na uzalendo wa hali ya juu.

Pia alisema sifa hizo zilijenga ushawishi mkubwa na kurahisisha mwingiliano wa karibu baina ya wenyeji na wageni waliotembelea Zanzibar katika vipindi mbalimbali vya mapitio ya kihistoria.

Alisema mwingiliano huo ulisaidia ukuzaji wa mila, silka, desturi na miiko ya jamii na kustawisha hali njema kwa jamii ya Zanzibar ndani na nje ya visiwa vya Unguja na Pemba.

Kadhalika jamii haina budi kuelewa kwamba utamaduni ni mfumo unaojitosheleza katika nyanja zote za kimaisha, hivyo ni lazima uendane na mwenendo na utaratibu wa maisha uliokubalika kufuatwa ndani ya jamii husika.

Pia jamii imekuwa ikishuhudia mmong'onyoko mkubwa wa maadili unavyoendelea kulikumba taifa kwa kuona vijana namna walivyovutiwa na tamaduni za kigeni na kusababisha ukiukwaji wa maadili ya taifa.

Alisema matendo maovu wanayofanya vijana yamekosa uadilifu na kusababisha chuki, mifarakano, visasi baina ya familia na kuhatarisha mshikamano wa kijamii ambao wakati mwingine husababisha uvunjifu wa amani.

Balozi Iddi alisema kuwa vijana wengi hawafuati mfumo halisi wa maisha unaowakuza na hatimaye kuwa waathirika wa kuiga, kukumbatia na kufuata tamaduni ambazo kimfumo haziendani na mazingira na maisha halisi ya Mzanzibari.

Matendo hayo yameendelea kulitia aibu taifa pamoja na watu wake na kwa sasa wananchi wote wanapaswa kuyakemea.

Akitoa taarifa ya Tamasha la Mzanzibari kwa mwaka huu, Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Amour Mohamed Bakar, alisema lengo ni kukuza utamaduni wa Mzanzibari katika nyanja zote.

# Waumini dini ya Kiislam wakumbushwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAUMINI wa dini ya Kiislam nchini wametakiwa kutekeleza ibada ya hija kwa kila mwenye uwezo kwa kuwa ni nguzo muhimu.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema hayo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya mahujaji na maimamu wa misikiti Zanzibar, yalioandaliwa na Jumuiya ya Kiislamu wa Mashia Tanzania.

Alisema hija ni jambo muhimu kwa kila mwislamu mwenye uwezo wa hali na mali hivyo ipo haja kutekeleza ibada hiyo ya nguzo ya tano katika Uislam.

Alisema iwapo wenye uwezo wa fedha na kiafya watashindwa kufanya ibada hiyo wajue wanafanya makosa. "Iwapo mtu atakubaliwa hija na akadumu katika kufanya mema hadi kufa kwake, mtu huyo malipo yake ni pepo," alisema Mkuu wa Mkoa huyo.

Vile vile, alisema suala la amani katika nchi ni muhimu hivyo ipo haja ya wananchi kuwa makini kuitunza na kuunganisha nguvu zao katika misingi ya dini ili waweze kumtumikia Allah kwa wepesi zaidi.

Akizungumzia vitendo vibaya vya udhalilishaji wa watoto na vijana vinavyo favywa na baadhi ya viongozi wa kidini na viongozi wa kitaifa, alisema kuwa linawapotezea heshima, utu wao na kuwafanya kutoaminika na jamii. Alisema wapo baadhi ya watu wanatumiwa vibaya kuiharibu jamii kwa udhalilishaji wa kingono, kuwabaka watoto kwa kuwalaghai kwa thamani ndogo isio ya kibinadamu.

Alisema Mkoa wa Mjini Magharibi utachukua hatua kali kwa watu hao bila ya kuoneana haya kwa kufuata sheria na miongozo iliyopo.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Waislamu wa Shia Tanzania, Sheikh Ramadhani Ali Mwelekwa, alisema kuwa Jumuiya yao inatumika kwa kufanya masuala mbalimbali yakiwamo elimu, masuala ya kiafya na maji kwa kutoa huduma kwa jamii.

Alimshukuru Mkuu wa Mkoa kwa kukubali kuungana nao katika mafunzo ya mahujaji na maimamu wa misikiti Zanzibar. Alisema jumuiya inaungana na serikali katika kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

# Waomba malipo kahawa haraka

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WAKULIMA wa Kijiji cha Buma, Kata ya Kishanje na Kijiji cha Buhendangabo, Kata ya Bushagala wilayani Bukoba mkoani Kagera, wameuomba uongozi wa vyama vikuu vya ushirika kuharakisha malipo yao, baada ya vyama vya msingi (AMCOS) kupokea kahawa kutoka kwa wakulima hao.

Walieleza hayo katika mkutano na viongozi wa vyama hivyo kwa kushirikana na taasisi za kibenki za TADB, NMB na CRDB ambazo zinatoa elimu ya ufahamu wa mfumo jumuishi kwa mkulima ambao unalenga kusaidiwa mkulima kumwongezea tija katika uchumi na kuondoa usumbufu wa kufuata huduma umbali mrefu.

Dauson Mjwahuzi, mkulima wa Kijiji Butelangabo, alisema vyama vya msingi vimekuwa vikichelewesha malipo kwa mkulima, wakati mkulima hutegemea malipo kuendesha maisha na kuendelea kuboresha mibuni.

Mjwahuzi alisema, licha ya kukamilisha taratibu zote zinazotakiwa na serikali, lakini hawajalipwa fedha zao.

Jovith Joseph, mkulima wa Kijiji cha Bushagala, alisema haelewi kwa nini mifumo inayotumiwa haimsaidii mkulima kupata malipo yake kwa wakati licha ya makubaliano yaliyofikiwa.

Alisema amekaa kipindi cha mwezi mmoja sasa hajapata pesa ya malipo wakati tayari amepeleka magunia mawili ya kahawa ya maganda kwa bei elekezi ya shilingi 1,100 na imeshaanza kukobolewa ili kupeleka viwandani uongeza ubora.

Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Kagera (KCU), Edson Rugaimukamu, alisema ucheleweshaji wa malipo unafanywa na makarani ambao wanatakaa taarifa za mkulima ambazo zinatakiwa zifikishwe katika chama kikuu kwa ajili ya kutoa pesa inayotakiwa.

Rugaimukamu alisema chama hicho kilipanga kulipa mkulima ndani ya siku saba kupitia akaunti ya benki au kampuni ya simu ambazo zitalinda usalama wa fedha za mkulima baada ya kukamilisha taarifa zake za malipo.

"Niwahakikishie tu wakulima tayari pesa ipo na italipa wakulima wote ambao taarifa zao zinafikia vyama vikuu," alisema Rugaimukamu.

Naye Kaimu Meneja wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) Kanda ya Ziwa, Kaizilaabi Jumanne, alisema kazi kubwa ya benki hiyo ni kutoa uwezeshaji wa mikopo kwa vyama vikuu vya ushirika ili fedha iweze kumfikia mkulima kama sehemu ya kusogeza huduma kwa haraka.

# Agizo la JPM vifaa vya meli laanza kutekelezwa

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango zimeanza utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli la kupeleka vifaa vya miradi minne ya ukarabati wa meli mbili za Mv. Victoria na Butiama katika Bandari ya Mwanza Kusini jijini Mwanza.

Wakizungumza na waandishi wa habari katika bandari hiyo juzi, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Dk. Leonard Chamuliho na Naibu Waziri, Elias Kwandikwa, walisema kuwa utekelezaji huo unatokana na agizo la Rais Magufuli alilolitoa Julai 16, mwaka huu baada ya kutembelea bandarini hapo.

"Kufuatia agizo la Rais, tumeanza kutekeleza miradi hiyo ambayo ni pamoja na ukarabati wa meli mbili za Mv. Victoria na Mv. Butiama, ujenzi wa chelezo la kujengea meli mpya ya kisasa yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika Bandari ya Mwanza Kusini, alisema Dk. Chamuliho.

Alisema makontena matatu ya vifaa kati ya 56 yameshawasili katika bandari hiyo, na kwamba hata mengine yako mbioni kuwasili ili kwenda sambamba na kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Miradi hiyo inayotekelezwa na kampuni ya huduma za meli nchini. Rais Magufuli alipotembelea bandarini hapo, alitoa muda kwa wizara hizo mbili pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhakikisha mizigo ya makandarasi iliyokuwa imekwama katika Bandari ya Dar-es Salam kwa takribani siku 30 itolewe na kupelekwa Mwanza.

Mizigo hiyo ilikwama kutokana na changamoto ya msamaha wa kodi ya ongezeko la Thamani (VAT) inayoondolewa bandarini hapo ili kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya kimkakati inafikia malengo yaliyokusudiwa na serikali.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli, ambaye ni msimamizi mkuu wa miradi hiyo, Eric Hamisi, aliahidi kuwa atahakikisha utekelezaji wake unakamilika kwa wakati.

Hamisi alisema kukamilika kwa wakati miradi hiyo kutawasaidia wananchi wa Mwanza, Bukoba na Nansio-Ukerewe wana kuwa na usafiri wa uhakika na salama kupitia Ziwa Victoria.



Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Hisham Hendi, akizungumza na vijana katika sherehe ya maadhimisho ya miaka 20 ya Shirika la AIESEC, Dar es Salaam, juzi. Aliwahamasisha vijana kujiandaa kuwa viongozi wa baadaye na kuchangia katika maendeleo ya nchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shahidi adai alivyomwona mama ubatizo

**INATOKA UK. 10**

alimkuta amefariki.

Wakili wa Jamhuri: Ulijuaje kama amefariki.

Shahidi: Mama mdogo na wakina dada wawili walimpeleka hospitali akarudi dada mmoja nikawasikia wanalia.

Alidai mshtakiwa alikuwa akimpiga Naomi mara kwa mara pamoja na yeye na kwamba alikuwa anawafinya kwa kutumia kisu cha ugali (aliionyesha mahakama makovu mkono wake wa kushoto yaliyotokana na kipigo cha mshtakiwa.

"Mama mdogo alinipiga na ubapa wa kipanga kifupi wakati najikinga kikanikata," alidai shahidi huyo ambaye ni mjomba wa marehemu Naomi.

Alidai kuwa alikwenda kuchukuliwa na askari akanunuliwa chakula, akapelekwa hospitali na baadaye kwenye kituo cha watoto yatima.

Alidai kuwa hakumbuki lini alitoka kwa watoto yatima na kwamba wajukuu wa babu yake walimwonyesha kaburi la Naomi. Akihojiwa na wakili wa utetezi, mahojiano yao yalikuwa kama ifuatavyo:

**Wakili wa utetezi:** Umeshawahi kuona mtu aliyefariki?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili wa utetezi:** Unamfahamu vipi?

**Shahidi:** Anatoa mapovu.

**Wakili wa utetezi:** Ulifahamu kaburi.

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili wa utetezi:** Kaburi ni nini?

**Shahidi:** Shimo lililofukiwa na kuwekwa jeneza la mbao.

Alidai kuwa yeye na Naomi walikuwa wanasoma shule, lakini waliachishwa na kwamba marehemu alikuwa anamwita mshtakiwa bibi.

Shahidi wa pili, Dk. Abdukarimu Hasan (36) kutoka Hospitali ya Rufani Temeke alidai kuwa siku ya tukio mshtakiwa aliongozana na watoto wake wawili, huku akiwa amembeba mgongoni mtoto na mwingine mdogo wa miezi saba akiwa amembeba mkononi.

Alidai anamfahamu mshtakiwa alikwenda ofisini kwake na alipofika kitengo cha dharura kati ya saa 6 na 7 mchana, alionyesha kupaniki na hofu na kwamba alijitambulisha ampeleja mjukuu wake anasumbuliwa na malaria. Alidai mshtakiwa alionekana akiongea 'mwanangu ...mwanangu' lakini bado mtoto alikuwa amemfunga mgongoni.

"Nilimsaidia kumfungua kanga nikamlaza mtoto kitandani, lakini nilipompima vipimo vya awali ikiwamo mapigo ya moyo na kumwangalia macho ya mtoto yalikuwa wazi na mdomo pia," alidai na kuongeza:

"Nilimwangalia mboni za macho zilikuwa wazi akionyesha kwamba amefariki saa zaidi ya nne zilizopita, nilimkagua mwili wake kichwani alikuwa na uvimbe," alidai shahidi.

Alidai alimhoji mshtakiwa mtoto aliyempeleka ni mgonjwa au la, alimjibu kwamba alikuwa kazini akapigiwa simu amepata malaria imepanda kichwani akaanza kuweweseka ndipo akarudi na kumpeleka hospitali hapo. "Nilimkagua mtoto kichwani alikuwa ana uvimbe mkubwa mwilini alikuwa na makovu ya zamani na mengine mapya yaliyokuwa yanatiririsha maji, mkono wa kulia alikuwa umevunjika mara mbili na bega lilikuwa limeteguka," alidai Dk. Hassan hali iliyosababisha mshtakiwa kuinamia chini kwa huzuni.

Alidai alipomhoji mshtakiwa kuhusu taarifa yake ya kumpeleka mgonjwa wakati akijua ni mwili wa marehemu alijibu kwa jeuri kwamba mtoto anaumwa malaria imepanda kichwani akiwa shuleni.

Dk. Alidai inasikitisha kwa sababu mtoto huyo hakuwa na hali ya kwenda shule kutokana na kudhoofika. Katika kesi ya msingi, ilidaiwa Machi 25, 2017, Tuangoma Wilaya ya Temeke jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alimuua mjukuu wake kwa kumpiga.

## Mwanamke ajilipua, aua wengine 30

**ISLAMABAD,** Pakistan

MWANAMKE aliyejitoa mhanga, amejilipua nje ya hospitali moja nchini Pakistan na kusababisha vifo vya watu tisa na kuwajeruhi wengine 30.

Mkasa huo ulitokea wakati majeruhi kadhaa wa shambulio la awali dhidi ya polisi wakiwafikisha hospitalini hapo.

Ofisa Mwandamizi wa Jeshi la Polisi wa Jimbo la Dera Ismail Khan, Salim Riaz Khan (pichani), amesema mtu mwenye silaha aliyekuwa katika pikipiki alifyatua risasi katika makazi ya polisi na kuwaua watu wawili.

Mshambuliaji wa kujitoa mhanga alijilipua katika lango la kuingilia hospitali, na kuwaua polisi wengine wanne na raia wawili. Kundi la wapiganaji la Taliban, limedai kuhusika na shambulio hilo ingawa halijasema kuwa mwanamke ndiye aliyehusika na mashambulizi.

Katika miaka ya hivi karibuni, Jeshi la Pakistan limekuwa likiendesha operesheni kabambe dhidi ya kundi la Taliban na makundi mengine ya wapiganaji katika eneo la mpaka wake na Afghanistan. **DW**



## Boris aendeleza msimamo EU

**LONDON,** Uingereza

BORIS Johnson ambaye anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu wa Uingereza wiki hii, amedhamiria kufanikisha taifa lake kujiondoa katika Umoja wa Ulaya ifikapo Oktoba 31, licha ya upinzani mkali bungeni.

Jonhson, meya wa zamani wa Jiji la London, anatarajiwa kushinda nafasi ya kukiongoza chama cha Kihafidhina na kuchukua nafasi ya Waziri Mkuu, Theresa May.

Baada ya matokeo kutangazwa hapo Jumanne, kura za wanachama 160,000 zinatarajiwa kumwibua Johnson mwenye umri wa miaka 55 dhidi ya Waziri wa Mambo ya Nje, Jeremy Hunt. Duru zinampa Hunt nafasi finyu ya ushindi. **DW**



# Iran sasa yakanusha madai ya Marekani ndege kutunguliwa

**TEHRAN,** Iran

IRAN imetoa picha kwenye vyombo vya habari ikikana madai ya Marekani kuwa imetungua ndege isiyo na rubani ya Iran katika eneo la Ghuba.

Televisheni ya taifa imesema inaonyesha meli za kivita katika eneo hilo, na zilipigwa picha na ndege hiyo hiyo baada ya muda ambao Marekani ilitangaza kuwa ilitungua ndege hiyo.

Pamoja na Iran kukana, Rais wa Marekani, Donald Trump amesema "hakuwa na shaka" ndege isiyo na rubani ilitunguliwa.

Video inaonyesha picha za rangi nyeupe na nyeusi za meli za kivita zikitembea ndani ya maji, ikionyesha muda, tarehe na eneo la kijiografia.

Televisheni ya taifa ya Iran imesema kuwa picha hizo zilichukuliwa na ndege isiyo na rubani inayodaiwa kutunguliwa wakati ikiwa angani usawa wa karibu na meli ya kijeshi ya Marekani.

Jeshi la Iran, ambalo lilichapisha picha za video, limesema picha hizo zilirekodiwa "kabla na hata baada ya Marekani kutoa madai hayo".

Lakini picha hizo zina mashaka, anasema mwandishi wa masuala ya kidiplomasia Paul Adams. Anasema baadhi ya picha zinaonekana kupigwa picha na helikopta ya Iran ambayo ilikuwa pia kwenye eneo hilo.

**Video inaonyesha picha za rangi nyeupe na nyeusi za meli za kivita zikitembea ndani ya maji, ikionyesha muda, tarehe na eneo la kijiografia.**

Rais wa Marekani, Donald Trump, alisema Jeshi la Maji la Marekani limetungua ndege isiyo na rubani ya Iran katika eneo la mpaka kati ya ghuba ya Uajemi na ghuba ya Oman.

Alisema meli ya jeshi lake "ilichukua hatua ya ulinzi" siku ya Alhamisi baada ya ndege hiyo kusogea kwa takriban mita 914 karibu na chombo hicho.

Iran haraka ilitupilia mbali madai ya Trump, huku ofisa mmoja wa juu akisema kuwa huenda walilenga ndege yao wenyewe kimakosa.

Wakati huo huo, sauti zilizorekodiwa zimebaini majibizano makali kati ya wanamaji wa Uingereza na wanajeshi wa Iran waliokuwa ndani ya meli ya kijeshi, muda mfupi kabla ya meli ya mafuta iliokuwa na bendera ya Uingereza kukamatwa katika Ghuba.

Katika sauti hizo, meli ya Iran iliiambia meli hiyo ya mafuta ya Uingereza kwa jina MHS Montrose iwapo ingependelea kuipekua meli hiyo kwa masuala ya kiusalama.

Lakini Balozi wa Iran mjini London aliionya Uingereza dhidi ya kusababisha mgogoro.

Hamid Baeidinejad alisema katika twitter yake kwamba: Hii ni hatari sana na sio busara wakati kama huu katika eneo hilo.

Iran hata hivyo ni imara na iko tayari kwa matukio yoyote.

Waziri huyo wa masuala ya kigeni ameitaka Iran kuiachilia meli hiyo. Anayodai ilikamatwa kwa njia ya haramu. Jeremy Hunt amesema kuwa wabunge wataarifiwa Jumatatu kuhusu hatua zitakazochukuliwa na serikali.

Stena Impero ilikamatwa na wanajeshi wa Iran almaarufu Iranian Revolutionary Guard Ijumaa katika eneo muhimu la maji katika Ghuba.

Meli hiyo ya mafuta ilizingirwa na meli nne na helikopta kabla ya kuelekezwa katika eneo la maji la Iran, amesema Waziri wa mashauri ya kigeni wa Uingereza Jeremy Hunt.

Amesema kuwa "kuhusu usafiri wa majini lazima uimarishwe" na akaonya kuwa itakuwa na "athari mbaya " kama hali haitatatuliwa haraka..

"Hatuangalii hatua za kijeshi," na kuongeza kuwa: "Tunatafuta njia za kidiplomasia za kutatua hali hii." **BBC**



Maofisa wa afya wakisafirisha mgonjwa aliyeambukizwa virusi vya ebola katika kituo cha matibabu cha Butembo nchini Congo. **PICHA: BBC**

# Maandamano ya kushinikiza uchunguzi yaanza Hong Kong

**HONG KONG,** China

MAELFU ya waandamanaji wameanza maandamano mapya katika eneo la wazi yenye lengo la kushinikiza uchunguzi dhidi ya mbinu za polisi katika jimbo la Hong Kong, nchini China.

Wakiwa wamekusanyika katika kipindi cha joto kali, waandamanaji wamevaa mavazi meusi, huku kukiwa na bango kubwa lililoandikwa "Uchunguzi Uhuru kwa Utawala wa Sheria."

Maandamano hayo makubwa ya wapigania demokrasia yalianza mwezi uliopita, kupinga mswaada wa sheria unaotoa ridhaa kwa wakazi wa Hong Kong kushtakiwa China Bara, jambo ambalo wakosoaji wanasema haki zao zinaweza kuathiriwa.

Kiongozi wa jiji hilo alitangaza kuwa muswada huo umesitishwa, lakini waandamanaji wanamtaka ajiuzulu katika wakati ambapo kumekuwa na hofu ya ongezeko la mmomonyoko wa haki za kiraia katika eneo hilo lililo chini ya mamlaka ya China. **DW**

# Serikali yaridhishwa na hali ya chakula

**Na Beatrice Moses**

HALI ya uzalishaji wa mazao ya chakula kitaifa katika msimu wa 2018/2019 utafikia tani 16,408,309 kwa mlinganisho wa nafaka (Grain Equivalent) ambapo nafaka ni tani 9,007,909 na ambazo siyo ni tani 7,400,400.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipozungumza na waandishi wa habari juzi kuhusu hali chakula ilivyo nchini.

Waziri Hasunga alisema kuwa Mei hadi Juni 2019 wizara hiyo ilifanya tathmini ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa 2018/2019 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2019/2020 katika mikoa yote 26 Tanzania Bara kwa lengo kubaini uzalishaji na mahitaji. Hasunga alisema imekuwa na kiwango cha utoshelevu wa chakula kati ya asilimia 120 hadi 125 na imekuwa ikizalisha ziada kati ya tani 2,582,717 hadi 3,322,689 katika kipindi cha miaka mitano mfululizo.

"Ikilinganishwa na msimu uliopita, uzalishaji wa mazao ya chakula umeshuka kwa tani 483,665, ambapo nafaka hususan mahindi yameshuka kwa tani 365,642 na mchele kwa tani 210,454. Aidha, uzalishaji wa isiyo nafaka (non cereals) umeongezeka kwa tani 46,283," alisema.

Alisema uzalishaji wa mazao ya nafaka ulifikia asilimia 103 na mazao yasiyo ya nafaka yalifikia asilimia 145, hivyo uzalishaji wa jumla wa mazao ya nafaka na yasiyo ya nafaka ulifikia asilimia 119.

"Katika kufanya tathmini ya hali ya chakula, hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula na usalama wa chakula tunaangalia baadhi ya mazao muhimu yanayohitajika zaidi kama vile mahindi, mtama na ulezi, mchele, mikunde, ngano, ndizi, muhogo na viazi," alisema.

Waziri huyo alibainisha kuwa mchango wa uzalishaji wa mazao ya chakula kitaifa katika msimu wa 2018/2019 unaonyesha kuwa mahindi yamechangia kwa asilimia 35, muhogo kwa asilimia 17, mchele kwa asilimia 12, viazi kwa asilimia 10 na mazao mengine.

Alisema hali ya uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula nchini imeendelea kuwa nzuri katika kipindi cha miaka mitano mfululizo kufuatia uzalishaji wa ziada wa mazao ya chakula kuanzia msimu wa kilimo wa 2013/2014 hadi 2017/2018 ambapo kwa msimu wa 2018/2019 nchi imejitosheleza ikilinganishwa na mahitaji.

Waziri aliwataka wananchi wote nchini kuzalisha mazao ya chakula kwa kuzingatia kanda za kiekolojia, kuwa na hulka ya kuhifadhi chakula kulingana na mahitaji ya kaya.

Aidha, wakulima waliopata chakula cha ziada wanashauriwa wasiharakishe kuuza mazao yao mapema bali wasubiri hadi bei zitakapokuwa nzuri ndipo wauze na kwa wale wenyewe waliopata utoshelevu kidogo wa chakula watumie vizuri mazao hayo kwa ajili ya chakula na si vinginevyo.

## Alat yapigwa jeki mil. 750/- mkutano mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetoa Sh. milioni 750 kwa ajili ya mikutano mikuu ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa (ALAT), kwa miaka mitano mfululizo huku ikiahidi kuendelea kushirikiana na serikali za mitaa nchini kutatua changamoto mbalimbali.

Ofisa Mkuu wa Wateja Wadogo na wa Kati, Filbert Mponzi, aliyasema hayo mwishoni wa wiki, jijini Mwanza wakati akikabidhi udhamini wa benki hiyo kama mdhamini mkuu wa mkutano mkuu wa mwaka wa ALAT unaoanza leo, jijini Mwanza.

Mponzi alisema benki hiyo inatambua uhusiano wa kibiashara uliopo kati ya NMB na ALAT kupitia zaidi ya halmashauri 180 na inashirikiana kukusanya mapato ya serikali huku taasisi hiyo ikiwa mmbia wa karibu na serikali.

Mwenyekiti wa ALAT taifa, Gulamhafeez Mukadam ameishukuru Benki ya NMB kwa kuonyesha kujali serikali za mitaa na mchango wa mwaka huu unaonyesha dhamira na ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili.

Aliiomba pia benki hiyo kuangalia namna ya kuangalia upya misaada yake inayotolewa kwa jamii kupitia uwajibikaji kwa jamii (CSR), akiomba benki kuanza kusaidia jambo ambalo mwisho linakuwa kubwa kuliko misaada midogo ambayo inaweza ikawa na mchango mdogo kwenye jamii.

# 6 hawajaguswa tangu wateuliwe na JPM

INATOKA UK.2

ukurasa wake akimkaribisha Makamba kwenye viti vya kawaida ndani ya Bunge yaani 'Back bench'.

"Rafiki yangu@jmakamba karibu tena back bench tuendelee na kazi. Ulikuwa mbunge bora sana back bench 2010-2012 na ninaamini itakuwa hivyo tena tofauti ya kutawala na kuongoza. Namna ulivyoongoza marufuku ya mifuko ya plastiki ilionyesha falsafa yako ya uongozi ni tofauti sana na falsafa ya serikali yenu ya CCM. Tuna kesho nyingi tupambane kuijenga Tanzania inayojali watu wake na ya kidemokrasia," alisema Zitto.

Katika ukurasa wake, Bashe alitweet kwa kuandika: "Ndugu zangu awali nimshukuru Allah kwa yote. Namshukuru kwa dhati Mh. Rais kwa imani yake, ni jukumu zito nimelipokea kwa uwezo wa Allah tutavuka ni sekta iliyoajiri Watanzania wengi na changamoto nyingi nawashukuru Watanzania na wananchi wa Nzega na kwa dhati chama changu."

**MAWAZIRI AMBAO HAWAJAGUSWA**

Rais Magufuli alianza kazi na Baraza la Mawaziri 19 na Manaibu 18 na ambao hadi sasa wapo kwenye nafasi walizoanza nazo awali ni Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Muhagama.

Wengine ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu. Vile vile, katika uteuzi wake wa kwanza, wizara nne mawaziri wake walipatikana baadaye na baadhi yao wapo kwenye nafasi hizo hadi sasa ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango na Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Dk. Joyce Ndalichako.

Wengine walioanza na Rais na kuhamishiwa kwenye wizara nyingine na bado wapo kwenye Baraza la Mawaziri ni Prof. Makame Mbarawa, aliyeanza kama Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kwa sasa ni Waziri wa Maji.

Dk. Harrison Mwakyembe, alianza akiwa Waziri wa Katiba na Sheria na sasa ni Waziri Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Balozi Dk. Augustine Mahiga, alianza akiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, ambaye kwa mabadiliko ya Machi 4, mwaka huu, aliteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Pia, Waziri Angella Kairuki, alianza akiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, baadaye aliteuliwa kuwa Waziri wa Madini na mabadiliko ya Januari mwaka huu, aliteuliwa kuwa Waziri wa Wizara mpya ya Uwekezaji.

**MANAIBU WALIOPANDA**

Rais Magufuli alianza kazi na manaibu waziri 16 na baadaye waliongezeka na kufika 18, baadhi yao walihamishwa wizara na wengine kuwa mawaziri kamili.

Manaibu waziri waliodumu kwenye nafasi zao bila kubadilishwa ni Stella Manyanya (Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi), Angela Mabula (Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi) na Anthony Mavunde (Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira).

Wengine ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Tate Ole Nasha na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni Yusuph.

Walioanza kama manaibu waziri na sasa ni mawaziri ni Dk. Hamisi Kigwangalla, aliyeanza kama Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, na kwa mabadiliko ya Oktoba 2017, aliteuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, akichukua nafasi ya Prof. Jumanne Maghembe, aliyeondolewa.

Mwingine ni aliyeanza kama Naibu Waziri wa Muungano na Mazingira, Luhaga Mpina, ambaye Oktoba 2017 aliteuliwa kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Medard Kalemani alianza kama Naibu Waziri wa Nishati na Madini, ambayo ilikuwa nafasi ya Prof. Sospeter Muhongo, aliyejiuzulu Mei 24, mwaka 2017, baada ya ripoti ya kamati ya kuchunguza masuala ya kisheria na kiuchumi kuhusu mchanga wa madini unaosafirishwa nje maarufu kama makinikia, na katika hotuba yake Rais Magufuli alimtaka Prof. Muhongo kujitafakari na ikiwezekana ajiuzulu na alifanya hivyo saa chache baadaye.

Selemani Jafo ambaye alianza akiwa Naibu Waziri wa Tamisemi na kwa mabadiliko ya Oktoba 2017, aliteuliwa kuwa waziri kamili na kupewa manaibu wawili ambao ni Joseph Kandege na George Kakunda.

**WAPYA WALIOINGIA**

Wengine ni Ramol Makani, aliyekuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, ambaye nafasi yake ilichukuliwa na Mbunge wa Vwawa, Japhet Hasunga na kwa sasa inashikiliwa na Constantine Kanyasu, Anastansia Wambura aliyekuwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo, aliyerithiwa na Juliana Shonza.

Pia katika mabadiliko hayo aliteuliwa Kangi Lugola, kuwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ambaye baada ya Mwigulu Nchemba, kuondolewa alipewa Lugola.

Katika mabadiliko hayo, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu iliongezewa Naibu Stella Ikupa kwa ajili ya kushughulikia masuala ya wenye ulemavu. Kadhalika, Novemba mwaka jana aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Charles Tizeba, aliondolewa na aliyekuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Hasunga alipewa nafasi hiyo, huku Kakunda aliyekuwa Naibu Tamisemi alipewa nafasi ya Waziri wa Viwanda na Biashara, akimrithi Charles Mwijage.

Hasunga aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Kilimo akichukua nafasi ya Kanyasu, huku Dk. Mary Mwanjelwa akiteuliwa kuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kabla ya uteuzi alikuwa Naibu Waziri wa Kilimo.

Katika mabadiliko hayo, Mwita Waitara aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Tamisemi, nafasi anayoishikilia hadi sasa.

Mabadiliko mengine yalimwondoa Waziri wa Maji, Mhandisi Gerson Lwenge na kupewa Mbunge wa Katavi, Mhandisi Issack Kamwele, aliyekuwa Naibu Waziri wa wizara hiyo. Manaibu wengine ambao walianza na Rais Magufuli na hawapo kwenye nafasi zao baada ya kuondolewa au kuteuliwa nafasi nyingine ni Dk. Possy Abdallah, aliyeteuliwa kuwa balozi.

Waziri wa kwanza kwenye serikali ya awamu ya tano kutumbuliwa alikuwa Charles Kitwanga, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, aliyedaiwa kuingia bungeni kujibu maswali ya wizara akiwa amelewa.

Vile vile, mabadiliko mengine yalimwondoa aliyekuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Nape Nnauye, aliyeunda kamati ya kuchunguza kuvamiwa kwa kituo cha televisheni Clouds.

Baada ya Dk. Mwakyembe kuziba pengo la Nape, aliteuliwa Prof. Palamagamba Kabudi, kuongoza Wizara ya Katiba na Sheria hadi mwaka huu, alipopelekwa Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa akibadilisha na Balozi Mahiga aliyepelekwa Katiba na Sheria.

**MAWAZIRI WALIONDOLEWA**

Mawaziri walioanza na Rais Magufuli na sasa wamebaki kuwa wabunge ni Mbunge wa Mwanga Prof. Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mtama, Nape, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mwijage, Mbunge wa Misungwi, Kitwanga, Mbunge wa Musoma Vijijini, Muhongo, Mbunge wa Iramba, Mwigulu na sasa ingizo jipya ni Mbunge wa Bumbuli, Makamba.

**MANAIBU WALIONDOLEWA**

Manaibu walioanza na Rais Magufuli na kuondolewa na kubakia kuwa wabunge ni Dk. Susan Kolimba, aliyekuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa.

Pia, katika uteuzi wa jana Rais amemteua Balozi Dk. Martin Lumbanga, kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), ikiwa ni kipindi cha pili.

# SARRI: NAMHUSUDU POGBA



**SINGAPORE CITY,** Singapore

KOCHA wa Juventus, Maurizio Sarri, amebainisha kwamba, anamhusudu kiungo wa Manchester United, Paul Pogba na kwamba angependa kumwona akitua klabuni hapo kipindi hiki cha majira ya joto.

**Majaliwa ya Pogba hapo katika dimba la Old Trafford bado yapo shakani huku kukiwa na uvumi kwamba anataka kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto pale kwenye Ligi Kuu ya England.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 anataka kutafuta changamoto mpya kwa mujibu wa wakala wake, Mino Raiola na sasa Sarri amebainisha hisia zake kwa kiungo huyo raia wa Ufaransa.

Akizungumza kabla ya mchezo wake wa kirafiki dhidi ya Tottenham jana Jumapili hapa Singapore, Sarri alisema: "Nampenda mno, lakini yeye ni mchezaji wa Man United.

"Mimi sio mkurugenzi wa ufundi, hivyo sijui hali jinsi ilivyo."

Inaaminika kwamba, Man United wanataka kiasi cha pauni milioni 150 ili kuweza kumwachia Pogba kipindi hiki cha majira ya joto.

Raiola mapema wiki iliyopita alikoleza moto uvumi wa majaliwa ya Pogba kwa kudai kwamba mipango yake ya kuondoka bado inaendelea kufanyiwa kazi.

# Newcastle yajipanga kumsajili Andy Carroll

**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle itafuatilia kwa karibu maendeleo ya matibabu ya Andy Carroll ambaye ni majeruhi, kwani inafikiria kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto.

Carroll ambaye ni shabiki wa timu hiyo tangu utotoni, aliondoka hapo kwenye uwanja wa St James' Park miaka nane iliyopita, na aliweka rekodi ya kuwa mchezaji ghali zaidi wa Uingereza wakati Liverpool ilipolipa kiasi cha pauni milioni 35 kumsajili.

Lakini kipindi chake cha uchezaji kimekumbwa na majeruhi ya mara kwa mara na msimu uliopita alicheza mechi 14 tu na klabu yake ya West Ham ambapo ulikuwa ni msimu wake wa mwisho.

Manuel Pellegrini alipanga kumpa mkataba mpya Carrolll, lakini sasa Newcastle ipo mbioni kusaka saini yake.

Imeripotiwa kwamba Newcastle wanafuatilia kwa karibu zaidi hali ya Carroll wakati wakiwa kwenye harakati za kuimarisha safu yao ya ushambuliaji.

Wote Salomon Rondon na Ayoze Perez wameondoka klabuni hapo, huku kinda Elias Sorensen akiwa ameanza kwenye kikosi cha kwanza wakati waliposhinda bai 1-0 dhidi ya West Ham kwenye mchezo wa kirafiki wa maandalizi ya msimu mpya barani Asia.

Carroll amefunga mabao 34 katika mechi 142 alizozichezea West Ham tangu alipotua hapo akitokea Liverpool.




# Arsenal yakaribia kumnasa Saliba




**LONDON,** England

ARSENAL inakaribia kumsajili beki wa kati, William Saliba mwenye umri wa miaka 18 kutoka klabu ya Saint-Etienne kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 27.

Mfaransa huyo kesho Jumanne anatarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya yake tayari kujiunga na miamba hao kutoka London Kaskazini, kabla ya kurudi tena Ufaransa kwenye klabu ya Ligue 1 kucheza kwa mkopo wa muda mrefu. Saliba alicheza mechi 16 wakati alipojumuishwa kwenye kikosi cha kwanza Septemba mwaka jana.

Licha ya Arsenal kuwa mwenye matatizo katika safu yake ya ulinzi, wameamua kumpeleka kwa mkopo kinda huyo kwa sababu hatakuwa na nafasi ya kucheza mara kwa mara chini ya kocha, Unai Emery msimu ujao.

Anaachiwa kurudi kule Saint-Etienne kucheza kwa mkopo ili apate uzoefu zaidi na kujiimarisha yeye mwenyewe.

Rais wa Saint-Etienne, Roland Romeyer amedai kwamba, mchezaji mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kuendelea kucheza kwa mwaka mmoja zaidi hapo katika dimba la Geoffroy-Guichard.

Uamuzi wa Arsenal kumrudisha kinda huyo kwa Saint-Etienne kwa mkopo, kutampa nafasi ya kujiweka sawa na kujiandaa vizuri zaidi kabla ya kutua kwenye Ligi Kuu ya England kipindi kijacho cha majira ya joto.

# Pacquiao amchapa Thurman

**LAS VEGAS,** Marekani

BONDIA Manny Pacquiao raia wa Ufilipino amefanikiwa kumpiga na kumchafulia rekodi ya kutopoteza pambano, aliyekuwa bingwa wa dunia wa masumbwi mkanda wa WBA uzito wa Welter, Keith Thurman.

Pacquiao alishinda kwa pointi 115-112 dhidi ya 114-113 za Thurman.

Pacquiao ambaye ana umri wa miaka 40, alianza mapema kuwaamsha mashabiki wake baada ya kumwangusha Thurman katika raundi ya kwanza kwenye pambano hilo lililofanyika kwenye ukumbi wa MGM Grand Garden Arena usiku wa kuamkia jana.

Bingwa huyo wa masumbwi ambaye pia ni mbunge nchini kwake aliendeleza ubabe katika raundi tano za mwanzo, lakini Keith alirejea kuanzia raundi ya sita ya pambano na ikawa piga nikupige.

Hata hivyo, pambano hilo lililoziweka roho za mashabiki juu wakati wote lilimalizika katika raundi ya 12 na uamuzi wa jopo la majaji watatu lilimtaja Pacquiao kuwa mshindi.

Ushindi huo unaandika historia ya aina yake kwa Pacquiao ambaye wengi walikuwa wanamshauri kuachana na masumbwi kutokana na kuwa na umri mkubwa na majukumu ya kisiasa.

Pia, utaandikwa kwenye historia ya masumbwi kwa kuzingatia kuwa amempiga kijana machachari mwenye umri wa miaka 30 aliyekuwa anatajwa kwenye orodha ya wapiganaji bora zaidi watano duniani.

Keith, sasa anaandika rekodi ya kushindwa kwa mara ya kwanza na kupigwa chini kwa mara ya kwanza ulingoni akiwa na rekodi ya kushinda mara 29, kupigwa mara moja na ushindi wa KO mara 22.





# DE GEA AKUBALI KUTIA SAINI MIAKA SITA MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

DAVID de Gea anapanga kutia saini mkataba mpya wa miaka sita na Manchester United ambao utamfanya kupokea mshahara wa pauni 375,000 kwa wiki, na hivyo kuwa golikipa anayelipwa zaidi duniani.

Mhispania huyo alikuwa amebakiwa na miezi 12 tu kwenye mkataba wake wa sasa na alikuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka klabuni hapo kipindi hiki cha majira ya joto.

Hata hivyo, kwa mujibu wa gazeti la The Telegraph, atasaini mkataba wa miezi sita mara tu Man United itakaporudi kutoka kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya, na kumaliza uvumi ulioenea kwamba anaondoka hapo Old Trafford.

De Gea hapo awali alikaribia kuondoka United, huku mashetani Wekundu hao wakilazimika kumwongezea mkataba wa mwaka mmoja ili kuepusha mchezaji huyo kuondoka akiwa huru kipindi hiki cha majira ya joto.

Klabu za Real Madrid, Juventus na Paris Saint-Germain zilikuwa zikitajwa kuwania saini yake, lakini sasa kocha, Ole Gunnar Solskjaer ameonekana kulimaliza hilo.

Inaaamini kwamba, De Gea alikuwa na nia ya kubakia hapo United, lakini alitaka aongezewe mshahara kumfikia Alexis Sanchez ambaye analipwa pauni 350,000 kwa wiki, kitu ambacho awali kilionekana kuwa kigumu.

Mkataba huo sasa utamfanya kuingiza kitita cha pauni milioni 117 kwa kipindi cha miaka sita na itakuwa ahuweni kubwa kwa Solskjaer, ambaye anapigana kukiimarisha kikosi chake msimu huu.

# *Kante arudishwa ziara ya Chelsea*

**TOKYO,** Japan

N'GOLO Kante amerudishwa nyumbani kutoka katika ziara ya Chelsea ya maandalizi ya msimu mpya nchini Japan baada ya kuwa na hofu kwamba anaweza kutonesha majeraha yake.

Kante atarudi jijini London kuendelea kutibiwa majeraha yake ya goti aliyoumia wakati wa maandalizi ya mchezo wa fainali ya kombe la Ligi ya Europa mwishoni mwa msimu uliopita.

Kocha Frank Lampard alimchukua kwenye ziara hiyo kwa matumaini kwamba angekuwa sehemu ya mchezo wa kirafiki dhidi ya Barcelona kesho Jumanne.

Kante alifanya mazoezi na kikosi cha kwanza wiki iliyopita, lakini hakuwapo kwenye mazoezi ya jana Jumapili.

"Mimi sio daktari, lakini nimekuja na wachezaji wengi ambao hawajalala tangu tutue hapa," alisema kocha huyo wa Chelsea.

"Tumelazimika kumrudisha nyumbani kwa maelekezo ya daktari ili akaendelee kujiuguza, maana huku anaweza kuwa kwenye wakati mwingine mgumu, hivyo tumeamua arudi nyumbani."



# DONDO SOKA
## MAGAZET ULAYA




# ZIDANE ATHIBITISHA BALE KUONDOKA REAL

Abainisha ataondoka haraka ndani ya saa 24 au 48, lakini...

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amebainisha kwamba, Gareth Bale anakaribia kuondoka hapo katika Klabu ya Real Madrid baada ya nyota huyo wa kimataifa wa Wales kuukosa mchezo wa kirafiki dhidi ya Bayern Munich juzi Jumamosi.

**Bale amekuwa hana nafasi pale katika dimba la Santiago Bernabeu, lakini hakuna timu ambayo imeonyesha nia ya kutaka kumsajili, huku yeye mwenyewe akikataa ofa ya kwenda kucheza soka nchini China.**

Manchester United imekuwa ikihusishwa na mpango wa kumsajili mshambuliaji huyo kama ilivyokuwa kwa vipindi vingine vya majira ya joto, huku pia Tottenham na Bayern zikitajwa kuwania saini yake.

Sasa Zidane amenukuliwa na Goal.com akithibitisha kwamba Bale hakuwapo kwenye mchezo huo wa kirafiki waliofungwa 3-1 na mabingwa hao wa Bundesliga kwa sababu anakaribia kuondoka klabuni hapo.

Alisema: "Bale hakucheza kwa sababu anakaribia kuondoka.

"Tuna matumaini ataondoka hivi karibuni, litakuwa jambo bora kwa kila mmoja. Tunafanyia kazi uhamisho wake kwenda timu mpya."

Zidane alibainisha sababu ya Bale kuondoka ni muda wa mabadiliko na uamuzi wa mchezaji huyo wa zamani wa Tottenham kuondoka ulifanywa na yeye.

Aliongeza: "Sina tatizo lolote la kibifansi na yeye, lakini kuna wakati mambo yanatakiwa kubadilika kwa sababu yanatakiwa kufanyika, nimefanya maamuzi, tunatakiwa kubadilika.

"Kundoka kwake ni maamuzi ya kocha, na pia kwa mchezaji, ambaye anajua hali halisi.

"Hali itabadilika, najua ndani ya saa 24 au 48, lakini itatokea, na ni jambo zuri kwa kila mmoja."

Bale amekuwa na wakati mgumu hapo Real, huku akikabiliwa na majeraha ya mara kwa mara, lakini bado aliisaidia klabu kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nne, La Liga moja, Copa del Rey na Supercopa de España.

## ZISIKUPITE

### ATAKIWA ARSENAL, EVERTON

KLABU ya Everton ipo tayari kuipa changamoto Arsenal kumwania mshambuliaji wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, ambaye anauzwa na klabu yake ya Crystal Palace kwa kitita cha pauni milioni 80. ***(Evening Standard)***

### MATUIDI AGEUKA KUWA LULU

TIMU za Manchester United, Everton na Paris St-Germain zimefanya mazungumzo ya awali na klabu ya Juventus kuhusu uwezekano wa kumsajili beki wake, Blaise Matuidi. ***(Le Parisien)***

### MAN UTD KUMNASA VIC-SAVIC

KLABU ya Manchester United imeongeza jitihadi za kutaka kumsajili kiungo mbunifu wa timu ya Lazio ya Italia, Sergej Milinkovic-Savic ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Serbia**.** ***(Mirror)***

### AZIGONGANISHA SURS, W. HAM

TOTTENHAM Hotspurs wameingia kwenye mbio moja na West Ham za kumwania, Diego Llorente mwenye umri wa miaka 25 ambaye anakipiga pale katika klabu ya Real Sociedad. ***(El Mundo Deportivo)***

### ANUKIA WOLVERHAMPTON

TIMU ya Wolverhampton Wanderers inataka kumsajili mshambuliaji wa Italia na AC Milan, Patrick Cutrone ambaye anatajwa kuwa na thamani ya takriban pauni milioni 20. ***(Express & Star)***

### PALACE YATANGAZA DAU

CRYSTAL Palace imetangaza dau la pauni la milioni 8 la kutaka kumsajili kiungo wa Everton, James McCarthy ambaye naye ameonyesha nia ya kutaka kuondoka klabuni hapo. ***(Sky Sports)***

### AWAKATA MAINI EVERTON

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amemaliza matumaini ya Everton kwa kumsajili, Kurt Zouma ambaye aliutumia msimu uliopita akiwa pale Goodison Park kwa mkopo. Everton walikuwa na matumaini ya kuendelea kumtumia mchezaji huo kwa msimu ujao wa Ligi Kuu. ***(Mirror)***

### DZEKO KUONDOKA AS ROMA

NYOTA wa AS Roma, Edin Dzeko mwenye umri wa miaka 33, huenda akaondoka klabuni hapo baada ya kucheza kwa misimu mitatu, huku Inter Milan ikiwa na mpango wa kupata saini ya mchezaji huyo kwa kitita cha pauni milioni 15.***(Sky Sports)***

### KINDA WA CHELSEA ATIMKA

MCHEZAJI kinda wa Chelsea, Ethan Ampadu, 18, amefanya vipimo vya kiafya kabla ya kuhamia katika timu ya RB Leipzig ya Ujerumani. ***(Sky Sports)***

### TAU ATAKIWA UBELGIJI




KLABU ya Brugge ya Ubelgiji ina mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Brighton na Timu ya Taifa ya Afrika Kusini, Percy Tau, aliyecheza michuano ya Kombe la Mataifa Afrika. ***(Daily Mail)***

## HABARI MICHEZO

# Adadi ahimiza vijana kujikita kwenye vipaji

**Na Steven William,** MUHEZA

MBUNGE wa Jimbo la Muheza, Balozi Adadi Rajabu, amewataka vijana kujikita zaidi kwenye vipaji vyao hasa vya mpira wa miguu, kwani mchezo huo kwa sasa ni ajira kubwa.

Adadi alisema hayo juzi wakati wa kufungwa kwa michuano ya kombe la Adadi ambayo ilizishirikisha timu 19 kutoka Tarafa ya Ngomeni wilayani Muheza mkoani Tanga.

Alisema kuwa katika ligi hizo washindi wamekuwa wakipewa zawadi ya fedha, ng'ombe, jezi na mipira kwa lengo kubwa kutoa motisha katika timu hizo zilizoingia fainali.

"Naamini ligi hii itaweza kuibua vipaji vya vijana wetu ambao baadaye wataweza kuchukuliwa na timu kubwa katika Ligi Kuu Tanzania Bara na wengine hata kuuzwa nje ya nchi," alisema Adadi.

Alisema tayari kuna vijana wameshachukulia na timu kubwa ikiwamo Yanga, Coastal Union, Simba na KMC ya Kinondoni jijini Dar ambapo wamepata ajira.

Fainali ya michuano hiyo ilizikutanisha timu ya Mjesani FC na Kicheba Center.

# Ofisa michezo Temeke ataka kurejeshwa riadha

**Na Shufaa Lyimo**

OFISA Michezo Wilaya ya Temeke, Ingridy Kimario, amewataka wadau mbalimbali kuuendeleza mchezo wa riadha mbio fupi ili urejee kama ilivyokuwa miaka iliyopita.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam ndani ya Uwanja wa Taifa alipokuwa mgeni rasmi wa mashindano ya kukimbia mbio fupi za mita 100, 200 na 400, Kimario alisema anawashukuru waandaji kwa kukaa na kuamua kufanya mashindano hayo.

"Kwa kweli nimefurahi kila kijana ameweza kuonyesha kiwango chake ingawa kwa sasa hivi mchezo wa kukimbia mbio fupi haupo," alisema.

Aidha, alisema atahakikisha anafanya juhudi kwa kushirikiana na serikali kufufua mchezo huo na kuwataka vijana waongeze juhudi ya kufanya mazoezi.

"Wachezaji wasikate tamaa waongeze juhudi ya mazoezi ili waweke miili yao fiti kwa sababu bado wana nguvu," alisema.

Kwa upande wa mwandaaji wa mashindano hayo, Mossy Ally anayeishi nchini Norway alisema ameamua kuandaa mashindano hayo baada ya kuona mchezo huo umekufa.

"Nimekereketwa kuona michezo mingine inadumishwa lakini huu wa kukimbia mbio fupi hauthaminiwi," alisema Mossy.

Washindi wote walipewa zawadi za fedha.

# ZFF YAFANYA MABADILIKO KANUNI ZA MASHINDANO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF) limefanya mabadiliko madogo ya kanuni ya kuendesha mashindano ya mwaka 2019/2020.

Kwa mujibu wa barua iliyosainiwa na Katibu Mkuu wa Shirikisho hilo, Mohammed Ali Hilal inaonyesha kuwa mabadiliko ya kanuni hayo yamefanywa katika kifungu namba 7, kifungu kidogo cha kanuni I, II, III na IV.

**Barua hiyo alisema kuwa kufanyiwa marekebisho ya kifungu hicho kitakuwa kimekufa kama kilivyokuwa kinaonekana katika kanuni ya kuendesha mashindano ya mwaka huu.**

Alisema kuwa katika mabadiliko hayo sasa daraja la Vijana la Juvinile umri wa wachezaji utakuwa chini ya miaka 13 na 15 na mashindano ya daraja hilo yatasimamiwa na chama cha soka wilaya husika.

Kwa daraja la Junior umri wa wachezaji utakuwa chini ya miaka 15 na 17 na mashindano yake yatasimamiwa na chama cha soka mkoa husika.

Aidha, daraja la Central umri wa wachezaji utakuwa ni chini ya miaka 21 na mashindano yake yatasimamiwa na Shirikisho la Soka Zanzibar ZFF.



Wanamitindo wakipita mbele ya hadhara kuonyesha mavazi ya vitenge yaliyobuniwa na mbunifu wa mitindo Tanzania, Ally Rehmtullah kwenye maonyesho ya wazi ya vazi la kitenge maarufu kama "Vitenge Vyetu Ufahari Wetu" yaliyoandaliwa na mbunifu huyo kwa kushirikiana na kampuni ya Flygle and Hightech Wear, yaliyofanyika juzi kwenye viwanja vya Mnazi Moja jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Simiyu, Dodoma, Arusha wang'ara selebuka*

**Na Renatha Msungu,** SONGEA

MWENDESHA baiskeli kutoka Simiyu, Masunga Duba, ameendeleza ubabe katika Tamasha la Majimaji Selebuka 2019 baada ya kutetea ushindi alioutwaa mwaka jana.

Katika mbio hizo za baiskeli kwa afya zilizoanzia Makumbusho ya Mashujaa wa Vita vya Majimaji hadi eneo la Liganga kisha kurejea, ikiwa ni umbali wa kilomita 100, Masunga alishinda akitumia saa 2:50:43 akiboresha muda alioutumia mwaka jana wa saa 2:53:05.

Nafasi ya pili pia ilikwenda mkoani Simiyu kwa Boniphace Masunga aliyetumia saa 2:51:01 huku nafasi ya tatu ikinyakuliwa na Denis Julias kutoka Arusha saa 3:15:00.

Masunga kwa ushindi huo alijinyakulia kitita cha Sh. milioni 1 na medali ya dhahabu huku mshindi wa pili Boniphace akilamba Sh. 700,000 na medali ya fedha wakati mshindi wa tatu Denis akiondoka na Sh. 500,000 na medali ya shaba.

Mshindi wa nne aliibuka Ombeni Mbiliny wa Iringa aliyetumia saa 3:15:03 na kuzawadiwa Sh. 300,000 na medali ya ushiriki, huku nafasi ya tano ikienda kwa Asso Gadas kutoka Dar es Salaam saa 3:15:41 na kujipoza kwa Sh. 100,000 na medali ya ushiriki.

Ipyana Mbogela kutoka Iringa mshindi wa tatu mwaka jana, aliporomoka hadi nafasi ya sita akitumia saa 3:20:41, nafasi ya saba ikaenda kwa Kwilasa John wa Manyara saa 3:22:45, wa nane Hagai Sanga saa 3:30:53, Elias Tala alitumia saa 3:40:11 huku kumi bora ikifungwa na Abdul Kajenje aliyetumia saa 3:54:22 wote kutoka Mbeya. Washindi wa sita hadi kumi kila mmoja alipata kifuta jasho cha Sh. 50,000 na medali za ushiriki.

Tukio hilo la baiskeli, ndilo lilikuwa la kuhitimisha tamasha hilo ambalo lilikata utepe Julai 13 kwa mchezo wa riadha kwenye Uwanja wa Majimaji mjini hapa.

Akizungumza wakati wa kufunga tamasha la mwaka huu, Mkurugenzi wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Songea Mississippi (So-Mi), ambao ndio waandaaji wa tamasha hilo, Profesa Julian Murchison, alisema lengo la kuanzishwa kwa tamasha hilo ni kuinua vipaji na fursa mbalimbali mkoani Ruvuma na ndio maana wamekuwa wakilifanya kila mwaka.


"Tamasha hili tuna malengo mbalimbali, tunataka kuinua vipaji hususani kwa vijana mkoani Ruvuma, kutoa fursa na pia kujenga mahusiano bora kati ya mji mkuu wa Ruvuma, Songea na Mississippi kupitia mahusiano haya tunabadilishana mawazo ya kujenga vitu mbalimbali," alisema Profesa Julian.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Tamasha hilo, Nathan Mpangala, alisikitishwa na wenyeji kutojitokeza mwaka huu kwenye mchezo huo tofauti na misimu minne toka lianzishwe tamasha hilo.

# Michezo

Jumatatu Julai 22, 2019

Nipashe

Zidane athibitisha Bale kuondoka Real UKURASA 30



Nyota wa Real Madrid, Eden Hazard, akimtoka Corentin Tolisso wa Bayern Munich (kushoto) wakati wa mchezo wa kirafiki baina ya timu hizo mbili uliopigwa mjini Houston nchini Marekani juzi. Bayern iliibuka na ushindi wa mabao 3-1. **PICHA NA MTANDAO**

## Mazoezi ya Yanga Moro dozi nzito

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Yanga umesema mazoezi wanayoendelea kufanya wachezaji wake mkoani Morogoro ni ya aina yake kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Frederick Mwakalebela alisema kuwa msimu ujao hawatakuwa na muda wa kupoteza, zaidi ya kutoa dozi tu.

"Msimu ujao tutaingia na nguvu mpya uwanjani, ndio maana tukajificha Morogoro ili tufanye mazoezi yetu sehemu tulivu," alisema Mwakalebela.

Aidha, Mwakalebe aliongeza kuwa hadi sasa wachezaji wote wanaendelea vizuri, wakiwa na morali ya juu tayari kwa ajili ya msimu ujao.

"Wachezaji wetu wanaendelea vizuri na mazoezi ya nguvu nina imani msimu ujao tutashika nafasi ya juu," alisema.

Alisema wamesajili vifaa vya aina yake vitakavyoleta mafanikio ndani ya klabu hiyo kongwe hapa nchini.

Yanga inafanya mazoezi yake kwenye uwanja wa Chuo cha Biblia, kilichopo eneo la Bigwa mkoani Morogoro.

# Simba kuanza kazi Sauzi

### ●●● Kesho itashuka dimbani kwa mchezo...

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Simba kesho Jumanne itaanza rasmi kujifua kwa kucheza mechi yake ya kwanza ya kujipima nguvu dhidi ya timu ya Chuo Kikuu cha Orbit Tvet mjini Rusternburg nchini Afrika Kusini.

**Simba ambayo inanolewa na kocha, Patrick Aussems imeweka kambi yake nchini humo kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu pamoja na michuano ya kimataifa.**

Kwa mujibu wa orodha ya mechi nne za kujipima nguvu iliyotolewa na Simba, itaanza na timu hiyo inayoshiriki ligi ya chini Afrika Kusini kesho Jumanne.

Mechi nyingine ni dhidi ya Platinums Stars ya Rusternburg itakayopigwa Jumatano, ikifuatiwa na ile dhidi ya Township Rollers ya Botswana itakayochezwa Julai 27 na Orlando Pirates ya Johannesburg itakayopigwa Julai 30 mwaka huu.

Simba imefanya usajili wa wachezaji wapya kwa ajili ya kuboresha kikosi chake, wakiwa na nia pia ya kuhakikisha wanatetea ubingwa wao wa Ligi Kuu msimu ujao.

Simba imesajili wachezaji 11 wapya, ambao ni kipa Beno David Kakolanya, beki Gardiel Michael Mbaga na kiungo Ibrahim Ajibu Migomba wote kutoka Yanga SC, ambao kwa pamoja na beki wa kati, Kennedy Wilson Juma kutoka Singida United na Miraj Athumani kutoka Lipuli wanafanya idadi ya wachezaji watano wazawa wapya Msimbazi hadi sasa.

Wengine sita wote ni wa kigeni, Wabrazil mabeki, beki Gerson Fraga Vieira ATK ya Ligi Kuu ya India na Tairone Santos da Silva kutoka klabu ya Atletico Cearense FC, mshambuliaji, Wilker Henrique da Silva kutoka Bragantino, zote za daraja la nne nchini Brazil na viungo Mkenya, Francis Kahata Nyambura, Msudan Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman na winga Deo Kanda kutoka TP Mazembe ya kwao, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Pamoja na kusaini wachezaji wapya, Simba SC pia imewapa mikataba mipya wachezaji wake kadhaa wa msimu uliopita, wakiwamo kipa Aishi Manula, mabeki Erasto Nyoni, Shomari Kapombe, Nahodha Msaidizi, Mohammed Hussein 'Tshabalala, Muivory Coast, Serge Wawa Pascal viungo Jonas Mkude, Mzambia Clatous Chama na washambuliaji Nahodha Mkuu, John Bocco na Meddie Kagere raia wa Rwanda.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002